Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TISA

**Kikao cha Tisa – Tarehe 9 Novemba, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZLIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:-**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa Mwaka 2006.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 114

**Posho mbalimbali kwa Watumishi wa Afya**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD (K.n. y. MHE. DIANA M. CHILOLO)** aliuliza:-

Kwa kuwa watumishi wa hospitali ya Mkoa wa Singida na Wilaya zake kwa maana ya Madaktari, Wauguzi na watumishi wengine wamekuwa wakitumikia Serikali bila kupewa posho zao za *extra-duty*, muda wa ziada wa kazi, posho ya mazingira magumu, posho ya safari na kadhalika.:-

(a) Je, Serikali inazo takwimu za watumishi na fedha wanazodai kwa Mkoa wa Singida na kwa nchi nzima?

(b) Kama jibu katika sehemu (a) ni ndiyo. Je, ni lini Serikali itamaliza kazi ya kulipa madeni yaliyopitwa na wakati?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa madeni mbali mbali ya watumishi wa Umma wakiwemo watumishi wa Afya ikiwa ni pamoja na watumishi wa hospitali ya Mkoa wa wa Singida.

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo katika ofisi yangu, hadi kufikia Juni, 2007, jumla ya shilingi bilioni 2.1 ni madeni mbali mbali ya watumishi wa afya yakiwemo malimbikizo ya likizo, ada za masomo, kufanya kazi kwa muda wa ziada, uhamisho na gharama za matibabu.

Watumishi wa afya wa Mkoa wa Singida wapatao 529 wanaidai Serikali malimbikizo yenye kufikia shilingi milioni 95.7/= ambapo shilingi milioni 34.1/= ni madai ya watumishi wa hospitali ya Mkoa wa Singida, shilingi 32,472,302/= Halamashauri ya Wilaya ya Singida, shilingi 20,501,117/= Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, shilingi 4,478,000/= Halamashauri ya Manisapaa ya Singida na shilingi 3,113,000/= Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kipindi cha Februari, 2007 ilifanya uhakiki wa madai mbali mbali ya walimu na tayari madai yaliyobainika yamewasilishwa Hazina kwa hatua za malipo. Mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kuwa madai ya watumishi wote yanalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Halamashauri zimeanza kutekeleza agizo la kulipa madeni. Kwa mfano; Halamashauri ya za Mkoa wa Dar es salaam, Iringa, Dodoma, Mtwara na Rukwa ambazo zimefanikiwa kulipa madeni yote ya watumishi wake. Halmashauri ambazo hazijaanza kutekeleza agizo hili na bado zinadaiwa na watumishi wa Idara ya Afya ni za Mikoa ya Pwani, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Shinyanga na Manyara. Aidha, Serikali inakusudia kufanya uhakiki wa madeni ya watumishi wengine wakiwemo watumishi wa Afya kama ilivyofanya kwa walimu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kuwa madai ya watumishi wote yanalipwa. Katika kuhakikisha kuwa mkakati huu unatekelezeka , Halmashauri zote zimeagizwa kutenga katika Bajeti zake fedha kwa ajili ya kulipa madai ya watumishi ili kuepuka malimbikizo ya madeni. Aidha, Serikali inatarajia kufanya zoezi la uhakiki wa madai ya watumishi wa Afya kama ilivyofanya kwa madeni ya walimu.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana! Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa malimbikizo haya yanayoonekana yanakuwa mengi na hasa huko Mkoani Singida, yanasababisha na yanaleta kisingizio kwa hawa wafanyakazi na pia wanashusha morali ya ya utendaji wao wa kazi. Je, sasa Wizara haioni ipo haja sasa ili morali ipande kwa hawa wafanyakazi, walipe haya madeni na ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba Serikali inafahamu kwamba kuna tatizo la malimbikizo ya madeni kwa watumishi mbali mbali na ndiyo maana imeanza kufanya uhakiki. Uhakiki wa kwanza ni kwa walimu. Tumefanya hivyo kwa sababu walimu wana malimbikizo mengi sana na baada ya kufanya hivyo ndipo tulipotambua kwamba hata watumishi wa afya nao wana malimbikizo mengi sana. Kwa hiyo, sasa hivi hili zoezi tumeishaanza kuwaambia Ma-*RAS* wote katika Mikoa yote, kuleta yale malimbikizo ya watumishi mbali hasa watumishi wa afya na baadhi yao wameleta na sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tutahakikisha kwamba tunatuma watu wetu katika Halmashauri mbali mbali kuhakikisha kwamba madeni haya yanahakikiwa na mwishowe yanawekwa kwenye Bajeti ili tuweze kuwalipa. Kwa hiyo, naomba wafanyakazi wote wasipunguze morali kwa ajili ya kutolipwa malimbikizo yao. Serikali itahakikisha kwamba inalipa madeni yote. Haitamwonea mtumishi yeyote iwapo madeni hayo yatahakikiwa.

Na. 115

**Sifa za Msingi za Ajira ya Maafisa na**
**Watendaji wa Tarafa**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO (K.n.y. MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Maafisa Tarafa na Watendaji wa Tarafa ni watu muhimu sana katika kubuni, kuandaa na kusimamia miradi ya wananchi:-

Je, sifa za msingi za ajira ya Watendaji hao ni zipi na hali ikoje kiutendaji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mhehimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muundo wa Utumishi, hakuna cheo cha Watendaji wa Tarafa, bali Maafisa Tarafa. Maafisa Tarafa ni watu muhimu sana katika kubuni, kuandaa na kusimamia miradi ya wananchi. Majukumu ya Maafisa Tarafa yameelezwa vizuri katika Waraka wa Utumishi Na. 01 wa Mwaka 1998 unaohusu taratibu za kiutendaji katika Muundo wa Tawala za Mikoa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa za kuingilia kazini moja kwa moja kwa Maafisa Tarafa ni kuajiri Wahiimu kuanzia Shahada/ Stashahada ya Juu katika mojawapo ya fani za Sheria, Menejimenti, Utawala au Sayansi ya Jamii kutoka Vyuo mbali mbali vinavyotambuliwa na Serikali.

Aidha, sifa za kuingia Maafisa hao ni Maafisa waliyomo kazini i kubadilishwa cheo kuwa Maafisa Tarafa *(Recategorization)*. Maafisa hawa huwa na sifa za ziada kama vile uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitano mfululizo na wenye utendaji mzuri wa kazi kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma.

Hali ya kiutendaji ya Maafisa Tarafa hao kwa sasa ni nzuri ingawa huko nyuma kulikuwepo na tatizo la kiutendaji hasa wakati Afisa Tarafa alipotaka kutekeleza majukumu yake.

Tatizo hili lilitokana na Afisa Tarafa kuwa ni Msaidizi wa Mkuu wa Wilaya ambao wote ni watumishi wa Serikali Kuu. Maeneo ambayo Afisa Tarafa alitakiwa ayasimamie ili aweze kutekeleza kazi zake za kisheria ni katika maeneo ya Kata na Vijiji ambavyo vyote vipo chini Halmashauri za Wilaya au za Mitaa.

Kwa mantiki hii ni kwamba Afisa Tarafa alisimamia maeneo ya watumishi ambao hawakuwa chini yake kiutendaji au kwa maana nyingine hawakuwajibika kwake. Hali hii ilifanya utendaji wake kuwa mgumu. Tatizo hili kwa sasa limepatiwa ufumbuzi baada ya Serikali kuamua kwamba Maafisa Tarafa waundiwe Muundo na utaratibu chini ya Utumishi wa Umma utakaowafanya wawajibike kwa Mamlaka ya Serikali Kuu na pia kuwajibika kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Maafisa Tarafa kuwa Watumishi wa Serikali Kuu kwa upande mmoja, kumechukuliwa kama ni kuzipunguzia Serikali za Mitaa mzigo. Tatizo lililokuwa likijitokeza ni kuwa Maafisa Tarafa wamekuwa wakitumika kama wanasiasa. Lakini, kwa kufuata Waraka wa Utumishi Na. 01 wa mwaka 2000, sasa kada ya Maafisa Tarafa haitakuwa tena ya kisiasa na hawataruhusiwa kujihusisha na shughuli za kisiasa kama hapo awali.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kujua Maafisa Tarafa wanajiriwa kwa sifa za utaalamu mbali mbali, lakini kazi ya Afisa Tarafa kwa vitendo ni tofauti na hizo sifa.

Je, kuna mafunzo maalum ambayo yameandaliwa kwa ajili ya watu hawa ili waweze kutenda kazi zao vizuri kama ilivyokuwa inafanywa siku zilizopita kule Ukiliguru?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwa watumishi wengine wanapoajiriwa mara ya kwanza, wanapewa *Induction Course, Orientation* na kwa Maafisa Tarafa ni kawaida kuwafanyia *Induction Course* katika Vyuo mbali mbali. Kwa hiyo, mafunzo yanatolewa ili waweze kujua wajibu wao na kazi zao.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa, Maafisa Tarafa ni waajiriwa wa Serikali Kuu na kwa kuwa kada wanayofanya nayo kazi kwa maana ya Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata ni waajiriwa wa Halmashauri ambao kimsingi wangekuwa chini yao.

Lakini, kwa sababu ajira ya Afisa Tarafa iko Serikali Kuu, haoni ni wakati mzuri ajira yao ikawa moja kwa moja kwenye Halmashauri ya Wilaya ili utendaji wao ukawa na ufanisi zaidi kuliko ilivyo sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Maafisa Tarafa kama nilivyosema kwamba ni waajiriwa wa Serikali Kuu.

Lakini, pia nimesema kwamba kutokana na Muundo wao kwa sasa hivi, pamoja na kwamba wanaajiriwa na Serikali Kuu, lakini wanafanya kazi za kiutendaji katika Serikali za Mitaa. Tunafahamu kwamba kwa sasa hivi Maafisa Tarafa wanaruhusiwa kisheria kuingia katika vikao mbali mbali vya Halamshauri ili kutoa taarifa katika Tarafa zao kutoka kwenye Vijiji na kutoka kwenye Kata.

Kwa hiyo, ni nia ya Serikali kwamba hao Maafisa Tarafa wabaki Serikali Kuu, lakini kiutendaji kazi zao nyingi ziko Serikali za Mitaa. Nia ya Serikali ni kuwapunguzia Serikali za Mitaa mzigo mkubwa wa kuwalipa mishahara hao Maafisa Tarafa.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Baada ya majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na mimi ninakubaliana naye kabisa kwamba Makatibu Tarafa wabaki kuwa watumishi wa Serikali Kuu na wala si wa Halmashauri.

Napenda niulize swali la nyongeza. Huko nyuma, Makatibu Tarafa wamekuwa wakipewa usafiri wa pikipiki. Tukaona kwamba mahali pengine maeneo yao ni makubwa sana. Hivi kweli unampa Katibu Tarafa wa Makete, wa Njombe Pikipiki ili aende nayo wapi!

Je, Waziri atakuabaliana na mimi kwamba wakati umefika kwamba Makatibu Tarafa badala ya kukopeshwa pikipiki, sasa wakopeshwe angalau vigari hata viwe vidogo, lakini ili mradi vigari vya magurudumu manne ya *4 wheel drive? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nilijua tu Mzee Malecela ataniulizia hata mimi! *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali hilo, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa John Malecela kwa kustaafu nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na kumpongeza sana Mkewe Mama Anna Malecela kwa kura alizopata katika Halmashauri Kuu ya Taifa.Ni kweli maeneo mengine nchini ni makubwa sana na usafiri wa pikipiki ni vigumu kufanya kazi vizuri. Tutazingatia ushauri huo wa Mheshimiwa Malecela ili tuangalie uwezekano wa kuwapatia Makatibu Tarafa walio katika maeneo magumu, magari kwa ajili ya usafiri katika kufanyia kazi zao. *(Makofi)*

Na. 116

**Kituo cha Kulelea Watoto Yatima**

**MHE. JANET B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa vituo vingi vya kulelea watoto yatima wanaoishi kwenye mazingira magumu na wenye utindio wa ubongo ni vya madhehebu ya dini:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani katika kuvisaidia vituo hivyo kwa hali na mali?

(b) Kama imesaidia. Je, ni kwa mikoa gani na kwa misaada gani?

(c) Je, Serikali inazishirikishaje Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundina Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika kuhudumia vituo hivyo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa vituo vingi vya kulelea watoto walio katika mazingira hatarishi vinaendeshwa na madhehebu ya dini, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali pamoja na watu binafsi. Huduma hii inatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Makao ya Watoto Namba 4 ya mwaka 1968.

Wizara yangu imepewa mamlaka ya kusajili asasi zinazoendesha vituo vya watoto yatima walio katika mazingira hatarishi na kuvipa miongozo ya namna ya kuendesha na kutoa huduma zenye viwango vinavyokubalika. Wizara yangu pia hufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuweza kuwapa ushauri wa kitaalamu juu ya uendeshaji makao hayo. Aidha, Wizara huwashirikisha katika kuwajengea uwezo kuhusu utoaji huduma bora za malezi, matunzo na ulinzi kwa lengo la kuboresha huduma zinazotolewa katika vituo hivyo. Hadi sasa yapo makao 78 yaliyosajiliwa ambayo yanahudumia watoto 1736.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya masharti ya kuanzisgha na kuendesha makao hayo ni kuwa mwezeshaji wa makao ya aina hiyo anapaswa kuwa na uwezo wa kumudu kutoa huduma timilifu bila kutegemea msaada toka Serikalini. Hata hivyo, pale Bajeti ya Serikali inaporuhusu, Wizara yangu imekuwa ikitoa ruzuku kwa vituo vya makao hayo. Aidha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na jamii kuwa

kumpeleka mtoto katika makao iwe ni hatua ya mwisho baada ya jitihada zote za kutoa malezi katika mfumo wa jamii kushindikana.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu ilitoa jumla ya shilingi 25,624,319/= kama ruzuku kwa makao mbali mbali ya watoto yatima na wale waishio katika mazingira hatarishi makao ambayo yako katika Mikoa ya Arusha, Iringa, Mwanza, Kagera, Dodoma, Dar s salaam na Lindi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufahamu kuwa masuala ya yatima na watoto walioko katika mazingira hatarishi ni ya mtambuka, Wizara yangu imekuwa ikifanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Wizara yangu imekuwa ikishirikiana na Wizara hizo katika kuandaa miongozo na mikakati mbali mbali inayolenga kuboresha utoaji wa huduma kwa watoto hao. Vile vile Wizara yangu, pamoja na kuendelea kushirkiana na kutoa miongozo na maelekezo mbali mbali kwa waendesha vituo/makao ya yatima na watoto walio katika mazingira hatarishi, imekuwa pia ikihamasisha Jamii pamoja na wadau mbali mbali kuhusu malezi shirikishi ya watoto hao katika jamii. Hii ni kwa kuzingatia umuhimu wa malezi na matunzo ya watoto katika misingi ya jamii. Aidha, napenda kuwashukuru wadau wote ambao wamekuwa wakisaidia jitihada za Serikali katika kutoa malezi na matunzo kwa watoto hao.

**MHE. JANETH B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri na pia pamoja na kutambua kuwa Wizara ya Afya imekwishatoa dawa katika Kijiji cha Matumaini kilicho katika eneo la Kisasa ambacho kina watoto 150 na kiko chini ya shirika la Katoliki. Watoto hawa ni watoto waathirika na wana darasa la kwanza mpaka la saba la msingi tu. Je, Serikali inaonaje sasa, kuliko kuwa na vituo mbali huko na huko, wakafanya kituo hiki ambacho kiko Dodoma ambapo ni katikati ya Tanzania, wakapanua kijiji hiki kikahudumia watoto wengi zaidi. Sasa hivi wana watoto wa kutosha 150 kutoka Mikoa mbali mbali. Lakini, watoto wengi zaidi, kikawa ndiyo kama kituo mama.

Lakini, swali lingine la pili. Pamoja na kuwa wana huduma ya shule ya msingi, Wizara hizi zote tatu, zinafikiriaje kuanzisha Sekondari ambayo itatoa mafunzo ya mchepuo hasa wanaohitaji watoto hawa na pia kufuatilia misaada inayotoka kama *Action Aid* ambao walikwishatoa misaada kidogo na wakatoa ahadi ambazo hazijakamilika kutolewa na pia Wizara zote hizi zimefuatiliaje na zimekwenda pale mara ngapi kutembelea kituo hiki? Ahsante sana!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuona kwamba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wanatambua kwamba Serikali inafanya jitihada za kusaidia hivi vituo ambavyo vinalea watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Suala la kusema tutengeneze kituo kimoja kwa nchi nzima, mimi nafikiri kwa sasa hivi bado hatujafikia, kwa sababu ukiangalia watoto hao wote ambao tumewataja 1700 na zaidi ni kwamba wanatoka katika maeneo mbali mbali. Ni vizuri tukawa na vituo katika maeneo ambayo yako tofauti na Dodoma ili wale walioko kule waweze kusaidiwa katika maeneo ambayo wako nayo pamoja. Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia kwa sababu wale watoto wengine ambao wanaishi ni yatima wanakuwa wakati mwingine wanapata nafasi ya kwenda kuwasalimia hata wazazi wao, ikiwa ni bibi zao au ndugu zao, wanapewa nafasi ya kwenda kuwasalimu. Kuwaleta katika kituo kimoja, itakuwa ni gharama kubwa sana na pale inapobidi kumpeleka mtoto kwenda kusalimia itakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni kweli kabisa inahitajika kuwepo na Sekondari. Lakini, napenda tu nisema kwanza tuipongeze Serikali kwa sababu imeweza kuwapatia mpaka sasa hivi shule kutoka darasa la kwanza mpaka kufikia darasa la saba. Kama nilivyosema Wizara yangu na Wizara ya Elimu na Maendeleo ya Jamii, tunashirikiana ili kuweza kuona kwamba tunasaidia vituo hivi kwa kadri ya uwezo utakavyokuwa. Tutajitahidi ili kuweza kuona kwamba huduma zile za msingi zinapatikana katika vituo vyote, siyo Kituo cha Kisasa tu, lakini katika maeneo mengine ambako wanatoa huduma hizo ikiwa ni pamoja na kufuatilia misaada na mambo mengine yote ambayo yanahusika, ambayo ni muhimu kwa watoto hawa. *(Makofi)*

Na. 117

**Ushiriki wa Wabunge Katika Mazungumzo ya EPAS ya Makubaliano ya COTONOU**

**MHE. DR. LUCY S. NKYA (K.n.y. MHE. HAMZA A. MWENEGOHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkataba wa *COTONOU* umejengwa juu ya nguzo tatu; na kwa kuwa nguzo mojawapo ni *EPAS:-*

(a) Je, Wabunge wanahusishwa kwa kiasi gani katika mazungumzo ya dhati ya *EPAs* yanayohusisha pande zote mbili za makubaliano ya *COTONOU*?

(b) Je, mazungumzo hayo na matokeo yake yanaweza kuwekwa bayana kwa Wabunge kama siyo kwa wananchi wote?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, makubaliano ya *COTONOU* yanayohusu mahusiano ya kiuchumi *(Economic Partinership Agreements (EPA)* yanaendelea kwa hivi sasa kati ya nchi za *Africa, Carribean* na *Pacific (ACP)* na nchi za Umoja wa Uchumi wa Nchi za Ulaya *(EU).*

Majadiliano ya ubia wa kiuchumi *(Economic Partinership – EPA)* ulianzishwa ukiwa unalenga misingi ya *WTO* ambayo yanataka nchi zipeane unafuu wa kibiashara kwa mtindo wa nipe niukupe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majadiliano haya, Bunge lako tukufu linawakilishwa na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi ambaye ndiye Mwakilishi wa Wabunge katika majadiliano baina ya nchi za *ACP* na *EU*. Hata kwenye majadiliano ya dulu la nne yaliyofanyika Maputo, Msumbiji kati ya tarehe 15 – 19 Oktoba, 2007, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi alihudhuria na kushuhudia mwendendo mzima wa majadiliano hayo.

Aidha, Mheshimiwa Mporogomyi amekuwa akihudhuria vikao mbali mbali vya majadiliao ya *SADC/EPA* na *EU* mjini *Brussels,* Uberigiji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa mnamo mwezi Julai mwaka huu, Wizara yangu iliendesha semina kwa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara wakiwa pmaoja na Wenyeviti wote wa Kamati zote za Kudumu za Bunge. Semina hiyo ililenga kuwaelimisha Waheshimiwa Wabunge juu ya mwenendo wa majadiliano ya kibiashara kati ya kundi la nchi za *SADC* na nchi za Umoja wa Uchumi wa Nchi za Ulaya *(EU).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kushirikisha Bunge lako Tukufu jinsi majadiliano hayo yanavyoendelea ili waweze kujua zaidi na hivyo waweze kufikisha habari za mazungumzo na majadiliano hayo kwa wananchi ambao ndiyo wapiga kura wao na pia kuishauri Serikali ipasavyo.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwenye jibu lake la msingi amesema kwamba Bunge letu Tukufu linawakilishwa na Mheshimiwa Mporogomyi na akaongeza kwamba Wizara yake imeendesha semina kwa ajili ya Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Uwezeshaji na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa naomba kuuliza. Je, anaonaje kwa sababu amekiri kwamba Wabunge ndiyo wanaoweza wakapeleka huu ujumbe kwa wananchi akatengeneza mikakati ya kuhakikisha kwamba kila baada ya vikao vinapofanyika Bunge lako Tukufu linapewa semina ili tuweze kuelewa kwa sababu Wabunge wengi wanashindwa kujibu maswali wanayoulizwa na wananchi wao? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na masoko**,** napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Nkya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika kama ambavyo tumeeleza kwamba tumeshaanza kutoa semina kwa Wabunge wa Kamati mbalimbali na nimekiri hapa kwenye jibu la msingi kwamba tutaendelea kutoa taarifa kadri mkakati utakavyokuwa unaendelea, naafikiana naye kabisa kadri mazungumzo yatakavyokuwa yanaendelea na hasa sasa hivi kwa vile majadiliano haya yanafikia mwisho tutatoa taarifa kwa Wabunge kupitia semina ili waweze kuwafahamisha wananchi kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. WILBROAD P. SLAA**: Mheshimiwa Naibu spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza, kwa kuwa swali la msingi linauliza mazungumzo na matokeo yake kuwekwa wazi kwa Wabunge na kwa kuwa Kamati zilizotajwa siyo Wabunge wote walioko hapa na kwa vile mazungumzo haya mwisho wake ni Desemba mwaka huu na mkataba unaozungumziwa una fedha nyingi na Tanzania tusiposhiriki kikamilifu tunaweza kuzipoteza fedha hizo.

Je, Waziri anaweza kulieleza Bunge hili tumefikia hatua gani katika mazungumzo haya na sisi Tanzania tunazungumza kama *EPA* ipi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa viwanda, biashara na masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Slaa, Mbunge wa Karatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu spika, ushirikishi nilioueleza hapa ni ule wa kujua ni nini kinachoendelea na kama nilivyoahidi hapa nilipokuwa najibu swali la nyongeza ya kwamba hatimaye tutakapokuwa tumefikia mwisho wa majadiliano tutatoa taarifa kwa Wabunge ili waweze kuwafahamisha wananchi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwamba tunajadiliana katika *EPA* ipi na tumefikia wapi, nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa hivi sasa majadiliano hayo yapo katika mazungumzo ya hatua za mwisho. Kwa hivyo pengine si vema kwa sasa hivi tukaanza kujikita kutoa maelezo kwamba tutakuwa katika kundi lipi lakini muda si mrefu Serikali itatoa taarifa.

Na. 118

**Ujenzi wa Soko la Kimataifa la Mbogamboga,**
**Viazi na Matunda Segera**

**MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2005-2010, kwa shabaha ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Serikali imedhamiria kujenga soko la kimataifa la mbogamboga, viazi, matunda na kadhalika. Segera Mkoani Tanga; na kwa kuwa tayari eneo limekwishatengwa na kwamba kitendo cha kujenga soko hilo kimeamsha upya ari ya kuongeza ubora wa mazao mkoani humo:-

(a) Je! Ni eneo la ukubwa gani linahitajika na soko litaanza kujengwa lini?

(b) Je, katika eneo la soko kutakuwa na mpango wa nafasi kuanzisha eneo la kuzalisha bidhaa za kuuza nje ya nchi *(export processing zone (EPZ)?*

(c) Je, wazo la kuwapeleka viongozi na watendaji wachache wa mkoa wa Tanga kuona soko la kimataifa la mbogamboga, matunda, viazi, ndizi na kadhalika katika Jiji la Pretoria jiji dogo la TSHWANE Afrika ya Kusini, litaendelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa soko la Segera ni ekari 100. Mahitaji halisi ya eneo la soko yatabainishwa baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu (*feasibility study*). Wizara imeingia mkataba na taasisi ya utafiti ya Chuo Kikuu cha Sokoine kufanya upembuzi huo ambao umepangwa kukamilika wakati wowote mwezi huu wa Novemba2007. Baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu Wizara itatafuta washirika wa Maendeleo watakaoshirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ili kufanikisha ujenzi wa soko hilo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwezekano wa kuanzisha eneo la kuzalisha bidhaa za kuuza nje ya nchi yaani *Export Processing Zone – EPZ,* katika soko hilo; taarifa ya upembuzi yakinifu itarahisisha pia mapendekezo ambayo yataiwezesha Serikali kuamua kama eneo litakalojengwa soko linafaa kwa kuanzisha eneo la kuzalisha bidhaa za kuuza nje ya nchi au la.

(c) Mheshimiwa Spika, wazo la kuwapeleka baadhi ya viongozi na watendaji wa Mkoa wa Tanga kuona soko la kimataifa lililoko *TSHWANE* katika Jiji la Pretoria huko Afrika ya Kusini halijakamilishwa bado. Kwa hiyo, maandalizi ya mpango wa utekelezaji wa programu ya ujenzi wa soko hilo yatakapokamilika, wazo la kuwapeleka viongozi hao Afrika ya Kusini litazingatiwa ili ujenzi wa soko uende sambamba na mafunzo ya viongozi kwa kutembelea masoko ya mifano kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. ABDALLAH KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa dhana ya ujenzi wa soko hili sasa umechukua kipindi cha takribani miaka minne na Mheshimiwa Waziri anatueleza *feasibility study* imefanyika, hivi tunaweza kupata taarifa ya kuaminika kwamba ujenzi wa soko hili utaanza lini hasa ukizingatia kwamba eneo tumeshalitoa tunachosubiri ni ujenzi wa soko hilo.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** mheshimiwa naibu spika kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdalah Omar Kigoda, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mbunge kwamba wazo la ujenzi wa soko hilo ulianza mapema kidogo mwaka 2003 na kama nilivyoeleza hapa hatua za awali zilizochukuliwa ni kuteua watu wa kutafiti uwezekano wa ujenzi wa soko hilo na hapa nimesema wakati wowote mwezi huu wa Novemba, 2007 upembuzi utakamilika baada ya hapo sasa ndiyo tutaanza kutafuta washirika yaani *development patiners* ambao watashirikiana na viongozi wa Wilaya ya Handeni ili soko hili liweze kuanza kujengwa.

**MHE. SUSAN LYIMO:** Nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa masoko ni sehemu muhimu sana ya kuendesha biashara ndogondogo na hususani ya vyakula, na kwa kuwa serikali bado haijakidhi mahitaji ya kujenga masoko maeneo yote ya nchi. Je, watu binafsi wanaruhusiwa kujenga masoko ili kuweza kukidhi mahitaji hasa sehemu zile ambazo hakuna masoko ?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshiwa Suzan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kabisa kwamba si rahisi kwa serikali kueneza masoko katika nchi yote kwa pamoja na haraka na kama nilivyosema kwamba hata katika maeneo yale tuliyoyainisha kujengwa masoko bado tunatafuta washirika wa maendeleo tuweze kushirikiana nao. Kwa mantiki hiyo kama watakuwepo watu binafsi ambao wana uwezo na nia ya kujenga masoko, wawasiliane na mamlaka zinazohusika na suala hilo linawezekana kabisa.

Na. 119

**Chuo cha Maendeleo ya Jamii**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Chala- Nkasi kiliwahi kuwa na mfadhili siku zilizopita lakini sasa hivi hakina tena mfadhili:

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukitafutia mfadhili mwingine au kumrudisha mfadhili mwingine au kumrudisha mfadhili aliyekuwepo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani ina mpango gani wa kukarabati majengo ya chuo hicho ambayo sasa ni chakavu sana au kujenga mengine mapya?

(c) Kwa kuwa Walimu pia hawatoshi. Je, Serikali ina utaratibu upi wa kuongeza Walimu na vile vile kuongeza majengo?

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Waziri wa nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, zamani alikuwa Maendeleo ya Jamii.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIANI):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa maendeleo ya jamii, jinsia na watoto, naomba nilete salamu zake na kusema kwamba anaendelea vizuri na tuzidi kumwombea dua aweze ku-*recover* vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya jamii, jinsia na watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano D.Nyami, lenye sehemu a, b, na C kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Chala ni moja kati ya Vyuo 58 vya Maendeleo ya Jamii vilivyopo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Tangu kuanzishwa kwa Vyuo hivi kwa Vyuo hivi mwaka 1975 hapa nchini, vilikuwa vikifadhiliwa na Serikali ya Sweden kupitia shirika lake la Misaada la Maendeleo *(SIDA)* hadi mwaka 1966 ambapo Serikali ya Sweden ilisitisha ufadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mfadhili huyo asitishe huduma za kusaidia chuo hicho, Serikali imeendelea na jukumu la kuviendesha vyuo vyote, pamoja na hiki cha Chala kwa kutumia rasilimali zilizopo kwa kushirikisha wananchi na wadau wengine. Aidha uongozi wa Chuo na Bodi unahamasishwa kuwa na ubunifu wa kuweza kuwa na mpango wa kimkakati pamoja na kukaribisha wafadhili wengine.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeanzisha mpango wa kukarabati majengo ya Vyuo kwa awamu. Katika awamu ya kwanza 2001/2002 Chuo Cha Chala kilipatiwa fedha shilingi 3,500,000/- kwa ajili ya ukarabati mdogo. Vilevile katika mwaka 2004/2005 Chuo hicho kilipatiwa jumla ya shilingi 8,000,000/=. Katika mwaka 2006/2007 Wizara yangu ilifanya ukarabati kwa kuzingatia Vyuo ambavyo vilivyokuwa na hali mbaya zaidi ya majengo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Vyuo vingi vya Maendeleo ya Wananchi havina Walimu wa kutosha kikiwemo Chuo Cha Chala. Katika jitihada za kukabiliana na tatizo hili, katika mwaka wa fedha 2004/2005 wizara yangu baada ya kupata kibali cha ajira iliweza kuajiri Walimu kumi (10) wa kupunguza pengo la upumgufu wa Walimu Vyuoni. Walimu hao walipangwa kwenye vyuo vilivyokuwa na upungufu mkubwa zaidi, Chuo cha Chala kinao Walimu wanne (4) wa Wizara na mmoja wa kuazima kutoka Halmashauri ya Wilaya. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara yangu ilipata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na iliajiri Walimu nane wakiwemo mafundi stadi wapya watatu ambao walipelekwa kwenye Vyuo vilivyokuwa na upungufu wa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spka, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Nyami kwa kazi nzuri na kubwa anazoendelea kuzifanya akiwa kama Mbunge na Mjumbe wa bodi ya Chuo, kwa kufuatilia kwa karibu maendeleo ya taasisi hizi na huduma za wananchi wa Jimbo lake hususani Chuo cha Chala.

**MHE. PONSIANO NYAMI**: Nashukuru sana kwa majibu mazuri mno ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili:-

Kwa kuwa ufanisi wa Vyuo hivi, ambapo vijana wengi wanapata ufundi, inategemea sana katikavyuo hivi pawepo na maji na umeme, mahali ambapo Chala hakuna maji kwa maana ya kisima cha kuchimbwa na hata umeme kwa maana ya jenereta iwepo ili kuweza kuleta ufanisi katika shughuli mbalimbali zinazotegemea umeme kwa fani zilizopo pale. Je isingekuwa ni vizuri Serikali ikajitahidi kuwachimbia angalau kisima kimoja tu pamoja na kuwapa jenereta ili vijana waweze kupata fani zinazotakiwa na kuondokana na shidaya maji ambayo hayapo pale.

Pili, kwa vile Chuo hakina gari kutoka pale kijijini Chala kwenda makao makuu ya Wilaya ni kilometa thelathini na mbili na kwenda Sumbawanga ni kilometa sabini (70) mahali ambapo ndipo wanapata mahitaji yote. Je, Serikali isingeweza kuwapatia gari hata moja linaloweza kutumika lakini lina unafuu wa kufanya kazi ili kuwaondolea adha ya kusafiri kwa kudandia malori yanayotokea Mpanda kwenda Sumbawanga na Sumbawanga kwenda Namanyele?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIANI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyami kama ifuatavyo:-

Kuhusu suala la umeme, kama mnavyojua kwamba Wizara hii ina bajeti ndogo lakini imeendelea kuimarisha huduma mbalimbali katika vyuo vyake. Napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuimarisha huduma hizi ikiwa ni pamoja na kuzingatia suala zima la kupatikana kwa maji.

Kuhusu suala la umeme, sasa hivi tuna utaratibu wa kuanzisha umeme wa *solar* katika vyuo vyetu. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba chuo hiki cha Chala mara tu fedha zitakapopatikana, tutakiingiza katika utaratibu huo.

Kuhusu suala la usafiri, tutaendelea kufuatilia ili kuhakikisha kwamba baadhi ya gari ambazo tutaweza kuzipata hata kutokea Wizarani zitakazoweza kurekebishwa tutazipeleka katika vyuo ambavyo vina mahitaji makubwa ya usafiri.

Na. 120

**Kuboresha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**

**MHE. ROSEMARY KIRIGINI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa rais wa awamu ya nne aliahidi kupambana na tatizo la ajira kwa vijana, na tayari kuna matunda yanayoonekana kama mikopo ya kifedha katika taasisi za kijamii, kitaifa na

kimataifa uanzishwaji wa *SACCOS* mbalimbali; na kwa kuwa moja ya vikwazo vya ajira ni vijana kutokuwa na taaluma au ujuzi wowote:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipanua na kuvipatia vitendea kazi vyuo vya maendeleo ya jamii ili viweze kutoa mafunzo bora ya kiufundi kwa vijana wetu?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, napenda kutoa maelekezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wizara yangu inavyo vyuo vine vya Maendeleo ya jamii *(Community DevelopmenTraining Institute (CDTI).* Vyuo hivyo ni Tengeru (Arusha) kinachotoa mafunzo ya Stashahada ya juu katika taaluma ya Maendeleo ya Jamii, chuo cha Rugemba (Iringa) na Buhare (Mara) vinavyotoa mafunzo ya cheti katika taaluma ya Maendeleo ya Jamii na Ufundi Sanifu (ujenzi).

Mheshimiwa Naibu spika, Wizara yangu pia inavyo vyuo 58 vya Maendeleo ya wananchi *(Folk Development Collages (FDC)* Vyuo hivi vilianzishwa mwaka 1975 kwa madhumuni maalumu ya kuwapatia wananchi hususan wa vijijini elimu na stadi mbalimbali za maisha ili kuwawezesha kupambana na mazingira yanayowazunguka katika kuondokana na ujinga, maradhi na umaskini na hatimaye kujiletea maendeleo yao. Baada ya kusema haya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu spika, Serikali kupitia Wizara yangu inayo mipango kadhaa ya kuvipanua na kuvipatia vitendea kazi vijana na wananchi wetu. Mipango hiyo ni kama vile:-

- Kuandaa mitaala mipya ya mafunzo ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya stashahada *(Diploma)* katika vyuo vya Buhare, Misungwi na Rugemba ili viweze kusajili wanafunzi wa ngazi ya Stashahada kuanzia mwaka 2008/2009. Pamoja na kuanza kutoa stashahada ya miaka miwili, vyuo hivi bado vitaendelea kutoa mafunzo ya cheti ya mwaka mmoja.

- Upo mchakato unaoendelea ili itakapofikia mwaka 2008/2009 chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kiweze kutoa mafunzo ya shahada ya kwanza badala ya stashahada ya juu.

- Aidha, Wizara inaandaa utaratibu wa kuvipandisha hadhi baadhi ya vyuo vya Maendeleo ya wananchi vya Monduli (Arusha), Ruaha(Iringa), Mabughai(Tanga), Uyole (Mbeya) na Mlale (Ruvuma) ili viweze kutoa mafunzo ya Stashahada ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii.

- Wizara inaendeelea kuvifanyia ukarabati mkubwa na mdogo vyuo hivi na kuendelea kuvipatia vyombo vya usafiri kama vile magari mawili kwa ajili ya chuo cha Tengeru na Missungwi, ununuzi wa pikipiki, baiskeli, uwekaji wa umeme wa jua na huduma za mawasiliano *(internent)* kwa baadhi ya vyuo.

Na. 121

**Uhaba wa Askari wa Kike Nchini**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:

Kwa kuwa, Ulinzi na Usalama ni haki ya raia wa jinsia zote, na kwa kuwa, idadi ya Askari Wanawake ni ndogo sana katika Vituo vya Polisi Tanzania, hali inayosababisha usumbufu mkubwa pindi yanapotokea matatizo yanayohusu wanawake:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kulipatia ufumbuzi wa haraka tatizo hilo la muda mrefu ili kuwatendea haki Wanawake wa Tanzania?

(b) Je, inakuwaje mtuhumiwa wa kike ashikiliwe kituoni na Askari wa Kiume, jambo linaloweza kusababisha ushawishi wa jinsia?

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omari Juma, Mbunge waViti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa jinsia Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa inaongeza idadi ya Askari wa Kike wanaojiunga na Jeshi kila mwaka. Aidha, Makamanda wa Kike ndani ya Jeshi la Polisi wameanzisha Umoja unaoitwa *Tanzania Police Female Network* kwa madhumuni ya kuwaunganisha wasichana walioko mashuleni kujiunga na Jeshi la Polisi mara wamalizapo masomo yao ya Sekondari kwa lengo la kuongeza idadi ya Askari wa Kike.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu 26 cha Sheria Na. 9 ya mwaka 1985 cha Kanuni za Mashtaka ya Jinai kinaagiza kwamba mtuhumiwa wa kike anatakiwa kupekuliwa na Askari wa Kike. Naomba kunukuu:-

"*Whenever it is necessary to cause a Woman to be searched, the search shall be made by another Woman with strict regard to decency*"

Aidha, *P.G.O.* Na. 357 aya ya 30 inatoa ufafanuzi kwamba pale kunapokuwa hakuna Askari wa Kike basi mtuhumiwa huyo atapekuliwa na mwanamke yeyote. Naomba kunukuu:-

*"Female Prisoners must be searched by a Police Women or Female searcher out of public view and with strict regard to decency."*

Mheshimiwa Spika, makosa ya jinai hutendeka katika mazingira tofauti. Endapo itatokea mwanamke amefanya kosa lolote la jinai hana budi kukamatwa na Askari yeyote kwani haiwezekani mtuhumiwa mwanamke asikamatwe na kufikishwa kituoni kwa vile hakuna Askari wa Kike wa kumkamata kwa wakati huo.

Hata hivyo, mtuhumiwa wa Kike anapokamatwa na Askari wa Jinsia nyingine, Askari huyo anapaswa kuzingatia Sheria za Nchi na utu wa binadamu.

Na. 122

**Kuondoa usumbufu kwa Askari Wastaafu**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa Askari wastaafu wa Zanzibar wanapata usumbufu mkubwa sana kwa kufuatilia fedha zao Dar es Salaam na kwa kuwa Askari hao hulazimika kujigharama kwa muda wa hadi wiki mbili pindi wanapofuatilia fedha zao:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa Askari hao wanapata usumbufu mkubwa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuondoa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kustaafu askari na maafisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania upo kwa mujibu wa sheria. Hatua za kustaafu mwanajeshi huanzia kikosini kwake, miezi sita kabla ya tarehe ya kustaafu. Hatua hizo ni pamoja na kujaza fomu inayoitwa Hati ya Utambulisho. Katika kati ya utambulisho mhusika hujaza sehemu anayopendelea kupokelea pensheni na mafao yake.

Mheshimiwa Spika, taratibu za kustaafu zinapokamilika kikosini, faili la mhusika hutumwa Makao Makuu ya Jeshi ambako hufanyiwa mahesabu ya pensheni na mafao.

Baada ya taratibu na mahesabu kukamilika faili la mstaafu hupelekwa hazina kwa ajili ya kufanyiwa malipo. Hazina huandika hundi na kuipeleka sehemu ambayo mwanajeshi huyo aliandika kwenye hati ya utambulisho kuwa atakuwa anapokelea mafao na pensheni yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya utangulizi, askari au afisa wa Jeshi la Wananchi, kama atafuata ipasavyo taratibu za kustaafu, ni dhahiri kwamba hatapata usumbufu katika kupata mafao na pensheni yake. Wastaafu wa Jeshi la Wananchi wanaufahamu utaratibu ulivyo na ninashauri kuufuata. Suala la kufuatilia mafao Dar es Salaam ni matakwa ya mwanajeshi mwenyewe na halitokani na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu inawajali sana wastaafu na ni wajibu wetu kuona kila mstaafu anapata haki yake kwa wakati na bila bila ya ufumbufu wowote.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bado kuna manung’uniko miongoni mwa askari wastaafu. Je, sababu za msingi za nyaraka kutokamilika ni zipi na nani anayesababisha hilo, mwajiri au mwajiriwa?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba utayarishaji wa mafao na pensheni za wastaafu unategemeana sana ukamilifu wa nyaraka mbalimbali zilizomo katika jalada la mhusika. La msingi hapa ni kwamba kuna makosa huwa yanafanywa na mwajiri na kuna makosa huwa yanafanywa na mwajiriwa.

Kwa upande wetu sisi jeshi, tumeshaona kwamba hali ipo hivyo na hatua tumeanza kuchukua kupitia majalada yote ya wanajeshi miezi 18 kabla ya kustaafu ili makosa hayo yasiweze kuendelea na mafao na pensheni ziweze kupatikana kwa wakati. (*Makofi*)

Na. 123

**Hitaji la Benki ya NMB– Zanzibar**

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa benki ya *NMB* inatoa huduma nzuri zinazopendwa na wananchi wengi nchini na kwa kuwa ni benki pekee ambayo Serikali ina hisa kubwa zaidi ya asilimia 51 na kwa kuwa benki ni taasisi muhimu katika kusaidia kukuza uchumi wa wananchi kwa njia za mikopo na kuweka akiba:-

(a) Je, Serikali inaelewa kuwa benki hiyo haina tawi lake Tanzania Zanzibar?

(b) Je, Serikali inawaahidi nini wananchi wa Tanzania Zanzibar?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa kwa kuwa *BOT* watahamia katika jengo lao jipya hivi karibuni jengo wanalotumia hivi sasa pale Zanzibar litakuwa muafaka kutumiwa na *NMB*?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mbunge wa Tumbatu lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli kwamba *NMB* haina tawi Zanzibar ingawa haina tawi Unguja, pamoja na kuwa ina tawi Pemba. Huduma za kibenki zinahitajika katika maeneo mengi hapa nchini, hivyo *NMB* itafungua matawi katika maeneo yote Tanzania, ikiwemo Unguja, kulingana na vigezo vyote muhimu vinavyotakiwa. *NMB* imenuia kupanua mtandao wake na kufungua matawi sehemu ambazo hazijafikiwa ikiwa ni pamoja na Mji Mkongwe wa Zanzibar.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sera ya utawala bora katika ubinafsishaji na kulingana na mikataba ya mauzo kati ya Serikali na wawekezaji, Serikali itaendelea kuboresha mazingira kwa mabenki kufanya shughuli zao kwa ufanisi pamoja na kuishawishi *NMB* kuipa Unguja kipaumbele katika kuamua maeneo ya kufungua matawi mapya. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuwahamasisha wananchi kuanzisha benki zao katika maeneo yao na hivyo kuwapatia huduma za kibenki kwa gharama nafuu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa *NMB* tayari umepata kibali cha kufungua matawi yake Unguja. Hata hivyo, uamuzi wa kutumia jengo lililokuwa linatumiwa na Benki ya Kuu ya Tanzania, Zanzibar ni wa benki yenyewe kwa kuzingatia vigezo vya kibiashara.

**MHE. MZEE N. ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuna vigezo ambavyo vinahitajika ili waweze kufungua benki *NMB* lakini suala hili tunaliuliza mara nyingi sana ni vigezo gani vinakwamisha mpaka leo havijaweza kuthibitisha wakati ambapo mabenki mengine yote yapo kule Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nimesikia wanakuja.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vinavyohitajika ni kama ifuatavyo: Moja inazingatia uwezo wa kifedha wa wananchi wa eneo husika, kigezo cha pili. Matakwa ya kisheria na taratibu za udhibiti wa mabenki. Tatu jamii husika kuhitaji na kuwa uwezo wa kulipia huduma mbalimbali za kibenki kutokana na shughuli za kiuchumi zilizopo. Nne, kuwepo kwa usalama katika eneo husika, tano, miundombinu kama vile barabara, umeme, viwanja vya ndege, mawasiliano na simu. Vingi katika hivi vipo, kinachofanyika sasa hivi ni kwamba benki zote ikiwemo *NMB* kama kuna mahali panahitaji tawi la benki, wanakwenda kufanya utafiti, wakiridhika kwamba vigezo hivi vyote vimo na benki hiyo itapata faida kwa kufungua tawi pale, wanaweza wakafungua tawi la benki. Lakini kwa Unguja benki nyingine zipo. Kama aina maalum ya huduma ambayo wananchi fulani wanahitaji basi tuelezane ili tuwezeshe kuwashawishi *NMB* kuweza kufungua tawi.

Lakini nilivyosema katika jibu langu la msingi Benki Kuu tayari imeshatoa kibali kwa *NMB* kufungua matawi Zanzibar. Serikali si muafaka kuwachagulia sehemu maalum ya kufungua matawi. *NMB* yenyewe itafanya utafiti na pale watakapoona kwamba inafaa watafungua matawi mapema iwezekanavyo.

Na. 124

**Malipo ya Pensheni kwa Wastaafu**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa malipo ya pensheni yalikuwa na madhumuni ya kuwasaidia wastaafu waendelee kujikimu kimaisha na siyo kwa ajili ya anasa:-

(a) Je, kwa nini viwango vya pensheni kwa wastaafu hao visioanishwe na hali halisi ya maisha yalivyo ili kima cha chini cha mshahara kiwe ndiyo kigezo?

(b) Kwa kuwa fedha hutolewa kwa kipindi cha miezi sita sita. Je, kwa nini muda huo usipunguzwe uwe kati ya miezi miwili au mitatu ili wastaafu wawe na chochote kila wakati?

(c) Kwa kuwa wapo viongozi waliotumikia nchi yao kama vile Wakuu wa Mikoa, Wilaya na hata Wabunge. Je, isingekuwa vizuri mafao ya viongozi hao yakarekebishwa ili yalingane ya hadhi za kazi zao waliotumika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni sera ya Serikali ya Awamu ya Nne kuhakikisha inawajali wananchi wake wote ikiwa ni pamoja na wastaafu. Katika jitihada za kuboresha maisha ya wastaafu, Serikali imekuwa ikitekeleza kwa kuongeza kima cha chini cha pensheni kwa wastaafu wake kila hali ya uchumi inavyozidi kuwa nzuri. Hivyo, Serikali inaangalia uwezekano wa kuipitia sheria ya pensheni ili kuifanyia marekebisho kima cha chini cha pensheni kilingane na kima cha chini cha mshahara. Hata hivyo, mapitio hayo yataenda sambamba na ukuaji wa uchumi ambao ndiyo unaokuwa kigezo kikuu cha kuwezesha malipo hayo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wastaafu wanaolipwa na Wizara yangu hulipwa pensheni zao kila baada ya miezi sita. Kabla ya utaratibu huo wastaafu walikuwa wanalipwa pensheni zao kila mwezi lakini kutokana na malalamiko ya wastaafu wenyewe ya kwamba, kiwango cha pensheni kilikuwa ni kidogo na gharama za kufuatilia kwenye vituo ilikuwa ni kubwa kuliko pensheni yenyewe. Serikali ililazimika kubadilisha utaratibu wa kulipa kila mwezi na kulipa kila baada ya miezi sita. Hali hiyo, ilipelekea pia Serikali kuruhusu kupitisha sheria ya kuwaruhusu wastaafu wanaopenda kulipwa pensheni zao kwa mkupuo, walipwe badala ya kulipwa kila mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu baada ya kupokea malalamiko mengi ya wastaafu na kuona uzito wa suala hilo hatua zinachukuliwa za kuweka utaratibu wa kuwalipa wastaafu kila baada ya miezi mitatu mitatu kama wanavyolipwa wastaafu wa Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (*PSPF*). Aidha, kama nilivyosema wakati najibu swali Na. 91 la Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, katika mkutano huu wa Bunge, Serikali inahamishia huduma ya pensheni katika Mifuko ya Pensheni. Hivyo wastaafu husika watakuwa wanapata pensheni kulingana na taratibu za mifuko hiyo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wapo viongozi walioitumikia nchi yao kama vile Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na hata Wabunge ambao malipo ya kiinua mgongo yanakokotolewa kulingana na hadhi yao yaani kulingana na mshahara aliokuwa nao wakati anastaafu kwa cheo alichokuwa nacho na muda aliofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa wanaolipwa pensheni zao za kila mwezi kulingana na hadhi ya vyeo vyao walivyovitumikia ni wale tu waliotajwa kwenye kwenye ya pensheni namba 2 ya mwaka 1999 kifungu namba 20 (3). Wastaafu wengine wote ikiwa ni pamoja na Wakuu wa Mikoa na Wilaya mafao yao hulipwa kwa mujibu wa Sheria ya Pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, malipo ya pensheni yanalipwa kwa wastaafu wote kwa mujibu wa sheria za pensheni. Ili kuwezesha mabadiliko yoyote kufanyika ni lazima kwanza sheria husika zibadilishwe.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kujibu vizuri swali langu 124. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa suala linalohusu malipo ya wastaafu limekuwa likisuasua kwa kipindi cha zaidi miaka kumi na Waziri, anasema sheria inaandaliwa ili angalau sasa lishughulikiwe. Waziri anaweza kulihakikishia Bunge hili ya kwamba sasa nadhani kabla ya Bajeti ijayo suala hili litakuwa limekamilika ili wazee waendelee kupewa haki yao?

(b) Kwa kuwa katika sheria namba 14 ya mwaka 1981 malipo ya Wabunge katika pensheni yalikuwa ni asilimia 25 ya mshahara wake wa mwisho atakapomaliza vipindi viwili atalipwa pensheni. Lakini sheria hiyo ilikuja kufutwa na misingi iliyotumika kufuta haieleweki. Sasa Waziri atakubaliana nami ya kwamba ni vizuri hiyo ikarudishwa ili Wabunge wanapostaafu wapate pensheni na hali yao iendelee kuwa nzuri kuliko hivi sasa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya kaka yangu Mheshimiwa Paul Kimiti, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu sera Serikali kwa sasa hivi imeandaa sera ya pensheni, inajadiliwa Serikalini na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kimiti kwamba kuna kila dalili kwamba inawezekana sera hiyo ikapitishwa kabla ya kuanza mwaka wa fedha wa 2008/2009.

Kuhusu pensheni inayowahusu Wabunge, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba hii ni sehemu mojawapo ambayo itaangaliwa kama itabidi sheria hiyo, irudishwe Bungeni tutairudisha, lakini tunaichukua.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paul Kimiti, kuongezea majibu mazuri ya Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Wale ambao walikuwepo kwenye Bunge lililopita watakumbuka kwamba suala la pensheni ya Wabunge lilijadiliwa na uamuzi ulikuwa wa Wabunge kwamba tuhame kwenye *pension* twende kwenye *gratuity*. Kama Waheshimiwa Wabunge, wanafikiri ni vizuri kwenda kwenye *pension* badala ya *gratuity* basi tujadili ili sisi Wabunge tuamue ndipo iletwe Serikalini. Lakini uamuzi ni wa Wabunge wenyewe na siyo Serikali kwa niaba ya Wabunge. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa suala hili tunasubiri sheria ya Tume ya Bunge ndiyo itakayojadili maslahi ya Wabunge. (*Makofi*)

Na. 125

**Ujenzi wa Barabara ya Feri Kisarawe II**
**Tundwi Songani**

**MHE. JOHN PAUL LWANJI (K.n.y. MHE. MWINCHOUM A. MSOMI)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya ujenzi wa barabara kutoa Feri Kisarawe II hadi Tundwi Songani?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Barabara ya Kibada (Feri)- Kisarawe II – Tundwi Songani yenye urefu wa kilomita 31.6 iko katika kiwango cha changarawe na udongo. Kwa sasa barabara hii ina wastani wa kupitisha magari 74 kwa siku. Katika mwaka 2006/2007, kiasi cha shilingi 20,000,000 zimetumika kwa ajili ya kuifanyia matengenezo barabara hii. Matengenezo hayo yamehusisha kuchonga kwa greda, kusafisha mirefeji na makalvati, kujenga mifereji pamoja na kuweka kifusi katika sehemu korofi kati ya Kibada na Chekeni Mwasonga.

Aidha, kiasi cha shilingi 70,000 zimetumika kwa ajili ya kufungua barabara kati ya Tundwi Songani na Kimbiji.

Katika mwaka wa fedha 2007/2008 jumla ya shilingi 103,200,000 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya kawaida na sehemu korofi katika barabara hiyo kama ifuatavyo:-

- Sehemu ya Kivukoni hadi Mjimwema shilingi 43,500,000/=.

- Sehemu ya Kisarawe II hadi Tundwi shilingi 59,700,000/= ikijumuisha pia matengenezo ya madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia idadi ndogo ya magari yanayotumia barabara hii, Serikali kwa sasa haitajenga barabara ya Kibada – Kisarawe II – Tundwi Songani, hata hivyo tunapenda tumhakikishie Mheshimiwa kuwa tutaendelea kuifanyia matengenezo ya kawaida pamoja na kuweka changarawe sehemu korofi ili iendelee kupitika wakati wote.

**MHE. JOHN PAUL LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika ujenzi wa hiyo barabara kulikuwepo na ubomoaji wa nyumba pamoja na ukataji wa mimea kama mikorosho pamoja na miembe. Je, Serikali inasemaje kuhusu wale wanaostahili kulipwa fidia zao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ujenzi wa barabara hii ni kweli kwamba kulikuwa na miti kidogo iliyokatwa na kulikuwa na nyumba kadhaa ambazo ziliwekwa X na hayo mazao kung'olewa. Lakini napenda nimwambie Mheshimiwa hakukuwa na fidia kwa sababu watu hawa walijenga katika eneo la barabara *(road reserve).*

Na. 126

**Mawasiliano ya Simu za Mkononi**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wananchi wa Jimbo la Karagwe hususani Kata ya Kituntu, Ugurwa, Kihanga, Ndama, Nyaishozi, Nyakasimbi, Rugu, Ihembe, Myakakika, Kibondo, Nyabiyonza, Kiruruma na Bweranyange hawapati mawasiliano ya simu za mkononi kwa kuwa, mtandao hupatikana sehemu chache hasa zenye miinuko, hali inayosababisha kutembea umbali mrefu hata nyakati za usiku kutafuta mtandao na kwa kuwa, wananchi wengi wa Karagwe wanaishi mabondeni kwa kuwa eneo la Karagwe ni milima:

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuyapatia maeneo yote ya Jimbo hilo mtandao wa simu za mkononi?

(b) Je, mpango huo utakamilika lini?

(c) Je, ni maeneo yapi yatapatiwa mtandao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Serikali imekuwa na inaendelea kuwa makini katika kuhakikisha sera ya mawasiliano nchini ya kufikisha huduma bora kwa wananchi wote na kwa gharama nafuu inatekelezwa kwa ufanisi. Hivyo, inashirikiana na wadau wote yakiwemo makampuni ya simu kuhakikisha utekelezaji wa mikakati na mipango ni wa mafanikio.

Kwa upande wa maeneo yaliyoko katika Jimbo la Karagwe, Kampuni ya *Vodacom* imeanza kufanya utafiti wa kiufundi katika maeneo ya Nyaishozi, Mabira, Nkwenda, Kyerwa, Kaisho, Murongo *border*, Rwambaizi na kadhalika. Ujenzi wa mitambo ya mawasiliano utaanza mara tu mchakato mzima utakapokamilika ila juhudi za ziada zinaendelea kufanyika ili kufanikisha zoezi zima mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Celtel* imekwishakamilisha ujenzi wa mtambo/mnara wa mawasiliano katika Kata ya Nyaishozi ambao utasambaza huduma katika vijiji vya Nyakasimbi, Rugu, Ihembe na Nyakakiuka. vijiji vingine vya Kibondo, Nyabiyonza, Kiruruma na Bweranyange vitapata huduma ujenzi wa mtambo wa mawasiliano wa Kata ya Nyakaga utakapokamilika mwezi Julai, 2008. Kampuni ya *TIGO* imekwishapeleka huduma katika Wilaya ya Karagwe, katika maeneo mbalimbali ikiwemo Kananga, Kishao, Nkuenda, Kaisho/Isingilo. *TIGO* pia inao mpango wa kupeleka huduma katika maeneo ya Kyabitembe. Makampuni ya *Zantel* na *TTCL* nayo yanaendelea na kupanga mipango na mikakati pamoja na kufanya tafiti kwa lengo la kusambaza huduma katika maeneo yote ya Jimbo la Karagwe na kwingine kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila shaka Mheshimiwa Blandes, atakubaliana nami kwamba juhudi za kusambaza huduma katika Jimbo lake za mawasiliano ya simu na kwingineko zinaonekana wazi na hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine kuwa wavumilivu na kutoa muda kwa Serikali na washirika wake katika sekta hii ili watekeleze mipango ya maendeleo ya sekta nchini kote. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hali ya mawasiliano ya simu za mkononi katika Jimbo la Karagwe haitofautiani sana na hali ilivyo katika jimbo langu la Chambani na kwa kuwa Naibu Waziri anaelewa kwamba katika ukanda wa Mashariki wa Jimbo langu vikiwemo vijiji vya Mapape, Matele, Mambani, Chwale, Kekewani, Tumbani havina mawasiliano ya simu au yapo kwa tabu sana. Je, Serikali ina mpango gani na wa haraka wa kuyapatia maeneo yote hayo mtandao wa simu za mkononi?

**NAIBU SPIKA:** Unajua wewe Salim mimi nakuheshimu sana, hivi vijiji anavyo Waziri kweli? Lakini kwa sababu anaweza kuwa anafikia huko basi Mheshimiwa Waziri hebu jibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba mawasiliano ya simu Chambani bado hayajawa mazuri sana na sehemu nyingine. Lakini sehemu kubwa ya mawasiliano ya simu kwa kupitia kampuni ya *Zantel* kwa Mikoa miwili ya Pemba yanaendelea vizuri. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba huduma za mawasiliano za *Celtel* zitafika Chambani na tunategemea mwezi huu kwanza wanafungua mtambo wao kule Micheweni na baadaye huduma hizo zitasambazwa Mkoa wa Kusini.

**NAIBU SPIKA:** Tunashukuru Naibu Waziri ni makini sana katika mambo haya anaweza kujibu popote pale. (*Makofi*)

Na. 127

**Kupeleka Umeme Vijijini**

**MHE. WILSON M. MASILINGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mipango mizuri ya kupeleka umeme vijijini na imeweza kufikisha umeme huo katika Wilaya ya Muleba ukitokea nchini Uganda:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi wa kuwafikishia umeme wananchi wengi zaidi katika vijiji vyote vya Tarafa za Muleba, Kimwani, Nshamba na katika sekondari zote?

(b) Je, Serikali iko tayari kuviweka vijiji vya Tarafa za Muleba, Kimwani na Nshamba katika mpango maalum wa kupata fedha kutoka kwa wafadhili ili vipatiwe umeme haraka zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo Sida imeonyesha nia ya kufadhili utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme katika vijiji vya Mkoa wa Kagera. Upembuzi yakinifu ulishafanyika na *Project document* kwa ajili ya kuombea fedha kwa wafadhili imeishatayarishwa. Gharama za mradi huu ni dola za Kimarekani 10.4 milioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukubwa wa mradi wa kusambaza umeme katika vijiji vya Mkoa wa Kagera, Mshauri (*Consultant*) amelazimika kuugawa mradi huu katika awamu tatu za utekelezaji kama ifuatavyo:-

(1) Awamu ya kwanza, itahusisha maeneo ya vijiji vya Wilaya ya Bukoba Vijijini na itagharimu kiasi cha dola za Kimarekani 4.1 milini;

(2) Awamu ya pili, itahusisha maeneo ya vijiji vya Wilaya ya Karagwe na itagharimu kiasi cha dola za Kimarekani 4.9 milioni; na

(3) Awamu ya tatu, itahusisha maeneo ya vijiji vya Wilaya ya Muleba na itagharimu kiasi cha dola za Kimarekani 1.3 milioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu utatekelezwa kwa awamu kama ilivyoainishwa hapo juu kulingana na mapendekezo ya mshauri pindi fedha za utekelezaji zitakapopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za kupeleka umeme katika maeneo ya vijiji vya Tarafa za Muleba, Kimwani na Nshamba, zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 800. Gharama hizo ni kubwa, na kwa kuwa uwezo wa Serikali kugharamia mradi huu ni mdogo, utekelezaji wa mradi huu utategemea upatikanaji wa fedha kutoka kwa wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imeviombea fedha kutoka kwa wafadhili vijiji vya Wilaya ya Muleba vya Kagoma, Ilemera, Kashaluga, Lunazi, Nkomero, Karambi, Ihangiro, Itongo na Rwanda. Aidha, inaendelea kutafuta fedha kutoka katika vyanzo vingine vya ndani na nje ya nchi ili kupeleka umeme katika vijiji vingine vya Tarafa za Muleba, Kimwani na Nshamba.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa juhudi ambazo inazifanya kutuletea umeme. Nina swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa katika swali langu la msingi nilitaka kujua mipango ya Serikali katika kupeleka umeme katika vijiji vya Jimbo langu la Muleba Kusini. Katika jibu la Serikali la swali hili wametueleza mpango

mkubwa wa Mkoa wa Kagera ambao umetuonyesha huyu mshauri *consultant* hatutakii mema Muleba kwamba amelazimika kugawa mradi huo katika awamu tatu, Muleba akatuweka mwisho halafu katika mgao wa mabilioni akatupatia dola milioni 1.3 Wilaya ya Karagwe 4.9, Bukoba Vijijini dola milioni 4.1 kwamba amelazimika sisi kutupa dola milioni 1.3.

Napenda anieleze Mheshimiwa Waziri huyu mshauri anayelazimika kutuumiza na kutuletea majibu ya kutusononesha kwamba sisi tunauliza mnatuletea Maendeleo lini mnatueleza mtakapopeleka kwingine, ni nani na nani amemteua kushughulikia haya mambo? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masilingi kama ifuatavyo: Nampongeza Mheshimiwa Masilingi kwa kuendelea kuwatetea wananchi wa Muleba Kusini kupata nishati ambayo ni ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mshauri aliyefanyakazi hii aliangalia mgawanyo wa umeme katika Mkoa wa Kagera. Kwa sasa hivi Wilaya ya Muleba, kama Muleba imeweza kusambaziwa umeme kwa maeneo mengi vijijini ikiwemo maeneo ya Nshamba, Kamachumu na maeneo mbalimbali. Lakini utakuta Karagwe na Bukoba Vijijini, umeme haujaingia vijijini hiyo ndiyo sababu unaweza kuona kwamba uwiano wa fedha ulivyowekwa umezingatia hilo.

Lakini hata tunaelewa maeneo ambao ameyazungumza Mheshimiwa Mbunge hayajapatiwa umeme na wakati tuna mpango ule unaouzungumzia wa umeme vijijini, haya maeneo aliyoyazungumzia yatawekewa vile vile kipaumbele.

Pia amezungumza kwamba huyo mshauri aliyemteua ni nani? Hii miradi ambayo tunaipata ya misaada na tunafuata utaratibu wa kisheria wa *procurement*. Kwa hiyo, panapokuwepo mradi zinatangazwa hizi *tender* na wanaomba watu wengi wenye ujuzi kama huo.

Kwa hiyo, anayeshinda kufuatana na matakwa ya Kiserikali ndiyo anapata kazi hiyo. Tunajua kwamba haya yalikuwa ni matakwa ya Kiserikali siyo mshauri mwenyewe amejiamulia haya mambo alielekezwa maeneo gani na ayatafutie utafiti ndiyo aliyekuja na utafiti kama huo.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Mimi napenda kuipongeza Serikali kwa niaba ya wananchi wa Tarime kwa kuridhia kukubali kwamba umeme wa *grid* ambao unagharimiwa na kampuni ya Barrick uletwe Tarime utakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi wa Tarime na kampuni yenyewe inayochimba madini pale.

Swali langu mimi nilikuwa naomba kwamba Serikali itatuhakikishaaje kwa sababu umeme utapita katika vijiji kama 11 ambavyo ni Ikomasya, Sulubu, Bisawi, Borongo, Kembe, Ikelege, Wegita, Nyarwana, Nyakungulu, Matongo na Kiwanja na utachukua maeneo makubwa sana ya ardhi na wananchi wamenituma niiombe Serikali kwamba itahakikishaje ya kwamba wanalipwa fidia ya maeneo hayo ya ardhi yatakayochukuliwa kwa ajili ya mradi huo, kwa mujibu wa sheria hasa sheria ya vijiji ya mwaka 99 namba 4 na namba 5? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri unaweza kujibu hilo swali. Kila siku Mheshimiwa Chacha Wangwe ametoka nje ya swali la msingi. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru kwa kuishukuru Serikali kwa juhudi ambazo inafanya. Lakini pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwa ujumla wa Wilaya ya Tarime kwamba kabla miundombinu ya umeme haijapitishwa lazima taratibu za fidia kwa mujibu wa sheria zitakuwa zimefanyika na ndiyo utaratibu wa kawaida kwa hivi tunawaondolewa wasi wasi wananchi fidia zao zitalipwa kwa mujibu wa sheria zetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea muda haupo. Tunaye Mheshimiwa Peter Serukamba.

Na. 128

**Mradi wa Kupeleka Umeme wa *Grid* – Kigoma**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka 2006/2007, Serikali ilipitisha shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kupeleka umeme wa *Grid* ya Taifa Mkoa wa Kigoma:-

(a) Je, utekelezaji wa mpango huo umefikia hatua gani. Je, Serikali inaweza kunipa ratiba ya utekelezaji wa mradi huo kati ya sasa hadi mwaka 2010?

(b) Je, Serikali inafanya mpango gani wa dharura wa kuupatia Mkoa huo umeme wakati tukisubiri utekelezaji wa mradi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mpango wa kupeleka umeme wa gridi ya Taifa Mkoani Kigoma kama ilivyopangwa katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 kwa Serikali kupitisha shilingi bilioni 10, haukuweza kuendelea baada ya matokeo ya upembuzi yakinifu ya kupeleka umeme Kigoma kutoka Tabora kubainisha kuwa kiufundi na kiuchumi njia hiyo haikuwa muafaka. Aidha, hali mbaya ya ukame iliyolikumba Taifa letu mwaka 2005/2006 ilisababisha kutumiwa kwa kiasi hicho cha fedha kwa ununuzi wa mitambo ya dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, uunganishaji wa mji wa Kigoma katika gridi ya Taifa utafanyika chini ya mradi wa *North West Grid Extension*. Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Kahama – Geita – Nyakanazi – Kibondo – Kasulu hadi Kigoma. Kwa sasa *Project Document* ya mradi huu imepelekwa *SIDA* kwa ajili ya mapitio na kuombewa fedha kwa ajili ya utekelezaji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* wameishaagiza vipuri vya kufanyia ukarabati mkubwa mitambo minne iliyopo Kigoma. Ukarabati wa mitambo mitatu ulianza tarehe 25 Oktoba mwaka huu na unategemewa kukamilika mwishoni mwa mwezi Novemba kwa maana mwezi huu. Matengenezo ya mtambo wa nne yanategemewa kukamilika Januari 2008. Ukamilishaji wa mitambo hii utaongeza uzalishaji wa umeme kufikia kilowati 3,500 na hivyo kuwepo upungufu wa kilowati 1,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa upungufu wa umeme Kigoma, Serikali ina mpango wa kununua mtambo mpya wenye uwezo wa kuzalisha kiasi cha kilowati 2,000 ifikapo Desemba 2009. Makubaliano kati ya Shirika la *TANESCO* na Kampuni ya *Anglo Belgium Corporation* yameishakamilika na sasa kinachosubiriwa ni kuwekwa mkataba saini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008 hadi 2012 Serikali ina mpango wa kujenga kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu ya maji kwenye mto Malagarasi. Kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha. kilowati 8,000 ama *(MW 8)*. Mradi huu utafadhiliwa na *Millenium Challenge Corporation (MCC)* ya Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa miradi hii kutaleta nafuu kubwa sana kwa wananchi wa Kigoma na Wilaya zake kuhusu huduma ya umeme. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majawabu ya Naibu Waziri nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Tatizo la umeme Kigoma halionekani kuwa dharura

ukiangalia majibu aliyotoa Naibu Waziri hapa. majibu yote ni ya mpango wa muda mrefu na Kigoma sasa tuko kwenye giza.

Swali la kwanza. Nakumbuka Mheshimiwa Rais alipokuja Kigoma, Naibu Waziri huyu huyu alisema wako kwenye mchakato wa kuleta mashine mpya na mashine hizo zingekuwa zimefungwa kufikia 2008 mwanzoni. Lakini sasa imehamia Desemba 2009, napata shaka inawezekana suala la umeme Kigoma siyo *priority.* Nataka sasa Naibu Waziri aniambie kama wanafunga mtambo 2009 ambao utatupa megawati 2 na Kigoma tunahitaji zisizopungua megawati 7. Hizo megawati zinazopungua tutazipata lini?

Lakini la pili, tumeona wenzetu sasa wanaongea umeme vijijini, sisi leo tunaongelea umeme kwenye Makao Makuu ya Mkoa. Mnataka kuniambia huu mpango wa muda mrefu ambao amesema wa gridi wa *SIDA* anadhani utakuwa umetekelezwa lini?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua matatizo ambayo yako Kigoma kutokana na umeme na hata Mheshimiwa Rais amekwishaizungumzia mara nyingi hata kwenye Mkutano wake Mkuu tulioufanya wa CCM alilizungumzia hili suala la matatizo ya Kigoma na Serikali siyo kwamba imekaa kimya. Amezungumzia haya mambo ya muda mrefu kwa sababu pale Kigoma tunajua kwamba kuna mashine 9, mashine 2 hazifanyi kazi kabisa. Mashine 3 sasa hivi zinafanya kazi zinatoa megawati 1.5 tunajua haitoshelezi.

Lakini vipuri vya kutengeneza mashine tatu nyingine zimekwishawasili, mafundi wamekwishakwenda Kigoma kutengeneza hizo mashine, lakini wakishazitengeneza hizo mashine zitafikisha uzalishaji umeme Kigoma kufikisha megawati 3.5. Tunajua mahitaji ya Kigoma kwa sasa hivi ni megawati 5 patakuwepo upungufu, ndiyo sababu Naibu Waziri amezungumzia hizo mashine ambayo inaagizwa ya megawati 2 itafikisha hizo mpaka megawati 6 unazozizungumza patakuwepo na ziada ya megawati ya kilowati 500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anaweza kuona kwamba hakuna uharaka tunaposema kwamba mashine itakuwa tayari mwaka 2009 kwa sababu hizi mashine haziko madukani kwamba unakwenda kuiondoa pale. Ni kwamba unapoweka mkataba saini ndipo wanaanza kuitengeneza. Kwa hiyo, kipindi hiki ambacho anazungumzia kwamba tutaweka saini wataanza kuitengeneza itasafirishwa itakuja hapa itawekwa tuna uhakika mwaka 2009 ndiyo itaanza kufanya kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yameisha na muda wa Maswali umekwisha. Naomba niwatambulishe wageni tulio nao hapa. Kwanza kabisa tunao wanafunzi kutoka Shule ya *Bihawana Junior Seminary* na walimu wao, hebu m-*raise up.* Simameni, wanafunzi hao wa Bihawana. Karibuni sana. Mjifunze mambo, jinsi Wabunge wanavyofanya kazi zao. Ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu nina mgeni wa Mheshimiwa Wasira, Waziri wa Kilimo na Chakula anaitwa Mheshimiwa Siri Makanaki, yeye ni Katibu wa Vijana wa CCM Bunda, yuko wapi? Asimame, naona ametoka. Yupo? Hebu simama Bwana, karibu sana. *(Makofi)*

Halafu tuna mgeni, sasa ni mgeni wa Mheshimiwa Shah, anaitwa Ndugu Haruna Mbeyu, yeye anaishi London na ndiye Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Matawi yote yaliyoko UK ya CCM. Sasa yuko wapi, aha, karibu sana Ndugu Haruna Mbeyu. Kwa hiyo, kule London kuna matawi ya CCM, sasa matawi yote Mwenyekiti wake huyu, amekuja kuwasiliana na Makao Makuu baada ya uchaguzi. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, ni mtu muhimu sana yeye. Sasa Ndugu zangu shughuli za kazi, kama nilivyotanza mwanzo pengine Wenyeviti wengi walikuwa hawapo. Wenyeviti wa Kamati ya Kudumu ambao pia ni Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, mnakutana sasa hivi kule kwenye Chumba cha mikutano ya Spika kuna kikao cha dharura Wenyeviti wote. Kwa hiyo, mtakuta kwamba matangazo yenu mengi hapa mnasema saa 5 mtakuwa kwenye kikao, kwa hiyo mtajua namna ya kubadilisha.

Matangazo mengine ni kwamba Mheshimiwa Shellukindo sasa anaomba Kamati Ndogo ya Uwekezaji na Biashara kuwa leo hii wakutane saa 5 baada ya kipindi cha maswali. Nafikiri niko sahihi. Kuna Kamati Ndogo nadhani wanaifahamu wao.

Halafu Mheshimiwa Mwenyekiti, Dr. Abdallah Kigoda, Kamati ya Fedha na Uchumi anaomba Wajumbe wake wakutane leo tarehe 9 saa 7 nadhani. Saa 5 nasikia Naibu wake atahudhuria, katika chumba namba 219. Hii Kamati Ndogo ya Shellukindo ni chumba namba 219 zinagongana. Wata-*sought out* wenyewe kule.

Halafu tuna Mheshimiwa William Kusila, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge la Ulinzi na Usalama, anawatangazia Wajumbe wake kwamba wakutane saa 7 mchana katika chumba 428. Saa 7 mchana.

Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, anawatangazia Wajumbe wake leo saa 7 wakutane katika chumba 231. Hawa saa 7 Kamati ya Hesabu za Serikali.

Halafu Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, anawatangazia Wajumbe wake kwamba wakutane saa 7 katika chumba 227 saa 7 katika chumba 227.

Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Katibu wa Wabunge Wanawake wa CCM anawatangazia Wajumbe wote wanawake wa CCM kuwa leo wakutane mara baada ya kuahirisha kikao cha Bunge, hapana cha saa 7 kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa.

Ndugu Mmbaga kwa niaba ya Katibu wa Bunge, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa Jumapili tarehe 11 kutakuwa na semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote.

Semina hiyo ambayo inalenga kuelezea nafasi ya utamaduni katika maendeleo itaanza saa 3 asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa na imeandaliwa na Mfuko wa Utamaduni Tanzania. Kawaida Mikutano Jumapili inaanza saa 5. Ni saa 5. Naomba hiyo izingatiwe siyo saa tatu, ni saa tano.

Ndugu Mmbaga kwa niaba ya Katibu wa Bunge anawatangazia pia anasema niwatangazie Waheshimiwa Wabunge waliopata mwaliko wa Saringo, mimi sikifahamu hiki, kwamba mjadala utafanyika leo tarehe 9 saa 7 mchana katika Ukumbi Na. 428 ghorofa ya nne, jengo la Utawala. Kwa Saringo mnakijua nyie mlioalikwa. Mimi sikifahamu. *(Kicheko)*

Halafu Mheshimiwa Juma Killimbah, Katibu wa *Amani Forum*, yeye anawatangazia Wajumbe wote wa *Executive Committee* wa *Amani Forum, Tanzania Chapter* na wale wa *Regional* wakutane baada ya kuahirisha mkutano huu wa Bunge kwenye chumba cha Pius Msekwa kuna kikao kifupi. Halafu kuna Mheshimiwa Zainab Vulu, yeye ni Katibu wa Mikoa inayolima korosho, anaomba Wajumbe wote wakutane, nadhani kwenye ukumbi nje ya hapa baada ya kipindi hiki cha maswali, kuna ukumbi mmoja hapa karibu nafikiri ndiyo huko.

Halafu Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib yeye ni Katibu Msaidizi wa Wabunge wa CCM anatoa tu taarifa kwamba Jumatatu kutakuwa na kikao cha Chama cha Wana CCM, tutatangaza vizuri siku ya Jumatatu.

Baada ya kusema hivyo, Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema Kamati ya Uongozi itakutana sasa hivi katika Chumba cha Spika. Kwa hiyo, tunaendelea na shughuli za leo. Katibu!

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa Mwaka 2006**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipata nafasi ili niweze kusoma taarifa ya kazi ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa msimu huo wa mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi ya kukushukuru ili niweze kutoa Taarifa ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 88(11), ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2004, ninaomba sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea kuwasilisha taarifa hiyo, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa niaba yangu mimi mwenyewe binafsi lakini na wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa kumalizika vizuri kwa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi ambao ulimpa Mwenyekiti wa Chama hicho Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kura za heshima za kuonyesha ni namna gani alivyo mahiri katika kuiongoza nchi yetu na chama kwa ujumla. *(Makofi)*

Lakini Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi mwenyewe binafsi ninaomba niwashukuru sana wanachama wote wa Chama cha Mapinduzi Mkoani Ruvuma kwa kunichagua kwa kura za kishindo kuwa Mjumbe wa *NEC* wa Halmashauri Kuu ya Taifa kupitia Mkoa huo wa Ruvuma.*(Makofi)*

Lakini nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, nampongeza sana pia Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Bara na wa Visiwani kwa kupata kura nyingi na Wajumbe wote waliochaguliwa katika Mkutano huo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awape nguvu ya kukisimamia na kukiendesha chama chetu kwa taratibu tulizojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kabla sijaendelea ninaomba kwa masikitiko makubwa kwa niaba pia wananchi wa jimbo langu lakini kwa niaba ya Kamati nitoe rambirambi kwa kifo cha Marehemu Salome Mbatia, Mbunge aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto kilichotokea tarehe 24.10/2007. Kifo cha Salome Mbatia kimepokelewa kwa masikitiko makubwa sana kwetu sisi wote. Aidha, napenda kutoa salaam za rambirambi kutokana na kifo cha aliyekuwa Mjumbe wa Kamati hii Mheshimiwa Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, kilichotokea tarehe 26 Juni, 2007.

Kifo cha Mheshimiwa Marehemu Amina kimeacha pengo kubwa sana kwenye Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii. Hata hivyo tunamshukuru Mungu kwa muda aliotupa kufanya kazi na Marehemu wote wawili walitoa mchango wa kutosha na wametumika ipasavyo na wametuachia mambo mengi sana ambayo tulikuwa tunajifunza kutoka kwao. *(Makofi)*

Kama binadamu tulikuwa bado tunawapenda sana hawa ndugu wawili ambao tulifanya nao kazi kwenye Kamati yetu lakini kukaa nao sisi hapa duniani Mungu aliona anawapenda zaidi na ameamua kuwachukua hatuwezi kupingana na Mwenyezi Mungu na zaidi ya kuwaombea wenzetu walale salama mahali pema huko peponi. Na Mwenyezi Mungu awapokee kwa heshima ya utukufu wake.

Mheshimiwa Spika, aidha Kamati inawapa pole pia Wabunge wote na wananchi wote wa Tanzania waliopata majanga mbalimbali katika kipindi hicho Mwenyezi Mungu awape nguvu ya faraja ya kuvumilia yote machungu waliyoyapata na *inshallah* Mwenyezi Mungu atawaondolea hayo kwa wakati unaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwapongeza pia wananchi wa Jimbo la Tunduru kwa sababu taarifa hii inaposomwa ilikuwa pia ni kipindi ambacho ndugu yetu Mtutura alikuwa amepata heshima ya kuchaguliwa kuwa Mbunge wa kuliongoza Jimbo la Tunduru baada ya kifo cha aliyekuwa Waziri wa Nchi, Marehemu Juma Jamaldini Akukweti. Tunampongeza sana Mheshimiwa Mtutura na tunamtakia kazi njema za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati yangu kabla sijaendelea kutoa taarifa hii kwanza naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ambao wameainishwa katika Kanuni namba 102 Toleo la Kwanza ya Kanuni za Bunge la 2004. Wajumbe hao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hiyo ina Wajumbe kama walivyoorodheshwa katika nafasi hii. Mjumbe wa kwanza ni mimi mwenyewe Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, ambaye ni Mwenyekiti ninayeongoza Kamati hiyo, lakini nikisaidiwa kabisa kwa karibu na Mheshimiwa Haroub S. Masoud, Makamu Mwenyekiti wangu. Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Fatuma O. Ally, Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mheshimiwa Zuleikha Y. Haji, Mheshimiwa Issa K. Issa, Mheshimiwa Mgeni J. Kadika, Mheshimiwa Salim A. Khalfan, Mheshimiwa Kapt. John D. Komba, Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, na Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mjumbe.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mheshimiwa Mwinchumu A.. Msomi, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Mohamed A. Said, Mheshimiwa Bujiku P. Sakia, Mheshimiwa Elietta N. Switi, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Haroon A. Suleiman, na Mheshimiwa Florence E. Kyendesya. Aidha tunampongeza sana Mheshimiwa Florence Kyendesya kwa kuteuliwa kuingia katika Bunge letu na kujumuishwa ndani ya Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii ni kama yalivyoainishwa kwenye Kanuni za Bunge Kanuni ya 102 (2) na yanasomeka kama ifuatavyo:-

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Wizara ya Habari, Michezo na Utamaduni.

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo chanzo chake ni Wizara hizo husika.

(iii) Kushughulikia Taarifa za kila mwaka za utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hizo.

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) cha Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizofanywa na Kamati kwa mwaka 2006 zimeainishwa katika mafungu mbalimbali. Lakini ya kwanza ni:-

(i) Ni mikutano.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuanza kazi zake Kamati ilifanya mikutano mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mikutano ya awali ilikuwa ni baina ya Kamati na Wizara zinazohusika katika Kamati yetu na mikutano hiyo ilikuwa ina lengo hasa la kutambua Sera na Mipango mbalimbali inayoshughulikiwa na Wizara husika.

(iii) Aidha, Kamati ilifanya mikutano ya kupitia mapendekezo ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007. Maoni ya Kamati kuhusu mapendekezo hayo yaliwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu wakati wa Mkutano wa Nne wa Bunge hili.

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilifanya mikutano miwili maalum ya pamoja iliyojumuisha Kamati ya Miundombinu na Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii na Mawaziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Mawaziri pia wa Miundombinu ili kufahamu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2005 kuhusu ujenzi wa daraja la Kigamboni. Pamoja na vikao hivyo vyote bado ufumbuzi wa lini daraja la Kigamboni litaanza kujengwa haujfahamika. Wizara husika

zimeashachukua hatua mbalimbali za kiutendaji hata hivyo mwelekeo wa ujenzi wa daraja hilo bado haujachukuwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilipitia hesabu zilizokaguliwa za mashirika na Wizara husika. Hesabu za Shirika la *NSSF*. Kamati ilipitia Hesabu zilizokaguliwa za Shirika la *NSSF* za mwaka 2004/2005 na kulingana na viwango vya wakaguzi waliokagua hesabu za Shirika hilo, shirika lilipata Hati Safi ya Ukaguzi. Pamoja na Hati Safi ya Ukaguzi Kamati bado Kamati iligundua Mambo kadhaa kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na wadaiwa sugu ambao hawajalipa michango yao na wengine madeni ya mikopo mbalimbali, lakini Kamati inalipongeza Shirika kwa kuchukuwa hatua za kisheria kuhusiana na tatizo hilo.

(ii) Kamati ilipokea tatizo la wakopaji kuchelewesha hati maalumu za dhamana kutoka kwa msajili *(Registrar)* wa Serikali na hivyo kufanya wakopaji wa Shirika kupata matatizo wakati wa kushughulikia hatua mbalimbali za mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashirika mengine yanayofanyakazi katika Wizara za kisekta ndani ya Kamati yetu kwa sababu mbalimbali kwa muda huo ambao Kamati ilikuwa inafanya kazi yake hawakuweza kuwasilisha mahesabu yao katika kipindi hicho cha mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilifanya ziara za kukagua miradi na shughuli mbalimbali za kuleta maendeleo katika jamii ya Watanzania. Kamati ilipokea taarifa na kufanya ziara ya kukagua miradi kama ifuatavyo:-

(i) Eneo la ujenzi wa daraja la Kigamboni. Kamati ilitembelea eneo la mradi wa ujenzi wa daraja la Kigamboni. Mradi huu ambao ni muhimu sana sana lakini bado haujaanza kutekelezwa ingawa uko katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilitembelea mradi wa nyumba za kuishi za bei nafuu eneo la Kinyerezi huko Tabata uliojengwa na Shirika la *NSSF*. Kamati iliridhishwa sana na miradi hiyo ambayo imesaidia wananchi wengi ingawa bado kuna matatizo ya miundombinu katika maeneo hayo. Mfano, bado Serikali za Mitaa hazijasogeza huduma za masoko, barabara na kadhalika katika baadhi ya maeneo ya mradi huu.

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mwingine uliotembelewa na Kamati ni mradi wa *hostel* za wanafunzi Mabibo na mradi huo pia umejengwa na Shirika la *NSSF*. Mradi huu unatia moyo na umekuwa mradi muhimu sana kwa wanafunzi wetu wa Chuo Kikuu.. Majengo ni mazuri na yanavutia. Pamoja na mradi huo kukamilika Kamati iligundua kuwa mradi huo pia unakabiliwa na tatizo la miundombinu kwa mfano maji na tatizo la usafi kwa namna moja au nyingine na kadhalika.

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mwingine uliotembelewa na Kamati ulikuwa ni Mradi wa *Mafuta House* ambao pia umejengwa na Shirika hilo hilo la *NSSF*. Kamati ilipongeza taarifa ya uwekezaji katika mradi huo muhimu na juhudi zilizofanywa za kuhakikisha kuwa jengo hilo la *Mafuta House* linakamilika. Aidha, Kamati inalipongeza Shirika la *NSSF* kwa kukamilisha ujenzi wa mradi huo wa *Mafuta House.*

(v) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilitembelea Ofisi za Wakala wa Afya na Usalama mahali pa kazi *(OSHA)* na Shirika la Tija la Taifa *(NIP).* Kamati ilitembelea Ofisi ya Wakala wa Afya na Usalama mahali pa kazi na Ofisi ya Shirika la Tija la Taifa na kujionea utendaji wao na maoni ya Kamati nitayasoma katika karatasi zinazofuata huko mbele.

(vi) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitembelea pia Baraza la Michezo la Taifa BMT na kukagua. Aidha, Kamati ilifanyakazi ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa uwanja wa Michezo wa Taifa.

(vii) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilitembelea kituo cha kulelea watoto yatima cha Msimbazi na Vikundi vingine.

Kamati ilitembelea kituo hicho cha watoto yatima cha Msimbazi na vikundi vingine kama vile kikundi cha *Crew Tanzania*, kikundi cha *Waridi Women Group*, kikundi cha *Muungano Women Group*, kikundi cha *Together Women's Group*, na kutembelea kikundi cha *African Women in Mining Network* ambavyo vyote viko Dar es Salaam.

(viii) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata pia nafasi ya kutembelea Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na Chuo cha Sanaa, Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitembelea Ofisi hizo na kujionea utendaji wa kazi wa Ofisi hizo zilizotajwa hapo juu.

(ix) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilitembelea baadhi ya vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Chuo cha Kibaha Pwani na Misungwi na kuangalia ni jinsi gani shughuli zinavyoendeshwa katika vyuo hivyo vya Maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kutembelea vikundi na miradi mbalimbali ya maendeleo mambo yaliyojitokeza ni pamoja na haya yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iligundua kwamba kuhusu miradi ya jamii, kuna matatizo katika upatikanaji wa masoko ya kuuzia bidhaa zao zinazozalishwa, na hasa miradi inayoendeshwa na akina mama katika vikundi vya maendeleo ambavyo tulivipitia.

Kumekuwa na riba kubwa ya mikopo inayotolewa na hakuna mafundisho ya kutosha kuhusu mikopo na mabadiliko ya soko/biashara ndani na nje ya nchi, biashara na uhaba wa mitaji wa kuendesha biashara hizo ndogo ndogo na kubwa kwa vikundi hivyo vyote vya jasiriamali wanawake na vijana kwa ujumla.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, pia kumeonekana kwamba bado kuna ugumu wa kupata mikopo katika vikundi kutokana na masharti yanayotolewa kuwa magumu.

(c) Kuhusu vituo vya kulelea watoto yatima, kuna udanganyifu wa baadhi ya ndugu kuhusu watoto wanaopelekwa katika vituo vya kulelea watoto yatima na walioko katika mazingira magumu;

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumegundua kuna uchakavu mkubwa wa majengo katika Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Wananchi;

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa pia na tatizo lingine kubwa la upatikanaji wa ajira kwa vijana wanaomaliza katika Vyuo hivyo vya Maendeleo ya Wananchi; na

(f) Tatizo lingine tulilojifunza katika kutembelea vyuo hivyo, kumekuwa na uhaba wa vitendea kazi katika Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya Sanaa ambavyo viko katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2006, Kamati iliweza kushiriki semina mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Tuliweza kufanya semina kuhusu muundo na majukumu ya *SCCULT*. Katika semina hiyo pia kulitolewa mada kuhusu masuala ya *SACCOS* na uanzishwaji na uendeshaji wa *SACCOS* kibiashara;

(b) Tulifanya semina kuhusu muundo na majukumu ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Maendeleo ya Jamii yaani Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana;

(c) Vile vile Kamati ilifanya semina kuhusu masuala ya wasanii yaani wanamuziki, iliyoendeshwa na *Rulu-Promoters;* na

(d) Vile vile Kamati ilifanya semina kuhusu uchambuzi wa bajeti kwa mtazamo wa kijinsia na ndugu zetu wa *TGNP* waliisaidia sana Kamati kupata uzoefu katika eneo hilo la uandaaji wa bajeti kwa mtazamo wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati katika yale mambo yaliyojitokeza mwaka huo wa 2006 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *NSSF*, Kamati inalipongeza sana Shirika hilo la *NSSF* kwa kazi nzuri linayoifanya katika kuboresha utendaji wake wa kazi. Hata hivyo, Kamati inashauri:-

(a) Serikali kupitia Shirika la *NSSF* ijiwekee mikakati mahsusi ya kuongeza bidii katika kuhakikisha madeni yanakusanywa ili kuokoa fedha za wanachama zinazokaa muda mrefu kwa wadaiwa na hasa waajiri;

(b) Lakini Kamati pia imeipongeza *NSSF* kwa kufanya kazi nzuri kutokana na kuwekeza katika maeneo mbalimbali. Lakini Kamati iliishauri *NSSF* kuona namna ya kuhakikisha wanachama wananufaika na uwekezaji huo. Mfano *NSSF* iangalie jinsi ya kushirikiana na vyombo mbalimbali ili wanachama wake waweze kukopa fedha zao wakiwa bado na uwezo wa kufaidi mafao hayo kabla hawajawa wazee na hivyo kushindwa kutumia mafao yao vizuri kwa kuzingatia umri wao;

(c) Lakini vile vile kutokana na umuhimu na manufaa ya mradi wa ujenzi wa nyumba za bei nafuu kule Kinyerezi, mradi wenye nia ya kusaidia watu wenye hali ya chini, Kamati inashauri mradi kama huu usiishie Dar es Salaam tu uende hadi Mikoani na Wilayani na kuweza kuwasaidia wananchi na Watanzania wengine wanaohitaji misaada kama hiyo Mikoani na katika Wilaya zetu; na

(d) Kutokana na umuhimu wa Daraja la Kigamboni ambapo wananchi wa Kigamboni wanapata shida, Kamati inaishauri Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Fedha wanakamilisha taratibu za kuiwezesha *NSSF* kuendelea na ujenzi wa daraja hilo mapema iwezekanavyo ili kutimiza utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi iliyoainisha wazi kwamba *NSSF* itasimamia ujenzi wa daraja hilo kabla ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo la Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, pamoja na umuhimu wa vyuo hivyo katika kujenga uwezo wa vijana wetu, Kamati ilishauri mambo yafuatayo:-

(a) Serikali ivipe umuhimu unaostahili vyuo hivyo ili viweze kupata vijana wengi zaidi ikiwa ni pamoja na Serikali kuwa karibu navyo hasa katika ukabarati wa majengo na kuvipatia vitendea kazi vya kutosha katika kuwafundisha vijana wetu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, wanafunzi wanaosoma katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, ni mafundi katika fani mbalimbali, Serikali kupitia Halmashauri wanakotoka vijana hao ziwafikirie wahitimu katika kuwapatia zabuni zinazopatikana katika maeneo husika ili waweze kujitegemea na kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo na ushauri uliotolewa kwa ujumla katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Tatizo la upungufu wa watumishi katika Wizara hii ni la muda mrefu sana. Mahitaji halisi ya watumishi kwa mfano katika Wizara yetu ni 3,300 lakini watumishi waliopo mpaka sasa hivi ni 1,095 tu. Hivyo, Kamati ilishauri mambo yafuatayo katika kutatua tatizo hilo:-

(a) Serikali kuchukua hatua za haraka ili kumaliza tatizo kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika dhana ya kuleta maendeleo kwa jamii ya Watanzania;

(b) Pia Wizara ibadilike, iandae bajeti yake kulingana na mazingira ya sasa kwa kubuni namna mbalimbali za kuibua miradi kwa ajili ya kuwaendeleza vijana na akina mama. Aidha, Wizara ibuni shughuli za kimiradi zenye mitazamo ya maendeleo katika jamii mfano ili kuleta usawa wa kijinsia ni budi vitendea kazi kama matoroli na kadhalika vitumike kuhamasisha jamii kufanya kazi kwa pamoja kwa maana ya jinsia ya wanaume na wanawake kwa kushirikiana; na

(c) Serikali iondoe mtazamo kuwa Wizara hii haina majukumu mengi hivyo kuipa bajeti finyu kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilikuwa na maoni kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Kwa kuwa, mfuko huu ni muhimu sana katika kuendeleza wanawake nchini, hivyo basi Kamati ilishauri mambo yafuatayo:-

(a) Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kujenga mpango maalumu wa kupitia Halmashuri ili wanawake wasiofikiwa kabisa na wadau wa nje waelimishwe na Wizara yenyewe katika masuala ya ujasiriamali na hivyo kufaidi matunda ya mfuko huo.

(b) Kamati lakini ilishauri pia, Majumba ya Maendeleo ya Jamii yaliyoko katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu na ambayo yalikuwa yakitumika sana hapo zamani kwa ajili ya kuleta maendeleo, yafufuliwe kwa ajili ya kazi ya kuelemisha jamii stadi mbalimbali za maisha na ujuzi ili kuongeza ajira na tija katika uzalishaji miongoni mwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi zisizo za Kiserikali ambazo zinafanya kazi chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Taasisi zisizo za Kiserikali ni muhimu sana katika kuleta maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kuweka kumbukumbu za *NGOs* mahali zilipo, namna zinavyosaidia kuleta maendeleo katika jamii na ufuatiliaji wa utendaji wao wa kazi hasa kwa kuhakikisha kwamba zinawasilisha taarifa kama sheria inavyowataka na Serikali kufuatilia kwa makini kuona maendeleo yanayopatikana kupitia katika taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine lililopewa ushauri na Kamati yetu ni kuhusu vituo vya watoto yatima na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwepo na vituo vingi sana vinavyojihusisha na yatima na watoto waishio katika mazingira magumu, aidha, kumekuwepo na matatizo katika vituo hivi ikiwa ni pamoja na kutofanya kazi kwa manufaa ya watoto husika au kukosa vifaa na kuwaweka watoto hao katika mazingira duni sana hivyo Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(a) Serikali kupata takwimu ya vituo vya watoto yatima vilivyopo nchini vinavyosimamiwa na Serikali na watu binafsi;

(b) Serikali kufuatilia utoaji wa huduma inayotolewa katika vituo hivi kama kweli inawanufaisha wototo wenyewe ama inawanufaisha wanaomiliki vituo hivyo;

(c) Lakini Serikali iongeze idadi ya vituo vinavyohudumia watoto yatima vitakavyokuwa chini ya usimamizi wa Serikali yenyewe na sio kuviacha vingi mikononi mwa mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali; na

(d) Vilevile Serikali kutokana na ongezeko la kasi la watoto wa mitaani na ombaomba, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi kushughulikia tatizo hili ili kupunguza watoto wa mitaani na ombaomba katika mitaa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mikopo na akiba, kutokana na riba kubwa inayotolewa katika mikopo, vikundi vingi vya wanawake na vijana vinashindwa kumudu mikopo hiyo, hivyo basi Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(a) Serikali kuona uwezekano wa kupunguza riba ili mikopo iwanufaishe wananchi wa hali ya chini katika maeneo mengi ya nchi yetu;

(b) Elimu ya mikopo na biashara itolewe kwa wakopaji na elimu hii iende hadi vijijini kwa lengo la kuimarisha *SACCOS* mahali ambapo wanyonge wengi wangeweza kupata mikopo kwa urahisi zaidi;

(c) Serikali iangalie namna ya kuiwezesha *SCCULT* ili ijenge uwezo wa ndani kwa vyama vya akiba na mikopo nchini; na

(d) Waheshimiwa Wabunge nao kwa pamoja washirikiane na viongozi mbalimbali na wananchi wote waitikie wito katika kujiunga na *SACCOS* ili kuongeza idadi ya wanachama ambayo ndio nguvu kubwa ya *SACCOS* kwani idadi iliyopo sasa ni 255,164 ambayo ni ndogo sana ukilinganisha na wenzetu wa Kenya ambao wanaongoza kwa kuwa na idadi ya wanachama karibu 2,501,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu michezo, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi inayoonyesha katika kuendeleza michezo nchini. Hata hivyo, Kamati inashauri uhamasishaji huu uanzie katika shule za msingi ili kuweza kuibua vipaji mbalimbali vya vijana. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa ujenzi wa Uwanja wa Kimataifa ambao ni Uwanja wa Taifa Dar es Salaam. Pia Kamati inaishauri Serikali ione namna ya kuwezesha michezo ya aina yote kufanya vizuri katika nchi yetu ya Tanzania. Kamati inatoa ushauri kwa vilabu kuacha migogoro na hivyo kujenga uwezo wa michezo katika medani mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sanaa na utamaduni. Sanaa ni kitu kinachoonekana kusahaulika katika jamii yetu, hivyo basi, Kamati ilishauri mambo yafuatayo:-

(a) Serikali kuweka msukumo katika masuala ya sanaa ikiwa ni pamoja na kujenga majumba bora kwa ajili ya maonyesho ya sanaa.

(b) Lakini kwa kuwa, sheria ya haki miliki kwa wanamuziki inaonyesha kuwanufaisha zaidi *promoters* na *producers* kuliko wanamuziki wenyewe, Serikali ilete marekebisho ya sheria ili ilinde maslahi ya wasanii wetu na wanamuziki wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo Cha Sanaa Bagamoyo. Kwa kuwa, Chuo Cha Sanaa Bagamoyo ni muhimu sana katika kuendeleza sanaa hapa nchini, Kamati imesikitishwa sana na hali ya Chuo Cha Bagamoyo ambacho huko nje kinajulikana sana kwani wanafunzi wengi kutoka nje ya nchi yetu wamekuwa wakija kusoma katika chuo hicho lakini kwa kweli hakilingani na hadhi ya Kimataifa na hata hadhi ya jina lake. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ujenzi wa chuo hicho na ukarabati wa baadhi ya majengo ikiwa ni pamoja na kukipatia vitendea kazi ikiwemo gari kwani Kamati ilibaini kuwa chuo hiki hakina hata gari moja mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya mikakati ya kuongeza ajira, Kamati ilishauri yafuatayo:- Kamati inaipongeza Serikali kupitia Ilani ya Uchaguzi katika suala zima la kuongeza ajira hadi 1,000,000 ifikapo mwaka wa 2010. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kuweka mikakati madhubuti kwa ajili ya utekelezaji wa azma hii. Aidha, maeneo yote yanayoonekana kuelekea kutengeneza ajira yaainishwe na kuwekwa wazi. Vilevile Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kuangalia viwango vya mishahara na hasa kima cha chini. Kamati pia inashauri Wizara kuwa na mawasiliano na vyama vya wafanyakazi ili kutambua hali za wafanyakazi nchini. Tunaipongeza Serikali kwa kuwa tumeshaona suala hilo la Kamati limeshachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ongezeko kubwa la ajira kwa wageni nchini. Kwa kuwa kumekuweko na ongezeko kubwa la ajira kwa wageni hasa katika nafasi ambazo zingefaa kuajiri

Watanzania wenyewe, maeneo hayo ni kama biashara ndogo ndogo ya machinga, hoteli za kitalii, migahawa na kadhalika, Kamati haielewi ni kwa vipi wageni wamepata vibali vya kuingia nchini na kufanya kazi kama za umachinga wakati vijana wetu hawana kazi za kufanya? Hivyo basi Kamati inashauri:-

(a) Serikali kuwa makini kabisa katika utoaji wa vibali kwa wageni kuingia nchini kwa lengo la kufanya kazi na hasa zile kazi ambazo wakati mwingine vijana wetu wangeweza kuzifanya bila hata kupata utaalam wa juu.

(b) Aidha, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, ishirikiane na Kamati ya Kutoa Vibali kwa wageni kufanya kazi hapa nchini iliyoundwa ili kudhibiti tatizo hili katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilitoa maoni kuhusu Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi yaani *OSHA*. Kamati inaipongeza *OSHA* kwa kazi nzuri inayoifanya ya kuangalia usalama na afya ya wafanyakazi mahali pa kazi. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwepo kwa mapungufu katika Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi. Hivyo, Kamati inashauri:-

(a) Serikali kuharakisha sana kukamilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ili kuileta Bungeni na kuifanyia marekebisho na hivyo kuweza kutoa haki ya usalama huo kwa wafanyakazi wote katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania.

(b) Aidha, Kamati ilibaini kwamba *OSHA* ina wafanyakazi wachache sana na hivyo kusababisha viwanda na maeneo mengi ya kazi yasikaguliwe kwa wakati. Kamati inaishauri Serikali kuajiri wataalamu wa kutosha na hivyo kuyafikia maeneo mbalimbali ya kazi na kukagua usalama wa wafanyakazi mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika kwa umahiri wenu mkubwa katika kuliendesha Bunge letu. Aidha, nichukue nafasi hii kukupongeza sana wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa tena kuwa mjumbe wa *NEC* na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi ndani ya Chama chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Bunge na Mbunge kwa kufanya kazi nzuri za kuliendesha Bunge letu wakati wewe na Mheshimiwa Spika mnapokuwa hampo.

Aidha na mimi mwenyewe ninaomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuweza kuniunga mkono kwa hali na mali wakati ninapokalia Kiti, unapokuwa wewe ama Mheshimiwa Spika hayupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa ushirikiano walioipa Kamati yangu katika kutekeleza majukumu yake. Naomba niwatambue Mawaziri hao kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Kapteni John Chiligati, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Danieli Nsanzugwako, Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Joel Bendera, Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Naibu Waziri wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Naibu Waziri wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu wote pamoja na watendaji wa Wizara hizo husika kwa namna walivyotoa misaada ya kutosha na kushirikiana na Kamati kwa kikamilifu kabisa katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka huo wa 2006. Aidha, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Haroub

Masoud. Mheshimiwa Haroub Masoud amekuwa mahiri sana kuiendesha Kamati hii kila mara ninapokuwa na majukumu mengine na ameweza kushirikiana vizuri sana na Wajumbe wa Kamati yetu. Vile vile napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa ujumla kwa kufanya kazi kwa moyo na kwa utiifu mkubwa katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Bwana Damian Foka, kwa ushirikiano mzuri alioutoa katika Kamati yangu wakati wote katika kufanikisha majukumu yetu. Lakini si kwa umuhimu mdogo, lakini kwa nafasi ya pekee, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Katibu wangu wa Kamati, Ndugu Lawrance Robert Makigi na leo yuko hapo Mezani, kwa kweli amefanya kazi kubwa sana ya kuihudumia Kamati kwa makini ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa mbalimbali ikiwemo pia taarifa hii ambayo leo nimeiwasilisha mbele ya Meza yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa Bunge lipokee na kuikubali na kuijadili taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB S. MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupewa nafasi hii na kuwa wa kwanza katika kuchangia mada hii ambayo ni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii ambapo mimi mwenyewe ni Mjumbe wa Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwa niaba ya wananchi wangu wa Makete kwa kufuatia kifo cha Mheshimiwa Salome Mbatia, ambacho kwa kweli kimesikitisha wananchi wangu wa Makete. Kwa hiyo, kwa niaba yao, naomba nitoe rambirambi hizi kuungana na Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nataka nitumie nafasi hii kutoa pongezi nyingi sana kwa Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu, kwa kumchagua Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa kura nyingi na za kishindo. Niwapongeze wale wote ambao wamechaguliwa kuwa wajumbe wa Halmashauri Kuu na kuwa Wajumbe wa Kamati Kuu. Nawapongezeni sana bila kusahau kumpongeza sana dada yetu Anna Makinda, ambaye ni Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia hoja yangu hasa kwa kuzingatia kwamba Wizara ya Maendeleo ya Jamii ambayo ndio msimamizi Mkuu wa Vyuo Vya Maendeleo ya Jamii. Sasa tunatakiwa tufike mahali tuseme ukweli na tuangalie tunakotaka kwenda ni wapi. Asubuhi tumeambiwa vyuo hivi viko 58 na tulipokuwa tunatembelea kama alivyosema Mwenyekiti, Misungwi, kuna hivi vya Kibaha na Tengeru, tukagundua vyuo hivi vina matatizo mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile ukiangalia katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005, iliainisha kabisa kwamba moja ya malengo makuu ambayo yanatakiwa yatekelezwe ni pamoja na kuwa na vyuo vya *VETA* katika kila Wilaya. Sasa ukiangalia vyuo hivi vyenye mtandao ambapo viko 58 na ambavyo vina matatizo ya Walimu, matatizo ya vifaa na majengo kuchakaa, tulikuwa tunadhani kwamba huu ni mtandao muhimu sana ambao kama tungekaa na kujadili tukaona namna ya kuvihamisha viende kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na vile ambavyo viko juu kidogo kama Tengeru viende kwenye Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, ingesaidia

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo sababu, kwanza usimamizi mkuu wa elimu inatakiwa uwe katika sehemu moja yaani uwe kwenye Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambapo Wizara hizi ndio unakuta kuna vyombo vikuu vya kusimamia taaluma kama vile *TCU (Tanzania Commission for Universities), NACTE (National Council for Technical Eductaion)* na *VETA (Vocational Education Training in Tanzania)* ambayo iko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili kuweza kusimamia vizuri viwango hivi vya elimu, ni vizuri usimamizi ukawa ni mmoja maana hizi taasisi za elimu ziko katika Wizara hizi mbili. Lakini vilevile tukifanya hivyo tutakuwa tumefanikiwa kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kuwa na Vyuo vya Ufundi vya *VETA* vingi kwa wakati mmoja, ikiwezekana mpaka kufikia 2010 tukawa navyo vingi sana. Serikali sasa ingeelekeza nguvu zake baada ya kuchukua vile ambavyo vipo kwa mfano ukichukua Misungwi ambacho mafunzo yanayotolewa pale yanalinganalingana kidogo na mafunzo ya *FTC* ambayo sasa hivi ni *Ordinary Diploma* basi kile chuo nacho kingeweza kukabidhiwa kwenye Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kikawa kama *Technical College* ambapo tayari *zone* ya Mwanza ingekuwa na chuo cha ufundi kama hicho. Lakini vile vile Serikali ingeelekeza nguvu zake sasa kwenye zile Wilaya ambazo hazina vyuo vya ufundi kwa kujenga Vyuo vya Ufundi vya *VETA.* Baada ya kuchukua hivi 58 na vile ambavyo vinajengwa kwenye Kata na Wilaya basi idadi itakuwa kubwa zaidi. Hiyo ni hoja yangu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ni kuhusu hizi *NGOs*, taasisi ambazo sio za Kiserikali. Kimsingi, zinasaidia sana na nyingi zinasajiliwa katika kutekeleza malengo yake ya kusaidia hasa sekta ile ya watoto yatima na maeneo yanayohusika katika eneo hili. Sasa kumekuwa na tatizo mara nyingi hizi taasisi zikishasajiliwa zinafanya mambo mengi ambayo ni mazuri kwa jamii lakini ziko nyingine ambazo malengo yake hayatekelezwi kwa sababu zile huduma ambazo anakuwa amepewa haziwafikii walengwa. Kwa hiyo, hapa pendekezo langu ni vizuri Serikali ikasimamia kwa karibu sana hizi *NGOs* hata kama hakuna sheria inayosema kwamba lazima zikaguliwe na Serikali, basi kuna haja ya kuona ni namna gani hawa wanaweza wakaangaliwa kwa karibu zaidi ili kuona kwamba ile misaada inawafikia walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo mifano michache, mnapochanga michango ya harusi kunakuwa na Kamati za Harusi na kwa kweli hii michango inachangwa vizuri sana na zile hela zinatumika vizuri sana kwa sababu kulikuwa na ushirikiano mzuri katika uchangaji na Kamati zinatoa ripoti ambazo ni sahihi na za uwazi. Lakini katika hizi *NGOs* utakuta ziko ambazo zinafanya mpaka harambee na kualika viongozi mbalimbali wakubwa lakini baada ya hapo hakuna mkono wa Serikali wa kufuatilia kwamba ile harambee iliwafikia wananchi au vipi? Mara nyingi harambee yoyote inapofanyika mtu anaitumia kwa kutaja wale walengwa kwa mfano watoto yatima na hivyo wananchi wanaposikia taarifa kama hizi wanakuwa wanapenda kujua kile kiwango kilichopatikana kilitumika vipi? Kwa hiyo, napendekeza kwamba ni vizuri kwenye shughuli kama hizi Serikali pia iweze kufuatilia na kuona, je, michango hii ambayo ilikusanywa ina uwazi gani na wananchi wanaweza kuwa wamefaidi kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile najaribu kufuatilia suala hili la ujenzi wa barabara ya Kigamboni kwa sababu ni suala ambalo limeongelewa sana. Sisi Kamati ya Maendeleo ya Jamii, wakati tunapitia ripoti za hii *NSSF* walionyesha jinsi walivyo tayari kujenga daraja hili lakini mpaka sasa hatujaona taarifa au tamko rasmi toka Serikalini kwamba ni kwa namna gani wako tayari kujenga daraja hili? Mpaka sasa hakuna Mkandarasi ambaye ametajwa, kumekuwa na vitu ambavyo havieleweki. Nadhani ni vizuri kabisa tukaiona hiyo ratiba na ikajulikana kama ni *NSSF* atasimamia ili kazi ianze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuchangia ni kuhusu huu Uwakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (*OSHA).* Hii ni taasisi muhimu sana lakini ukiangalia sana haijapewa uzito hata kidogo kwa sababu hawa ndio wanaokagua mahali popote kiwanda kinapoanzishwa na kuidhinisha kwamba ile mitambo ifungwe. Mahali popote kazi za ujenzi zinapofanyika, hawa ndio wanaokagua na kuona kwamba sheria na taratibu *(safety precautions)* katika sehemu za kazi zinafuatwa. Lakini hawana wataalam, bajeti yao ni ndogo, vifaa hawana, hata magari hawana na ndio maana unakuta sehemu nyingi sasa majengo yanaungua kwa sababu inawezekana viwanda vile vilianza bila kuchekiwa vizuri zile *connection* za umeme na vitu vingine kama mitambo. Ukienda katika *site* mbalimbali watu hawavai zile kofia za kuzuia mawe kuanguka, watu wanavaa viatu vya kawaida, ni kwa sababu hakuna msimamizi wa karibu. Kama alivyosema Mwenyekiti wetu kwamba kama ingekuwepo hiyo sheria basi kwa kupewa uwezo zaidi hawa wangeweza kuwasimamia na kutoza *fine* na vitu mbalimbali ili matatizo kama haya yasitokee mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile nimshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kutoa taarifa yake vizuri na nimpongeze sana kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa .

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika taarifa hii ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, kwanza naungana na wenzangu kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mbatia. Vilevile natoa pole kwa wale wote waliofiwa na kwa wale wote waliopata ajali mbalimbali na Mungu atawapa afya njema. Lakini vilevile bila kusahau, natoa pole maalum kwa Kiongozi wangu wa Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mungu ampe afya njema na uwezo katika *operation* yake inayofanyika huko India.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nataka na mimi nichangie machache katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninapenda nichangie katika suala zima la watoto wanaoishi katika mazingira magumu na watoto ambao ni yatima. Taifa letu limeshuhudia kwa muda mfupi watoto wengi sana walioathirika na wazazi wao kufa na UKIMWI na wengine wametengwa na wazazi wao na kuwafanya wanahangaika mitaani. Hivi vyama au vyombo ambavyo wamejitolea kukusanya watoto hawa na kuwalea, tusione kwamba baadhi yao labda wanataka kufaidika tu, ukweli ni kwamba watu hawa wamejitolea inabidi tuwaunge mkono na tuwapongeze kwa kuacha kazi na kuamua kuwakusanya watoto wa aina hii na kuanza kuwalea na jamii nzima inatakiwa tuwaunge mkono katika suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuishauri Serikali kwamba sasa umefika wakati lazima itenge fedha za kutosha kwa Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kwa sababu gani nasema hivyo? Kwa sababu kundi la watoto ambao wanahitaji msaada ni kubwa sana na wananchi peke yao hawawezi na Serikali ina sehemu chache tu ambazo imetenga kwa ajili ya kuwalea watoto hao. Kwa hiyo, Serikali sasa itafute maeneo makubwa ili ijenge majengo ya kudumu na kuanza kuwalea watoto hawa katika mazingira mazuri ili wasome humo na vilevile wakue humo ili iwasaidie katika maisha yao ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumzia suala zima la daraja la Kigamboni. Daraja la Kigamboni mara kwa mara tumekuwa tunasikia likizungumziwa ndani ya Bunge hili, hili daraja ni muhimu sana. Sasa hivi Serikali imetoa viwanja sio chini 20,000 Kigamboni ambavyo Watanzania na wananchi wanategemea kujenga kule lakini jinsi gani watapitisha sementi zao kwenda kule na jinsi gani watapitisha vifaa vyao itategemea sana kuwepo kwa daraja hili. Pamoja na kuwa kuna njia ambayo inapita Mbagala lakini njia hiyo ni ndefu na itamgharimu mjenzi gharama kubwa kitu ambacho si sahihi. Kwa hiyo, napenda kutoa changamoto kwa Wizara ya Fedha na Wizara zinazohusika kwamba *NSSF* sasa imefika wakati lazima jambo hili lipewe umuhimu mkubwa sana ili itekeleze azma yake ya kujenga daraja hili na wananchi waanze kujenga maeneo hayo, waondokane na adha ya kutegemea kivuko cha kuhatari maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kusema maneno hayo kuhusu daraja lakini vilevile napenda sana kuzungumzia Vyuo vya Mafunzo vya Wananchi, vyuo hivi kwa kweli ni muhimu sana na Serikali imeanzisha vyuo hivi ili kuwapa elimu wananchi katika masuala mbalimbali ya kiufundi na kijamii, sasa ni vizuri vyuo hivi vikapata vitendea kazi vya kutosha. Tumesikia hapa katika hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati alipokuwa anasema kwamba vyuo vipo, mafunzo yanatolewa lakini vitendea kazi hamna. Kwa kweli suala hili ni la aibu sana.  Ndio maana vijana wetu wanakwenda katika mafunzo na baada ya kumaliza mafunzo wanapoomba kazi wanakosa ajira kwa sababu hawakupata mafunzo yanayotakiwa katika ajira ile mtu anayoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili, tuangalie ni kwa nini wageni sasa hivi ndiyo wanaochukua nafasi kubwa katika ajira kwenye maofisi ya Serikali na hata kwa watu binafsi? Mimi

napingana sana na ile dhana ya kusema kwamba wageni ndiyo wamesoma vizuri, sikubaliani nayo kwa sababu kuna vijana wetu wengi wamemaliza Chuo Kikuu wana *Degree* wana *Master* zao lakini hawapati kazi katika vyombo vya Serikali. Wakiomba kazi mtu anaulizwa ana uzoefu gani, mtu katoka Chuo Kikuu, hivi uzoefu ataupata wapi bila Serikali yenyewe ya Watanzania kumuajiri yule Mtanzania ili awafanyie kazi Watanzania? Hili suala lazima liangaliwe kwa sababu vijana wengi wanakosa ajira. Tunasema Watanzania hakusoma, vijana wengi wamesoma, wako mitaani na vyeti vyao lakini kazi inatangazwa Serikalini akienda hawezi kupata ile kazi ya Serikali kwa sababu tu hakupata mtu wa kumshika mkono, hili jambo lipo na naomba lifanyiwe utafiti wa kina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wa kujenga nchi hii wapo, vijana waliosoma wapo wala si kweli kwamba mtu aliyetoka Kenya au Uganda ndiyo kasoma vizuri, hapa hapa Tanzania tunashuhudia wananchi kutoka nchi hizo wanakuja kusoma Vyuo Vikuu vya Tanzania na nchi zingine za Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia suala hili la vijana na ajira sasa tuangalie wale wageni ambao sasa hivi wanakuja katika nchi na wanafanya kazi hizi ndogo ndogo. Ukienda Kariakoo utashuhudia asilimia kubwa ya wageni ambao wako pale na Serikali lazima sasa ifanye utafiti wa kina kuthibitisha je, haya yanayosemwa katika Bunge au yanayosemwa na wananchi, ni sahihi? Kuna wageni ambao wanaharibu biashara kabisa za wananchi wetu na za vijana wetu. Anatoka hapa Mtanzania anakwenda mpaka nchi ya nje kuchukua biashara anaileta lakini kwa mfano Wachina biashara ile ile anayoiuza Mtanzania yeye hapa hapa anazungumza China inakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nenda kuchukue hicho kiatu alichokileta Mchina, ukikivaa kiatu hicho na kutembea kutoka hapa nilipo Mheshimiwa Naibu Spika nikifika kwako, kiatu kishatoka soli. Kwa hiyo, tuangalie vitu hivi, watu wanalalamika sio kwamba wanalalamika kama vile hawana akili ni ukweli kwamba tunawadhohofisha watu wetu. Tunasema tunataka kuwasaidia wanawake na vijana katika ajira, tunatoa mikopo kwa vijana wetu ili wafanye biashara na wajiendeleze katika maisha yao lakini biashara hizo wanazifanya vipi bila Serikali kuwalinda vijana wetu ambao wanafanya biashara hizi kwa kutumia mikopo hii ili waweze kurudisha mikopo badala ya kuwa wanaadhirika baada ya kushindwa kurudisha mikopo kwa kuchukuliwa bidhaa zao au kuuliwa mtaji wao ambao wanakuwa nao?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili mimi nasikia uchungu sana na mimi niko tayari, nataka Waziri akija hapa atueleze ni hatua zipi ambazo zimechukuliwa katika kushughulikia suala hili. Hili suala linawakera sana wananchi na wameshawahi kuja mpaka hapa Dodoma kuleta malalamiko yao kwamba kuna kero ya wafanyabiashara hawa, tunasema wawekezaji, wakiomba ishughulikiwe. Naomba suala hili lichukuliwe uzito wa juu kabisa ili kuwaokoa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nina suala moja ambalo nataka Waziri baadaye anipe ufafanuzi kuhusu lile daraja la Kigamboni, tuambiwe daraja hili rasmi litaanza lini kujengwa kwa awamu ya kwanza? Naomba sasa suala hili nipatiwe ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii, kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niseme machache kuhusiana na taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kuchangia, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mwenyekiti ambaye amewasilisha taarifa hii hivi leo hapa Bungeni kwa uwasilishaji wake mzuri sawa na anapokalia Kiti kuliongoza Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nichukue nafasi ya kutoa pole kwa wale wenzetu ambao wamefikwa na maafa mbalimbali wakati tukiwa katika harakati hizi za Bunge na vile vile nje ya Bunge lakini wakiwa ni Wabunge wenzetu, wote nawapa pole kwa jumla na Mungu atawasaidia na wale waliokuwa hospitalini, Mungu atawapa nafuu ili waje waungane nasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia maeneo kama manne hivi ili nami niweze kuboresha zaidi taarifa hii na vile vile kuona kwamba pale kwenye upungufu Serikali iweze kuchukua hatua kwa nia

moja tu ya kuleta manufaa kwa Watanzania ambao tunaishi katika Jamhuri yetu hii ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na watoto yatima. Katika taarifa hii umezungumzia juu ya watoto yatima na watoto wa mitaani lakini si kwenye taarifa tu, watoto hao wamekuwa wakizungumzwa sana katika Bunge letu Tukufu na kuitaka Serikali ichukue hatua ya kuwaangalia watoto hawa ili na wao waishi katika nchi hii wakijadai kwamba wako katika Jamhuri yao ya Muungano wa Tanzania. Lakini tatizo lililokuwa hapo ni baadhi ya vituo wenzetu wamegeuza kama ni vitega uchumi. Sikatai kwamba watu hawa wasiungwe mkono na Serikali hapana, waungwe mkono kwa sababu wanafanya kazi nzuri ya kuwalea watoto wetu lakini na wao basi mkazo mkubwa watilie zaidi katika kuangalia hawa watoto kuliko kuangalia maslahi yao binafsi. Kwa sababu kufanya hivyo lile lengo litakuwa halifikiwi na lengo ni kuwaangalia watoto hawa katika suala la elimu na kuwatunza vizuri ili wawe na maadili mazuri, hapo ndipo tutapata vijana ambao wanaweza wakatusaidia sana katika nchi yetu Tanzania. Sasa wale wenzetu ambao wameanzisha vituo hivi badala ya kuwasaidia watoto wanaweka zaidi maslahi mifukoni mwao, ombi langu kubwa ni Serikali itupie macho suala hili kwa sababu kama haikuwa karibu, yale yote ambayo tunataka tuyatimize kwa watoto hawa, yatakuwa hayawezi kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi, naomba Serikali basi hivi sasa ianze kuratibu au iweke Kitengo Maalum cha kuweka kumbukumbu na mienendo ya vijana hawa, maendeleo yao kuanzia utotoni, wakiwa shuleni na hata wakimaliza shule. Kwa kufanya hivyo ndipo Serikali inaweza kwenda kifua mbele na ikajidai kwamba tumetunza vijana wetu na kuwahudumia vizuri na kuwapa masomo na kila kitu na hatimaye basi mmoja kati ya vijana hawa tunamuona siku nyingine ameingia humu Bungeni akiwa ni Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hapo Serikali itajidai lakini ikiwa tutaacha kuwafuatilia vijana hawa kwa sababu wanalelewa na watu fulani basi tutakuwa bado hatujaweza kufanya lile jambo la msingi linalotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mifano miwili. Juzi tulisikia kwenye taarifa mbalimbali kuna mwenzetu mmoja bahati mbaya amefungwa kule Gerezani lakini kufungwa kwake hakujamzuia kujiendeleza amejiendeleza na juzi ametunukiwa Shahada ya Sheria. Sasa ile ni moja katika mambo ambayo yanaleta sifa kwa Serikali kwamba Magereza yetu sio ya kutesa tu, hapana, yanatoa nafasi kwa watu wengine kujisomea ndani ya Magereza na hatimaye kupata Nishani au Shahada inayotambulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa upande wa hawa vijana wetu hawa basi siku moja tusikie katika kumbukumbu ya 1973, kijana huyu siku moja akawa Waziri, hakuna kosa, itakuwa ni Serikali ambayo itajidai kwamba imeweza kutunza vijana wa aina hii au kuwaangalia vizuri na kuweza kupata vijana ambao tunataraji waje kuwa viongozi bora katika nchi ya Tanzania badala ya kuwa vijana wanao dhurura hovyo, wala unga na wasiosaidia Taifa hili. Naomba Serikali ikaliangalia vizuri suala hili na kuweza kuwa na kumbukumbu ambazo zinaweza kusaidia hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano hai, kule Zanzibar mwaka 1964, ilifunguliwa nyumba maalum ya kulelea watoto na wale ambao walishindwa kuwalea watoto wao walikuwa wamewekewa chombo maalum pale chini kwenye ngazi, ikiwa humtaki mtoto unamweka pale mezani, italia kengele juu, anakuja kuchukuliwa. Watoto hawa sasa hivi wako katika Mawizara mbalimbali wanafanya kazi. Sasa ile ni fahari ya Serikali na inajulikana kwamba mtoto huyu ametoka mahali fulani lakini yuko Wizarani anafanya kazi kama Naibu Katibu Mkuu au Mkurugenzi. Sasa tukiwaacha tu hivi itakuwa hatuwasaidii inabidi sasa tuchukue mifano hii ili tuweze kuona basi na hawa vijana wetu tunaweza kuwalea vizuri katika mazingira ya Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nizungumzie suala *SACCOS*. Katika Tanzania tumeanzisha *SACCOS*, kwa kweli ni jambo la kufurahisha na ni jambo linalosaidia sana Watanzania lakini hasa akina mama wamepata mwamko sana wa *SACCOS* lakini *SACCOS* mwamko mkubwa uko Bara. Ombi langu hapa kwa Serikali ni kwamba mafunzo ya *SACCOS* bado yanahitajika sana kwa Tanzania Zanzibar ili watu wapate mwamko zaidi na hasa akina mama wa kujiunga katika *SACCOS* mbalimbali na kuweza kujitegemea na kufanya shughuli zao na kuacha utegemezi kutoka kwa akina baba ambapo kila siku akina mama hao wako nyumbani, maskini wengine wameolewa lakini hawana shughuli ya kuifanya, sasa *SACCOS* zitasaidia sana. Naiomba Serikali iweke mkazo zaidi wa Walimu wa *SACCOS* Zanzibar, ni

wachache mno, hawatoshi, watu wana mwamko mkubwa lakini bado hakujawa na Walimu ambao wanaweza wakasaidia katika Majimbo yetu, katika jamii yetu na katika maeneo yetu mbalimbali ambapo watu wanahamu ya kuanzisha *SACCOS* lakini hawajui waanze wapi? Sisi Wabunge tunafanya kazi ya kutoa elimu ya *SACCOS* lakini bado tunataka wataalam ambao wataweza kusaidia zaidi katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, napenda kuzungumzia suala la michezo. Kwenye taarifa hii, tumeambiwa Kamati imetembelea sehemu mbalimbali kwa mfano Baraza la Michezo na sehemu nyingine na Serikali imepongezwa. Vilevile na mimi nataka niipongeze Serikali kwa kujenga Uwanja mpya wa Taifa hapa Tanzania. Naipongeza na naishukuru sana kwa kitendo kile ambacho kimeleta haiba na sura mpya kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kitendo kizuri kwa Afrika Mashariki na Kati lakini pia ni kitendo kizuri kwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kujenga Uwanja wa Taifa bila kuutumia kwa kufuata taratibu za michezo yenyewe, itakuwa haijasaidia. Hivi sasa tumeshuhudia ligi hizi zinazoendelea, Serikali bado haijakubali kuutumia uwanja ule na mimi sijakataa wala siilaumu Serikali kwa kuzuia timu zetu zisicheze kwanza pale, naunga mkono sana kwa sababu gani nina hakika kuna watu wetu wanapenda mpira lakini sheria hawazijui. Ulitokea mfano mdogo tu kulikuwa na mechi moja ya kirafiki ilichezwa katika uwanja ule hata haujafunguliwa na Serikali lakini vyoo vilivunjwa, vioo vikavunjwa, madirisha yakavunjwa, milango ikang'olewa, watu wakaiba mifereji, sasa hapa lazima tuwe tunatoa kwanza elimu kwa watu wetu ya kuthamini kitu chake lakini elimu pia ya kuona kwamba yuko katika kitu ambacho yeye anatakiwa akilinde. Sasa vyombo vyetu vinavyohusika na mambo yale lazima vichukue nafasi ya kutoa elimu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo ninapenda nilizungumzie ni lile la Sheria za Michezo. Sheria za Michezo ambazo zimezungumziwa humu kwenye taarifa hii inatakiwa zianzie shuleni. Sasa hivi tusizungumzie Sheria za Michezo barazani tushakuwa watu wazima, tushaingia Bungeni ndiyo unamtaka Mbunge ajue Sheria za Michezo na bahati nzuri kila Mbunge hapa ana mapenzi yake, tabu kidogo. Sasa ninaomba Serikali hizi Sheria za Michezo hasa mpira wa miguu zianze shuleni ili vijana wetu hao tunaotarajia kuwa na vipaji watakapoondoka shuleni wawe wanajua sheria hizi kumi na saba zikoje?

Lakini vijana peke yake wa shuleni hawatoshi, hakuna watu wabaya katika kuanzisha vurugu katika michezo kama Watangazaji na Waandishi wa Habari. Watangazaji na Waandishi wa Habari ni vichochezi vikubwa sana katika mambo ya michezo. Kwa bahati mbaya baadhi yao, narudia tena baadhi yao hawajui Sheria za Michezo. Utasikia Mtangazaji anasema kwamba *Referee* kachezesha vibaya wakati yeye mwenyewe hajui. Ukimuuliza hiyo sheria inasemaje, hajui jinsi ya kuitafsiri. Sasa basi Serikali na Wizara husika ifanye bidii ya kuwapa elimu ya sheria Watangazaji na Waandishi wa Habari. Lakini pia hawa hawatoshi kama tunataka kuwa na wachezaji wazuri, Wachezaji wa Timu yetu ya Taifa nao wafundishwe sheria, ndipo tutakapoweza kuwa na mafanikio mambo ambayo yanaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa ninavyoongea, Wachezaji wa Timu ya Taifa wanacheza mpira kwa kuupiga uende mbele, hawajui sheria. Ni aibu kumuona Mchezaji wa Timu ya Taifa, *Referee* ananyoosha mkono kuonyesha kwamba ni *indirect free kick* lakini kwa sababu anajiona ana nguvu anakwenda kupiga shuti lake likikataliwa goli, anampiga *Referee*. Sasa lazima tuondoke katika hali hii, huu si wakati tena wa fujo katika viwanja. Ni lazima Serikali ifanye bidii kuanzia shuleni kwenye timu zetu za vijana na kuwepo watu maalum wa kutoa taaluma katika vikundi hivi ili tufike mahali tuweze kuokoa Taifa ili liweze kuondokana na vurugu na kupigana katika michezo, michezo ni furaha ni si ugomvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii. Naomba nianze kwa kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hii kwa ku-*present* taarifa yake vizuri sana na kwa ufasaha. Kama tunavyomfahamu, Mwenyekiti wa Kamati hii ametukuka kiuongozi wa Kamati mbalimbali na wote tunafahamu ukimwachia Kiti Mheshimiwa Naibu Spika huwa anatuongoza vizuri sana katika Bunge lako Tukufu, nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kwa kuishukuru Kamati kwa kufanya kazi yake vizuri katika kuishauri na kuisimamia Serikali katika mambo mbalimbali. Kamati hii ina Wizara tatu lakini imefanya kazi yake vizuri kama ilivyotoa taarifa yake. Lakini pia naomba niishukuru Serikali kwa kuingiza *SACCOS* zetu moja kwa moja katika awamu hii ya pili ya mikopo inayotambulika kwa umaarufu wa jina la mabilioni ya JK.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu ya kwanza ya mikopo, Wilaya yetu ya Namtumbo tulipata shilingi milioni 18 tu na sababu ya kukosa pesa wananchi wengi wa Wilaya ya Namtumbo ilikuwa ni kukosekana kwa Benki kwa sababu ya upya ya Wilaya yetu. Hali hii ilisababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi wa Wilaya ya Namtumbo wa kutoielewa Serikali kwani wengi wao hawakuipata mikopo hii. Lakini kwa ushirikiano mkubwa nilioupata kama mwakilishi wa wananchi wa Wilaya ya Namtumbo kwa uongozi wa Mkoa, uongozi wa Wizara, chini ya Mheshimiwa Chiligati na Naibu wake Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi mpaka sasa katika awamu hii ya pili, *SACCOS* zilizo chini ya Mtandao wa Dunduliza, zimeingizwa katika awamu hii ya pili na hivyo tunaishukuru sana Serikali. naiomba Kamati kuendelea kuishauri na kuisimamia Serikali ili kuhakikisha fedha hizo kweli zinawafikia wananchi na kama ilivyokusudiwa kwa riba nafuu *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna *SACCOS* zingine zilizoko katika Wilaya ya Namtumbo, Songea Mjini, Songea Vijijini haziko katika Mtandao wa Dunduliza. Tunaiomba Kamati iisimamie Serikali kuhakikisha *SACCOS* hizo nazo zinaingizwa na kupata pesa hizi moja kwa moja kuliko kupitia Benki ili kuwapunguzia mzigo wa riba wanachama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la michezo, mwenzangu Hafidh Ali amelizungumza vizuri sana kwani yeye amebobea sana, ni Kocha wetu Msaidizi na pia mwanataaluma mzuri wa michezo. Lakini mimi pia naomba niikumbushe Serikali, niliuliza swali la nyongeza kuiomba Serikali kwamba kwa kuwa Serikali imesharudisha michezo shuleni ianze kutafuta wale wachezaji wa zamani waliokuwa na uzoefu ili waweze kuwapa taaluma ya muda mfupi na kuwakumbusha sheria zile mbalimbali watoto wetu. Kwa hiyo, naiomba Kamati isimamie na kuishauri Serikali ili waweze kuwatafuta watu hawa, tunao wenye uzoefu, wajuzi wa michezo hususani wa mpira wa miguu na *netball* ili waweze kwenda kufundisha vijana wetu katika shule zetu. Tunaamini kabisa watasaidia kukuza taaluma hii ya michezo na kusaidia kupata wachezaji bora na kurudisha katika mstari nchi yetu ya Tanzania na katika medani ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni huo tu, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Naomba nianze kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Iringa kuwapa pole wale wote waliopata misiba na ajali mbalimbali ambazo zimetokea katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze pia kwa kumpongeza Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kura nyingi alizozipata na za kishindo na wale wote waliokuwa wanagombea nafasi ya *NEC* pamoja na wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kura nyingi ulizozipata na hatimaye kuchaguliwa kwenye Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja ambayo imetolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii na nimpongeze kwa kazi nzuri ambayo amefanya pamoja na wajumbe wote wa Kamati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la Vituo vya Watoto Yatima. Naipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanya katika kuangalia masuala ya watoto yatima lakini zaidi napongeza vituo mbalimbali ambavyo vinaendeshwa hapa nchini vingi vyake vikiwa ni vya Mashirika ya Dini ambavyo vinaangalia malezi ya watoto yatima na wale waliopo katika mazingira magumu. Vituo hivyo ni pamoja na vituo mbalimbali vilivyopo katika Mkoa wa Iringa vikiwemo Tosamaganga, Kipengere, Bulogwa, Mafia na vingi vinginevyo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vituo hivi vimekuwa vinafanya kazi kubwa ya malezi na kama tulivyosema watoto wengine ni wadogo, vituo vingine vinapokea watoto hadi wa siku moja na vingi vimekuwa vinafanya kazi hiyo kwa kutumia rasilimali zake ndogo walizonazo na kwa kupata mchango mdogo kutoka Serikalini. Mimi nafikiri sasa ni wakati ambapo Serikali inabidi iongeze ruzuku kwa vituo hivyo. Kwa sababu sio vituo vyote vinavyopokea ruzuku kutoka Serikalini, nawaomba waangalie utaratibu kama ambavyo Serikali inatoa ruzuku kwa Hospitali Binafsi na za Mashirika ya Dini kwa kufuata wagonjwa au idadi ya vitanda vilivyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia vituo hivi vipewe ruzuku kwa kuangalia idadi ya watoto waliopo katika vituo hivyo na wazingatie watoto wanaopelekwa kwenye vituo hivyo wengine wana mahitaji maalum. Watoto wengine ni wagonjwa, watoto wengine wana ulemavu wa aina mbalimbali, lakini wapo pia watoto ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI na maana yake ni kwamba wanahitaji matibabu, wanahitaji lishe bora na lishe bora hiyo saa nyingine inakuwa vigumu sana kwa vituo vyenyewe kuweza kumudu.

Kwa hiyo, naiomba kabisa Serikali iangalie na niiombe Kamati ya Maendeleo ya Jamii iweze kuangalia kwa undani huduma zinazotolewa katika vituo hivi, wasiangalie tu kwamba vituo vyote vinafanana lakini vituo hivi vina watoto ambao wana mahitaji maalum kwa maana hiyo, gharama za uendeshaji zinakuwa kubwa. Kwa hiyo, naomba waongezewe ruzuku na ruzuku hiyo itolewe kwa kila kituo lakini kwa kuangalia idadi ya watoto waliopo na mahitaji yao mbalimbali waliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo pia tuangalie hivi vituo, hawa watoto waliopo kwenye hivi vituo wanaishia wapi? Sasa hivi kuna wasiwasi hapa duniani kwamba kuna usafirishaji wa watoto, sijui sisi tumechukua mikakati gani ya kufuatilia ili kuona wale watoto waliopo kwenye vituo mbalimbali wanalelewaje? Je, tunajua kwamba wale wanaoondoka kwenye vile vituo wanakwenda wapi? Tunahitaji kufanya utafiti wa kina kuweza kujua kila mtoto aliyepo kwenye kile kituo je, kama yupo ni kweli yupo pale kituoni na kama ameondoka pale kituoni amekwenda wapi ili tuweze kuwalinda watoto hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba tumezungumzia watoto yatima lakini hatujazungumzia watoto yatima waliopo majumbani, tumezungumzia watoto yatima waliopo kwenye vituo. Watoto yatima waliopo majumbani ambao wengine wanajilea wenyewe na wengine wanalelewa na walezi wao ambao aidha ni wagonjwa au ni wazee, hatujawazungumzia. Tunahitaji kuweka mikakati maalum ambayo inaweza kuwasaidia hawa walezi wa watoto. Aidha, Serikali iweke utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba hawa walezi wanapewa huduma na wanasaidiwa kwa sababu wengine wameelemewa na mzigo wanalea hawa watoto kwa raslimali zao wenyewe na wakati mwingine wao wenyewe hawana hizo raslimali na matokeo yake ni kwamba hawa watoto wengine wanaondoka na kwenda mitaani.

Kwa hiyo, tunalo jukumu la kuangalia hawa watoto ambao wapo kwenye jamii, wanaolelewa na familia nilizozitaja, wanawekewa mazingira gani ili na wenyewe waweze kuishi kama watoto wa kawaida kwa kupatiwa huduma mbalimbali ikiwemo matibabu. Sielewi ni kwa nini hatuweki utaratibu wa kuhakikisha hawa watoto tunawawekea bima yaani watoto wote wapate huduma za matibabu ambazo zinaweza kuwa zimelipiwa kwa sababu wakati mwingine ni vigumu sana mlezi kuweza kumudu matibabu ya hawa watoto? Kwa hiyo, ninaomba Kamati pia itusaidie kwa hili lakini Serikali iangalie utaratibu mzuri ambao unaweza kusaidia zaidi ikiwa ni pamoja na kuwa na Kamati za Watoto Vijijini. Sasa hivi ndiyo nashukuru Serikali inafanya kazi nzuri ya kuweka Kamati za Watoto waliopo katika Mazingira Magumu zaidi lakini nafikiri kwamba tunahitaji kwenda zaidi ya hapo kuwa na Kamati za Watoto walioko Vijiji zitakazoangalia kama haki za watoto vijijini zinalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie suala la Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilivyopo huko vijijini ikiwemo Chuo cha Ulembwe na Njombe na Chuo cha Ilula na vingine mbalimbali ambavyo Waziri asubuhi wakati akijibu swali alituelezea. Ninafikiri hivi vyuo sasa vinatakiwa pia viwe na mpango maalum wa kuweza kuangalia mahitaji ya mafunzo ya wananchi, vifanye utafiti wa kujua mahitaji ya mafunzo ya wananchi kwa wakati wa sasa na kwa maana hiyo viweze kutoa mafunzo ya muda mfupi kulingana na mahali chuo kilipo na mahitaji ya mafunzo ya wananchi wa eneo lile. Sasa hivi tunazungumzia wananchi wanaunda *SACCOS* na Wabunge tumehamasisha *SACCOS* mbalimbali kuundwa lakini tatizo kubwa likanakuwa ni kupata mafunzo. Mimi ninashasuri kwamba vyuo hivi pia vitumike kutoa

mafunzo ya muda mfupi ambayo yanahitajika kwa wananchi kwa maeneo yanayohusika ikiwemo mafunzo na mbinu mbalimbali za usindikaji wa vyakula kwa akina mama na mafunzo mengine ambayo yataonekana ni muhimu kwa lile eneo linalohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *SACCOS, SACCOS* nyingi zimeundwa zikiwemo *SACCOS* za wanawake. Lakini kwa kuwa hizi *SACCOS* zina wanachama wengi mara nyingine inakuwa ni vigumu fedha zao zile kuzunguka na kuweza kumfikia kila mwanachama aliyeweka fedha zake inakuwa ni matatizo na inaleta malalamiko. Lakini tunashukuru fedha ambazo zimetolewa na Serikali yaani fedha za JK zimeweza kusaidia kuweza kupunguza kero hii lakini bado mahitaji ni makubwa.

Ninaomba fedha zinazotolewa za Mfuko wa Wanawake ziweze kwenda moja kwa moja kwenye *SACCOS* za Wanawake ili kuweza kuhakikisha kwamba fedha hizi zinafika na pia zile za vijana viende moja kwa moja kwenye *SACCOS* za vijana ili kuweza kuhakikisha kwamba vijana hawa wanapata mitaji ya kuweza kufanya kazi zao na SACCOS hizi pia zinaweza kutumika kutoa mafunzo mbalimbali. Naelewa kwamba vijana wengi wana ujuzi na taaluma ambazo nyingine ni vipaji walivyozaliwa navyo hebu tuinue hivi vipaji vilivyopo kwenye jamii, Maafisa Utamaduni watusaidie na hawa vijana pia waweze kupata mitaji kutokana na fedha hizi lakini kwa kutumia *SACCOS* zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la utamaduni. Napenda niupongeze Mfuko wa Utamaduni ambao umefanya kazi nzuri ya kuweza kutoa mitaji mbalimbali pamoja na mafunzo kwenye masuala ya utamaduni. Lakini naomba nizungimzie sasa kufufua utamaduni ambao ulikuwepo wa asili. Najua kila mahali kulikuwa na tabia nzuri yaani utamaduni mzuri ambao ungeweza kusaidia kwa kizazi cha leo. Kulikuwa na makabila mengine ambayo kila siku wazee wanatoa hadithi kwa watoto na hadithi hizi zilikuwa na mafundisho maalum. Sielewi masuala kama hayo yanaishia wapi, hiyo ni mifano michache tu. Ninapenda pia hili lifanyiwe utafiti na tunaelewa kwamba wazee bado wapo kwa hiyo tunaweza kufufua utamaduni ambao ulikuwa unatusaidia katika kuendeleza mila zetu nzuri ambazo mpaka leo nyingine bado zinahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge hoja hii mkono na ninapongeza sana Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa nyongeza kidogo kwenye Taarifa ya Kamati ambayo imewasilishwa hivi punde kwa umahiri mkubwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wetu Jenista J. Mhagama.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda nitoe salamu za pole sana kwa wapendwa na ndugu wote kwa msiba wa Mheshimiwa Marehemu Salome J. Mbatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikipongeze sana Chama cha Mapinduzi kwa kufanya uchaguzi wake na hasa niwaponge viongozi mbalimbali walioteuliwa na kuchaguliwa kushika nafasi za uongozi kwenye Chama chetu. Ni imani yangu kwamba viongozi wetu hawa watakiendesha Chama chetu vizuri na kwa uhakika na kukiletea ushindi mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, naomba nichangie kidogo kuhusu Taarifa ya Kamati. Kwanza, nikiri kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati hii kwa hiyo maeneo mengi sana ya Wizara hizi tatu nimekuwepo na tumeshirikiana na Kamati na tukaona upungufu mwingi uliowasilishwa na Kamati, ni vizuri Serikali ikazingatia kama ripoti yetu ilivyopendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo kadhaa ambayo ninapenda kuongezea hasa kuhusu Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Awali, ninapenda kuzungumzia suala la mikopo ya wajasiriamali maarufu kama mabilioni ya Jakaya. Katika uzoefu wa mwaka mmoja wa mfumo huu wa utoaji mikopo, kumejitokeza matatizo kadhaa ambayo kwa kiasi kikubwa yanakwaza baadhi ya Watanzania kufikiwa na mikopo hii na hivyo kujikwamua na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kumekuwepo na tatizo la riba isiyolingana. Ikumbukwe kwamba wakopaji wanaokopa moja kwa moja kupitia Benki ya *NMB* wanakopa kwa riba ya 10%. Pia wakopaji wengine wanaokopa kupitia kwenye *SACCOS* ambazo zinakopa kupitia *CRDB Bank*, zenyewe zinakopesha kwa riba ya 10% na hivyo zinalazimika kwenda kukopesha wanachama wake kwa riba ambayo inazidi 10% ambapo *recommendation* ni 12%. Kimahesabu, mtindo huu maana yake unakinzana na lengo zima la kuongeza ushirika kwa sababu kwa mtu yeyote mwelewa angependa sana kwenda kukopa moja kwa moja mwenyewe kwa sababu akikopa kupitia *SACCOS* inakuwa ni gharama. Sasa nafikiri kwa sababu wakopaji wanaopitia kwenye *SACCOS, SACCOS* yenyewe ni kikundi ambacho tayari wanadhaminiana kwa hiyo *risk of defaults* kwenye *SACCOS* ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, ninapenda kuiomba Serikali iwashawishi watu wa *CRDB* washushe riba kwenye *SACCOS* ili *SACCOS* ikope kwa riba ndogo zaidi tuseme 8% ili itakapokuja kukopesha kwa wanachama wake ikopeshe kwa asilimia ile 10% hata anayekopa moja kwa moja kwenye Benki ya *NMB* ndiyo anayochajiwa. Kwa sasa hivi, ina *discourage* watu kukopa kupitia kwenye ushirika na kwa sababu lengo letu ni kukuza ushirika basi ni vizuri na ninaamini inawezekana kwa sababu riba inakuwa kwenye benki kwa sababu ya *risk of defaults* na kama tayari kuna *guarantee* ya Serikali pia wale wakopaji wenyewe wanadhaminiana maana yake *risk* ni ndogo sana 8% hata 7% Benki inaweza ikakopesha ili mradi tu Serikali ichachamae na ninaamini kabisa kwamba na Mheshimiwa Naibu Waziri yupo hapa na ninavyomuamini anaweza akazungumza vizuri na hao watu wakafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika mfumo huu wa ukopeshaji kwa upande wa mikopo inayotolewa na Benki ya *CRDB* kwenye *SACCOS*, kwa uzoefu ambao nimeuona kwenye Benki ya *CRDB* Kahama wao wamekuwa wakikataa kukopesha *SACCOS* mpya. Hoja yao ni kwamba wanapenda hizi *SACCOS* zilizoanzishwa waanze kwanza wenyewe kukopeshana hela zao ili waone *financial discipline* waliyonayo na kwa maana hiyo wapate uhakika kama wakikopeshwa wataweza kukopesheka. Sasa kwa kufanya hivyo maana yake ni kwamba kwenye maeneo ambayo hakukuwepo na *SACCOS* kabla ya mtindo huu kuanza hawatapata fursa hii na hili limeathiri sana wananchi wangu wa Jimbo la Msalala ambao wengi wao wanatoka maeneo ya pembezoni ambapo vikundi vyao vya ushirika wameviunda katika kipindi cha mwaka mmoja au miwili ambacho sisi viongozi wa kisiasa tumekuwa tukiwahimiza kufanya hivyo. Maana yake ni kwamba kwa kufanya hivyo, wananchi wanaokaa vijijini wanakosa fursa hii. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri pia Serikali ikaikumbusha na kuibana Benki ya *CRDB* na ushahidi upo kwa Benki ya *CRDB* hii ninayoizungumzia. Nakumbuka si siku nyingi sana tulikwenda hata na viongozi wa *SACCOS* ya Segese ambayo ni *SACCOS* mpya ina kila sifa kasoro tu kwamba imeanza katika kipindi hiki, Benki ikakataa kutoa mkopo sasa sidhani kama ni dhamira ya Serikali kwamba *SACCOS* mpya zisipate mkopo na kwa maana hiyo ni kwamba zitapata zile ambazo zipo kwa muda wa miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza nyingine katika mfumo wa ukopeshaji kupitia kwenye huu mfuko wa wajasiriamali, pungufu ambalo binafsi nimeliona ni kukosekana kwa mafunzo. Mfuko wenyewe hauna *element* ya mafunzo. Ni kweli tunatoa fedha yaani mikopo lakini ukimkopesha mtu ambaye hana hata ile *basic business management skills*, hajui hata namna ya kukokotoa na kujua kama anapata faida ama hasara kwenye biashara yake yawezekana kabisa akatengeneza andiko zuri lakini baada ya muda mfupi atashindwa kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri ni vizuri Serikali pamoja na hizi benki kwa mara nyingine kuangalia utaratibu endelevu wa kutoa mafunzo kwa wajasiriamali ambao tunawa-*groom* ili waweze kuendesha biashara zao kitaaamu bila hivyo wataweza kukopa *round* ya kwanza lakini *round* ya pili na ya tatu watakopa wachache na watashindwa kuendelea kwa sababu *continuity ya business* haitakuwepo *simply* kwa sababu hawana taaluma ya biashara. Kwa hiyo, ni vizuri hilo likaangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ajira, ninapenda tu kuzungumzia japo kwa kifupi kuhusu ajira za wageni na hasa idadi ya wageni wanaoajiriwa na maslahi wanayoyapata hasa kwenye sekta ya madini. Kumekuwepo na manung'uniko mengi ya tofauti za mishahara kati ya watalaamu wa kizalendo

na waajiriwa wa kigeni ambao wanafanya kazi zinazofanana wakati mwingine wazalendo wanakuwa wanawazidi utaalamu wale wageni. Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Ajira ya mwaka 2004 inaelezea tu kwamba kutakuwepo na viwango vya chini vya mishahara ambavyo hivi juzi vimetangazwa lakini haijaainisha baada ya hapo inakuwaje na pia hakuna mwongozo unaoonyesha viwango vya mishahara na maslahi kwa wageni viweje. Suala hili lisipoangaliwa ni tatizo kwa sababu mishahara ni sehemu ya gharama ya uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mzungu mmoja au mwekezaji mmoja mjanja anaweza akaja na ndugu zake tuseme *family proprietorship* ya watu wanne akawaajiri na akawalipa mishahara minono na akaendelea kuripoti kwamba anatengeneza hasara. Ile hasara inatokana na *salaries* anazolipa kwa wafanyakazi kwa sababu *salary* ni *expense* ambayo inaondolewa kabla ya kupata faida inayotozwa kodi na kwa kuwa watu wale ni wageni hawatozwi kodi kwa mujibu wa Sheria yetu ya Mapato ya mwaka 2004 maana yake ni kwamba Serikali inakosa mapato na hata ile faida ambayo inategemea kuja kutozwa mwishoni inakuwa haipo. Kwa hiyo, kuna hasara kwa Taifa kwa upande wa mapato lakini pia inaleta mgongano yaani *social discomfort* kwa wafanyakazi wazalendo ambao wanafanya kazi za kufanana na wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri ni vizuri pamoja na kudhibiti idadi ya wageni lakini pia pawepo na utaratibu wa kuangalia maslahi yanayolipwa ili walau yalingane na ugumu wa kazi ambayo watu hawa wanafanya bila hivyo manung’uniko ya wananchi yatakuwepo. Kwa kukumbushia tu ni kwamba sasa hivi tumesikia katika kipindi cha wiki moja au mbili zilizopita kwamba wafanyakazi wa mgodi wa Bulyankhulu waligoma na moja ya malalamiko yao ni tofauti ya mishahara ya kwao na ya wageni. Kwa hiyo, manung’uniko ya namna hii yataendelea kutusumbua endapo Serikali haitachukua hatua ya kurekebisha matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigusie kidogo kuhusu Sera ya Hifadhi ya Jamii. Sera ya Hifadhi ya Jamii haijawa tayari kwa hiyo kumekuwepo na ugumu wa uendeshaji wa mifuko hii ambayo ina utaratibu tofauti na wanachama inawaandikisha kutoka kwenye sekta mbalimbali za uchumi. Bila sera hii kukamilishwa mapema, matatizo yataendelea kuwepo. Kwa sasa hivi matatizo ambayo yanakuwepo kwenye Sekta ya Hifadhi ya Jamii ni pamoja na uhamishwaji wa mafao pale ambapo Mwajiriwa anahama kutoka mfuko mmoja kwenda mwingine. Lakini pia kwa sababu mifuko hii inashindana inafika mahali inakuwa ni vigumu hata kufuatilia Waajiri sugu ambao hawaleti michango kwa sababu wanajua kwamba endapo wakiwa–*harass* watahama kutoka mfuko huu kwenda mwingine. Kwa hiyo, kwa sababu unambembeleza maana yake ni kwamba hata *compliance* inapungua, hili ni tatizo. Ningeomba Serikali iliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba nimalizie kwa haraka sana kuomba tu kwamba *OSHA* iimarishwe kama ambavyo wachangiaji wengine wamesema na kwenye *report* yetu tumesema kwamba Idara hii inayosimamia usalama na afya mahali pa kazi, ni muhimu sana. Maeneo yaliyo mengi, Idara hii haifiki kwa kuwa hii *agency* haifiki maana yake ni kwamba usalama wa wafanyakazi katika maeneo mengi uko mashakani. Kwenye maeneo ya migodi hasa migodi ambayo inafanya *exploration underground.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mgodi wa Bulyankhulu kumekuwepo na malalamiko sana kwamba kule chini shimoni kilometa 6 chini hali ya hewa na mazingira ya kule ni magumu sana. Sasa chombo hiki kikiimarishwa kitaweza kukagua maeneo yote ya kazi na kuweza kugundua matatizo ambayo yanakuwepo na hivyo kuweza kusaidia wafanyakazi ili waweze kufanya kazi kwa muda mrefu. Yawezekana madhara ambayo wanapata wafanyakazi yasijitokeze mara moja, ni matatizo ambayo yanajitokeza baada ya miaka saba au nane kwa maana hiyo ni vigumu ku–*link* kwamba tatizo alilonalo mtu fulani au ugonjwa alio nao ulitokana na kipindi alichokuwa kwenye ajira ya kule mgodini. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri sana hii Idara ikaimarishwa ili iweze kufanya kazi nchi nzima, iweze kukagua maeneo yote ya kazi na hivyo wafanyakazi wote wafanye kazi katika maeneo yaliyo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa *NEC* lakini pia

kwa kuwasilisha taarifa yetu kwa umahiri mkubwa na pia kwa kuendesha vikao vyetu vya Bunge anapopata nafasi kwa umahiri uleule.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naiunga mkono sana taarifa yetu na ninaomba kushukuru sana, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa namwita Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah atafuatiwa na Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu.

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Kamati hii muhimu yaani Kamati ya Maendeleo ya Jamii na hasa kama uboreshaji wa shughuli za kiutendaji kwa siku zinazokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina sababu ya kurudia kwa sababu juzi nilisimama na nikawa nimetoa rambirambi na pia nikatoa salamu za pongezi za Chama kwa walioshinda Ujumbe wa *NEC* pamoja na Mwenyekiti wetu wa Chama Taifa. Kwa hiyo, ninaomba leo hii niendelee moja kwa moja tu ili nizungumzie masuala muhimu yanayohusu Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakuwa katika maeneo matatu na maeneo haya ni katika hizi Wizara zenyewe ambazo Kamati hii inajishughulisha nazo. Nikianza na mchango wangu wa kwanza, nianzie na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Kamati imeliona hilo, Wizara hii kama ilivyotajwa ni Wizara nyeti sana na inashughulika na masuala muhimu na makubwa na mazito. Kwa hali ya sasa kutokana na nchi yetu inavyokabiliwa na tatizo la ugonjwa huu wa UKIMWI, maana tunapokuwa na tatizo la ugonjwa wa UKIMWI, tunakuwa na matatizo ya kuwa na yatima na watoto wa mitaani na kadhalika.

Sasa ninapoweza kuzungumzia kuhusiana na Wizara hii hasa uhusiano kupitia Kamati, ni kweli kabisa naungana na Kamati kwamba pesa ambazo tumekuwa tukiidhinisha katika Bunge hili Tukufu ukweli ni pesa ninazoziona hazitoshelezi kwa majukumu mazima kabisa ya kuweza kuifanya Wizara hii ikafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, katika kuboresha zaidi, niombe na niseme kwamba Kamati iendelee kutoa kipaumbele na ijaribu kushauri ili kwamba Wizara iandae mikakati ambayo itaieleza na itaishawishi Serikail ili kwamba bajeti ya Wizara hii iweze kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiacha hilo, nizungumzie kuhusiana na suala la utendaji wa Wizara yenyewe na hasa nihusishe na Kamati nini inachopaswa kushawishi sasa au kushauri kwamba Wizara iweze kuzidisha utendaji wa kazi zake. Maafisa Maendeleo ya Jamii wanahitajika sana kule Wilayani na wanahitajika si kwa ngazi ya Wilaya tu bali mpaka kwenye ngazi ya vijiji. Sasa tusiende huko vijijini lakini tuishie kwenye ngazi ya Kata, ni dhahiri tukiangalia Maafisa Maendeleo ya Jamii hatunao wa kutosha katika Kata zetu.

Kwa hiyo, ninaomba Kamati pamoja na mambo mengine yote kwamba Wizara pindi watakapokuja hapa mbele yetu, wakaja kwenye kipindi labda cha bajeti, wawe na mikakati ya kuhakikisha kwamba tayari sasa tutakuwa na Maafisa Maendeleo wa Jamii kwa kila Kata kwa Kata za nchi yetu. Hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii ndiyo ambao wanaweza wakafanya kazi za shughuli za maendeleo ya jamii kwa ngazi zote kuanzia Vijiji, Kata na wakasaidiana na Wilaya na wakaweza kuboresha shughuli za maendeleo kwa nchi nzima kwa sababu ni kweli sisi nchi yetu tupo katika mkakati wa kutokomeza umaskini uliokithiri. Sasa ni lazima tuwatumie sana hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi na kwa ajili ya kuelimisha juu ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo, naiomba Kamati pamoja na kwamba tunahitaji hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii lakini tumezungumzia na tumeambiwa kwamba tuna Vyuo vya Maendeleo ya Jamii hapa nchini vipatavyo karibu 58. Lakini hivi Vyuo vya Maendeleo ya Jamii bado haijulikani namna watu wanavyoweza kujiunga, utaratibu bado unaonekana haupo wazi. Tuna vijana wengi waliomaliza Kidato cha Nne na Sita lakini pana ugumu sana wa namna ya kuweza kujiunga katika hivi Vyuo vya Maendeleo ya Jamii.

Kwa hiyo, hili suala naona liwe la Kamati na isiwe ni suala la Mbunge mmoja mmoja kumfuata Waziri na kumwomba kwamba nina vijana kadhaa nataka wajiunge kwenye Chuo cha Maendeleo ya Jamii. Kwa hiyo, naiomba Kamati iweze kushauriana na Wizara ili suala hili liwekwe wazi na liwekwe wazi kwenye Wilaya zetu zote na ili wale wanaohitaji basi waweze kujiunga na vyuo hivi bila kuwa na vikwazo na bila kuwa na vipingamizi vyovyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie kuhusiana na suala vitendea kazi kwa hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii wachache ambao tunao, kwa kweli wanapata taabu sana katika kufanya kazi zao. Anaweza akawepo mmoja katika Kata akawa anahudumia zaidi ya Kata tatu zenye vijiji labda vipatavyo 18 au 20. Sasa unamkuta huyu Afisa Maendeleo ya Jamii anapata taabu sana kuweza kuzunguka na kufikia katika vijiji vyote. Wakati wa bajeti iliyopita Waziri alitueleza akasema kwamba basi watahakikisha kwamba kutakuwa na usafiri kama pikipiki. Kwa hiyo, Kamati isisitize kwamba vitendea kazi vipatikane hasa usafiri kama pikipiki ziweze kutolewa kwa hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii na waweze kufanya hiyo kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nizungumzie juu ya hizi *NGOs* ambazo zipo na ambazo zimesajiliwa kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kweli nakubali kabisa *NGOs* ni kitu mbadala ambacho kinafanya kazi kwa kusaidiana na Serikali lakini naomba Kamati ifanye juhudi za makusudi na ipewe orodha ya hizi *NGOs* zote ambazo zimesajiliwa na zinazofanya kazi na izitembelee kama inavyotembelea vitu vingine kama vyuo na ione zinafanya kazi kweli na hizo kazi ndiyo ilizofanya ikasajiliwa? Kwa sababu zipo *NGOs* nyingine za mfukoni na *NGO* nyingine zinafanya kazi kwa matakwa ya mtu mmoja. Lakini na hizo *NGOs* zina maadili yake ya utendaji wa kazi, Kamati itembelee na iishauri Wizara, ikishatembelea na ikaona utendaji wake wa kazi itakuwa na fursa nzuri ya kuishauri Wizara nini *NGOs* hizi zinapaswa zifanye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, nizungumzie hiki chombo kinachoitwa Baraza la Michezo la Taifa. Nashukuru kwamba Mwenyekiti wa Kamati hii ni Mjumbe wa Baraza hilo tena nafikiri ni Makamu Mwenyekiti. Hebu naomba kuuliza utendaji wa hii BMT unaishia wapi? BMT ndiyo iko pale juu tu hewani na huku Mkoani haipo na Wilayani haipo? Sasa tunaomba tuelezwe kama ipo ni ya akina nani, tuelezwe Wajumbe wake katika ngazi ya Wilaya, Mkoa ili tuwaelewe kwa sababu masuala mengi yanayohusiana na michezo, Baraza kama lipo linafanya kazi kwa ngazi ya Wilaya na Mkoa naamini mambo yote yatakwenda vizuri. Kwa hiyo, hili naomba sana kwa sababu naamini Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii pia ni Mjumbe wa Baraza hilo Kitaifa kwa hiyo anaweza akatusaidia akatueleza tatizo liko wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala la fedha hizi za uwezeshaji yaani Mfuko wa JK. Juzi tulipokuwa na Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rais alizungumza kuhusiana na *creation of employment*, akasema kwamba tayari karibu ajira 350,000 toka tulipoanza zimeshapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Kamati iende kukutana na Wizara ielezwe bayana hizi ajira ni za aina gani? Kwa sababu tulipoelezwa hizi ajira tukawa tunazisema tu kama alivyozungumza Mheshimiwa Rais, laki tatu na kitu, sasa tuchukue nafasi ili tuwaeleze wananchi ajira zilizopatikana ni za namna hii na hii ili kuweza kujua kwamba hizo ajira kweli ni zile ambazo zilikuwa zimeahidiwa na Mheshimiwa Rais kwamba ajira milioni moja zitapatikana kwa kipindi cha miaka mitano cha Serikali ya Awamu ya Nne. Naiomba sana Kamati, ilitilie mkazo suala hili ili kuwaambia Watanzania kwamba tumefikia hatua gani na ni ajira za aina gani ambazo zimekuwa zikitamkwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo tu, naomba nikushukuru sana na niishukuru Kamati ya Maendeleo ya Jamii na nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati, kwa ujasiri wake na uwezo wake mkubwa wa kuweza kuisimamia Kamati pamoja na mambo mengine ambayo amekuwa akiyafanya na ndiyo maana naamini kwamba amezidi kuongezewa imani na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wakamchagua akawa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama chetu cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, nafikiri hata Mheshimiwa Magdalena Sakaya anaweza kufikiwa. Kwa wale wanaoandika, muda upo mnaweza kuomba kuzungumza sio lazima muandike.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii. Kwanza kabisa, naanza kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Yusuf Makamba na viongozi wote waliochaguliwa katika mchakato huo wa kutafuta viongozi ndani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu na Kamati Kuu, ninachosema ni kwamba unastahili na unaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninapenda kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Kagera ambao ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi kwa kunichagua mimi kuwa Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa. Naahidi kwamba nitatoa ushirikiano ili kusudi tuweze kuleta maendeleo ya Chama chetu na ya nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama kwanza kwa kuchaguliwa kuingia kwenye *NEC* kutoka kwenye Mkoa wake, hiyo inaonyesha kwamba ni kwa jinsi gani wananchi wa Mkoa wake wanavyomuamini na wanavyothamini mchango wake katika Chama na katika kuleta maendeleo ya wananchi. Nipende vilevile kumshukuru kwa taarifa nzuri aliyoiwasilisha vizuri ambayo imeandaliwa kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nawapongeza sana *NSSF* kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya. *NSSF* ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii unaopanuka kwa maana ya kwamba mtaji unaendelea kuongezeka na wanachama wanaendelea kuongezeka lakini siyo hilo tu *NSSF* mafao yake yanaongezeka mwaka hadi mwaka. Sasa hivi mafao yameshafikia zaidi ya saba, kwa hiyo ina maana kwamba wale wachangiaji wanazidi kunufaika mpaka imefikia kiasi ambacho watu wanatoka kwenye nchi nyingine kuja kuangalia sasa *NSSF* wamewezaje kutoa mafao makubwa na mengi kiasi hicho kwa wanachama wake. Vilevile tumeona kwamba *NSSF* wamefanya kazi nzuri ya uwekezaji kwenye miradi mikubwa mikubwa. Sasa ushauri wangu kwa *NSSF* ni kwamba kadri wanavyozidi kuwekeza na kwa kadri wanavyozidi kupata faida, hiyo faida waitumie kuendelea kuboresha yale mafao wanayopata wale wanachama wanaochangia huo Mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* imejenga nyumba za kuishi za bei nafuu kama zile zilizopo Kinyerezi. Mradi huo ni mzuri sana, wanajenga nyumba za kudumu, wanamuuzia yule ambaye anataka kuishi mle kwa bei nafuu na kwa masharti nafuu, zile fedha hazilipi kwa mkupuo mmoja, anaendelea kulipa pole pole kwa muda wa miaka kama saba au miaka kumi. Kwa hiyo, huo mradi kwa Tanzania ndiyo tunaouhitaji kwa sababu watu wetu wengi hawana uwezo wa kupata fedha nyingi na kujenga nyumba. Kwa hiyo, *NSSF* wanapojenga nyumba, wakampa mtu akaendelea kulipa pole pole ina maana kwamba wanaweza kusaidia Watanzania wengi ambao ni maskini wapate nyumba nzuri za kuishi. Naiomba basi *NSSF* wasije wakaishia Mijini tu kama Dar es Salaam, hebu waende kule Chato, waende Ngara, Biharamulo, Karagwe, Muleba, Misenyi, Bukoba ambazo ni Wilaya zilizopo katika Mkoa wa Kagera. Miradi mingi mizuri ikianza inaanzia kwenye Miji mikubwa mikubwa kama Dar es Salaam lakini nina uhakika walengwa na wahitaji wengi wapo Mikoani kama Mkoa wa Kagera, waende kule wajenge hizo nyumba nzuri waweze kuwakopesha au kuwapa watu wale kwa masharti nafuu ili nao Watanzania wa Mkoa huo waendelea kulipa polepole katika miaka kumi na kwa kufanya hivyo basi tutaweza kuwasaidia Watanzania wengi na kuleta maisha bora kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Wengi wamevizungumzia, tumevitembelea ni kweli vingi vinahitaji ukarabati wa kina. Kwa hiyo, napendekeza basi Serikali itakapokuwa inatoa fedha kwa Wizara hiyo watoa fedha za kutosha ili kusudi vyuo vingi viweze kukarabatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kilichoniuma sana ni upungufu mkubwa wa wafanyakazi katika vyuo hivyo. Tulikuta Walimu hakuna na kama wapo hawatoshi. Tutulikuta kuna vyuo ambavyo havina Wahasibu kwa zaidi ya miaka saba. Sasa katika chuo ambacho hakina Mhasibu zaidi ya miaka saba mahesabu yanafanywa na nani? Kuna uwezekano wanachagua Mwalimu mmoja ambaye hajasomea taaluma ya Uhasibu ndiyo anafanya hayo mahesabu. Siwezi kushangaa kwa nini vyuo hivi vinaendelea kupata Hati Chafu za Ukaguzi kwa sababu hawana wataalam na ubadhilifu unaweza kutokea. Sasa sijui utakapotokea ubadhilifu nani atawajibishwa? Huwezi kumwajibisha mtu ambaye hajasomea hiyo taaluma na wewe ulikuwa umempa kazi ambayo inamzidi uwezo. Kwa hiyo, napendekeza kwa Serikali kwamba wahakikishe wanaajiri wafanyakazi wa kutosha hasa Wahasibu na Walimu ili kusudi vyuo hivi viweze kutoa elimu bora na sio bora elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumegundua vilevile kwamba wanafunzi wengi wanaosoma kwenye vyuo hivi wanasoma fani mbalimbali ikiwemo ujenzi, uhunzi, kilimo, ufundi wa magari na kadhalika lakini wakimaliza hawapati ajira na vilevile wanashindwa kujiajiri kwa sababu hawana mitaji ya kutosha. Lakini nchi nyingi zilizoendelea kama Singapore na China wameendelea kwa sababu wameweza kuwekeza katika sekta binafsi na wakawawezesha watu wao kwa kuwapatia mitaji na wakaanzisha viwanda vidogo vidogo, wakatumia elimu wanayoipata kutoka kwenye vyuo hivi, wakaweza kujiendeleza. Sisi tunavyo vyuo, tunatoa elimu, vijana wapo, hatuwawezeshi badala yake tunaendelea kuagiza bidhaa kutoka nje, ndio maana watu wanalalamika kwamba, kuna bidhaa nyingi zimezagaa Kariakoo hazina ubora wa kutosha, lakini bidhaa hizo hizo zingeweza kutengenezwa ndani ya Tanzania kama hawa vijana wangewezeshwa kwa kupewa mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napendekeza kwamba wanafunzi au wahitimu wanaotoka kwenye vyuo hivi, Serikali iweke mipango ya makusudi kuhakikisha kwamba wanapewa aidha mitaji au vifaa vya fani yake. Kama amesomea *carpenter*, akihitimu apewe vifaa hivyo, kama amesomea ufundi bomba, basi apewe vifaa vinavyoendana na ufundi bomba au kama amesomea kilimo basi apewe vifaa vinavyoendana na mambo ya kilimo ili kusudi waweze kutumia elimu yao kuanzisha viwanda vidogo vidogo kuzalisha mali na kujipatia kipato. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumepunguza umaskini uliokithiri lakini tukiwafundisha tu na wakatoka kwenye hivyo vyuo bila Serikali kuwasaidia kwa njia yoyote ile sidhani kama itakuwa inatusaidia sisi Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni Wizara moja ambayo ina majukumu makubwa sana na hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali imeahidi maisha bora kwa kila Mtanzania. Kwa kuitumia Wizara hii vizuri, tutaleta maendeleo ya jamii nikiwa na maana tutakuwa tumeleta maendeleo ya kila Mtanzania. Wizara hii ina majukumu ya kuhakikisha kwamba kila mtu ana makazi bora, kupunguza umaskini uliokithiri na Wizara hii inapaswa kuhakikisha kwamba yanatolewa mafunzo ya ujasiriamali ili watu waweze kufanya miradi midogo midogo ya kuwaletea kipato. Vilevile Wizara hii ina majukumu ya kushughulikia watoto na jinsia na kwa upande wa jinsia sasa hivi wana jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba wanatengeneza mikakati ya kuhakikisha kwamba uwakilishi kati ya wanawake na wanaume unafikia asilimia hamsini kwa hamsini. Haya ni majukumu makubwa sana kwa hiyo wanahitaji fedha za kutosha. Lakini kama mnavyoona mwaka hadi mwaka bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto huwa ni ndogo sana. Wizara ilishaandaa kitita cha *appropriate technology*, wanafundisha watu namna ya kutengeneza mikokoteni, pampu za umwagiliaji, majembe ya kukokotwa na wanyama, majiko sanifu, majiko ya *solar*, lakini ikaishia hapo, Serikali haijawapatia hela za kutosha kuweza kuendeleza hiki kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia kuanzisha viwanda vidogo vidogo kama Serikali ingeweza kuipa Wizara hii fedha nyingi wakaendeleza hiki kitu, ina maana vijana wetu wangeweza kupata mikopo na mitaji na kuweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo, wakatengeneza nyenzo hizo, kwa hiyo, badala ya kwenda kuagiza hizi pampu kutoka nje, *solar cookers* kutoka nje, vijana wetu ndio wangekuwa wanafanya hivi vitu. Kwa hiyo, napendekeza kwamba Serikali ione hii Wizara kama Wizara nyingine, iwape fedha za kutosha kusudi waweze kutimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi ni maskini ndio maana mwaka jana kila mtu alikuwa anahamasisha watu waingie kwenye *SACCOS*. Lakini la kwanza, tunapozungumzia kwamba vijana wa Tanzania hawana ajira na tunataja eti vijana wakope kwenye *SACCOS* na sasa hivi tunazungumza

kwamba zile fedha zinazopita kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ziende kwenye *SACCOS*, je, *SACCOS* za vijana zipo? Mimi kwa utafiti wangu mdogo nilioufanya, nimeona akina mama wengi ndio wamechangamkia *SACCOS* lakini vijana wengi wanakaa kwenye vijiwe hawajapata elimu ya ujasiriamali, hawajahamasika vya kutosha kuingia kwenye *SACCOS*. Kwa hiyo, naomba tafadhali kila mtu kwenye nafasi yake, tuendelee kuhamasisha vijana wajiunge na *SACCOS* ili waweze kupata elimu ya ujasiriamali na mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali kwa kuanzisha Mfuko wa Uwezeshaji. Kweli tuliona kwamba watu wengi waliomba mikopo, hii inamaanisha kwamba watu wengi wana miradi ya kufanya, lakini waliopata ni wachache, fedha zikaisha na wakulima wengi hawakupata, watu wengi waliopata ni watu wa mjini lakini pia ni wale wajuaji, watu wengi wa vijijini hawakupata. Serikali tangu mwezi wa saba bajeti ilipoanza inatwambia kwamba sasa wanataka kuanzisha mkondo wa pili wa fedha kupitia *SCCULT* pamoja na benki za wakulima. Tunauliza tangu mwezi wa saba mpaka leo kulikoni? *SCCULT* hata kabla ya kupata uwezeshaji huu wa Serikali walikuwa tayari wanazipa hela *SACCOS* zilizo vijijini hata ukienda leo Ngara, Buselesele na Missenye utawakuta, sasa kwa nini mlolongo unakuwa mkubwa hivi? Tunaomba tuelezwe kuna tatizo gani tangu mwezi wa saba mpaka sasa hivi mwezi wa kumi na moja kwa nini *channel* ya pili haijaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru *NMB* na *CRDB*, wamefanya kazi nzuri sana ya kukopesha watu lakini nina uhakika hawa watu waliokopa wanarejesha fedha. Sasa hizo fedha zikirejeshwa zinaingia benki? Kama zinaingia benki kwa nini wasiendelee kukopesha wajasiriamali wengine? Kwa hiyo, napendekeza kwa Serikali kwamba kwa kuwa wananchi wengi wa Tanzania ni maskini, wengi wameingia kwenye *SACCOS*, wengi wamejifunza ujasiriamali, kinachohitajika ni mitaji, basi Serikali iendeleze ule mfumo wa kwanza wa *NMB* na *CRDB* na wao waendelee kukopesha na waanzishe mara moja huo uwezeshaji wa *SCCULT* na benki za wakulima ili ziendelee kuwakopesha wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba niwapongeze wana-Kamati wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa kazi nzuri wanayoifanya na nimpongeze Mwenyekiti pamoja na Makamu Mwenyekiti wanavyoendesha Kamati hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kidogo kwenye taarifa hii ya Kamati ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia, naomba nitoe pongezi kwako kwa kushinda nafasi ya kuwa mjumbe wa *NEC* na kuingia kwenye Kamati ya Uongozi wa Chama chenu. Pia nimpongeze Mwenyekiti aliyewasilisha taarifa hii kwa kuwasilisha vizuri taarifa yake na pia kupata nafasi ya kuingia kwenye ujumbe wa *NEC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kutoa salaam za pole kwa kiongozi wetu wa Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid, ambaye yuko nchini India kwa ajili ya matibabu. Namwombea Mwenyezi Mungu amrejeshee tena afya njema aweze kupona na kuweza kurudi kwenye majukumu yake ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye mchango wangu kwa kuchangia taarifa iliyoko mbele yetu. Naomba nianze kwanza na viwango vya mishahara kwa wafanyakazi wa sekta binafsi. Wote tunatambua mchango wa sekta binafsi kwenye maendeleo ya Taifa hili na kwa ajili ya kuwaendeleza Watanzania na jinsi gani inavyoshiriki kikamilifu kusaidia wananchi wengi kuweza kupata ajira. Lakini kwa uzoefu tuliokuwa nao, mashirika mengi na sekta nyingi binafsi wamekuwa wanawatumikisha sana wananchi kulingana na kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni, Serikali imetangaza viwango vipya vya mshahara vikiwemo kima cha chini kwa wafanyakazi wa sekta binafsi. Lakini kwa uzoefu tuliokuwa nao sekta binafsi ni wachache watakaolipa kufuatana na utaratibu uliowekwa na Serikali. Sasa ningependa kutoa rai kwa Serikali kwamba pamoja na kutangaza lakini wafuatilie kwa ukamilifu sekta baada ya sekta, shirika baada ya shirika ili kuweza kuona kweli viwango vilivyowekwa na Serikali ndivyo vinavyotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kasumba au *tendance* ya mashirika au sekta binafsi pale wananchi wanapodai haki zao kwamba tunaombwa tulipwe kulingana na mishahara iliyowekwa na Serikali, wanawafukuza kazi, kuwasimamisha au hata kuwapa vitisho kwamba kama hutakubaliana na mshahara tunaokupa basi tunakuachisha kazi. Kwa hiyo, pale inawakatisha tamaa lakini kutokana na kwamba mfanyakazi yule hana pa kwenda inabidi afanye kazi kulingana na masharti ya pale alipo hata kama halipwi haki yake. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali pamoja na kuweka viwango maalum lakini ifuatilie kuhakikisha kweli viwango hivi wanalipwa wafanyakazi wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo naomba kulizungumzia ni la uanzishwaji wa Vyama vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS).* Tangu mwaka jana wananchi katika maeneo mengi walikuwa wamehamasishwa sana na wengi kwa kweli wamehamasika na wamekubali kuanzisha hizi *SACCOS* lakini vyama vingi vimekuwa vinakwamishwa na Maafisa wa Wilaya. Mara nyingi wananchi wamejitokeza, wameunda kikundi chao, wametoa michango yao vizuri lakini wakianza kufuatilia wapate mafunzo, halafu wapate usajili kwa kweli inachukua muda mrefu sana, kunakuwa na kuzungushwa kusikokuwa na maana. Matokeo yake wananchi wanaona kwamba ni kunyanyasika na kuteseka na hela yao ipo pale haifanyi kazi, mmoja mmoja anaamua kuichomoa baadaye ule Mfuko unakuwa haupo tena. Kwa hiyo, naomba sana hii *SCCULT* iwezeshwe kikamilifu ili iweze kutoa wataalam wa kutosha kwenda hadi Wilayani na kwenye Kata wakatoe elimu kwa wananchi jinsi ya kuanzisha hizi *SACCOS*. Kutumia tu maafisa Ushirika wa Wilaya kwa sababu yuko mmoja inakuwa ni vigumu. Kwa hiyo, wengi wameshindwa kuanzisha *SACCOS* hizi kwa sababu ya kukatishwa tamaa na vikwazo vinavyowekwa na Maafisa Ushirika. Naomba sana *SCCULT* iwezeshwe ili iweze kufanya kazi yake kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuwepo kwa taasisi zisizo za Kiserikali *(NGOs).* Tunatambua mchango mkubwa wa *NGOs* kwa kuleta maendeleo katika jamii na kwa kuelimisha jamii. Tunaiomba Serikali iweze kuzitambua hizi *NGOs* kila mahali zilipo na zinatoa huduma gani. Kama ilivyoomba Kamati na mimi naona ni muhimu kwa kweli na naongezea msisitizo, Serikali itambue kila *NGO* iko wapi. Mfano mdogo, huu Mtandao wa Akina Mama Tanzania (*TGNP*), unafanya kazi kubwa sana. Hakuna asiyetambua mchango wa taasisi hii hapa Tanzania hata mtu uliyefumba macho utaona kwa kweli wamefanya kazi kubwa ya kuelimisha vijana, akina maama na hawako *bias*, si kwa akinamama tu, hapana, wapo kila mahali. Kwa hiyo, mtandao kama huu au taasisi kama hii Serikali ingeitambua na pale ambapo wanakwama basi Serikali iweke nguvu ili iwawezeshe kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa ajili ya kusaidia wananchi wa Tanzania na kwa ajili ya kuleta maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la vituo vya watoto yatima. Hili suala limechangiwa na kila aliyesimama, nami pia nilikuwa nimeliweka kwenye orodha yangu ya kuchangia, naomba niligusie kwa ufupi. Kuna jibu lilitolewa hapa Bungeni jana au juzi sikumbuki vizuri lakini mimi lilinisikitisha sana. Mheshimiwa aliyejibu swali alisema kwamba Tanzania mpaka sasa hivi hatujui idadi ya watoto yatima waliokuwepo lakini pia akasema kwamba hatujui idadi ya wale ambao wanaanzisha vituo vya watoto yatima. Kwa mfano, mtu anajitolea kwa ajili ya kuanzisha kituo cha watoto yatima lazima ahakikishe kwamba anakuwa na uwezo wa kutosha wa kuwahudumia. Lilinigusa sana kwa sababu, kwa utaratibu wa utawala tuliokuwa nao Tanzania kuanzia *Central Government* hadi kwenda kwenye *Local Government* labda kuanzia ngazi ya Kijiji, sasa inakuwaje Serikali iache kujua idadi ya watoto yatima waliokuwepo wakati tuna ngazi mbalimbali za uongozi? Tunaanza na utawala wa Balozi wa nyumba kumi kumi, tunakuja Kitongoji, Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, inakuwaje taarifa kama hizi ziache kuwepo wakati Balozi wa nyumba kumi kumi labda kama kuna watoto ambao wamepoteza wazazi ni lazima ajue. Kwa *trend* hiyo, lazima inakwenda kidogo kidogo kupanda juu mpaka inafika Wilayani. Inakuwaje mpaka leo Taifa liache kufahamu kuna watoto yatima wangapi na watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu wangapi, watawezaje kuwahudumia kama wanashindwa kuifahamu idadi yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naomba Serikali sasa ichukue jukumu kuhakikisha kwamba inakwenda kona zote, *system* yetu ya uongozi inaiwezesha Serikali kupata *data* zote kutoka kwenye kona yoyote ya Taifa hili ili iweze kufahamu kwa uhakika kwamba tuna watoto wangapi ambao wanaishi katika mazingira magumu. Kwa kuwafahamu tu idadi yao inakuwa rahisi hata kuweza kuwajengea taratibu tuwasaidie vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hivyo pia tunaomba vile vituo vya watoto yatima pamoja na kwamba vinaendeshwa na dini na watu wengine binafsi ambao wamejitolea na vingine vinaendeshwa na taasisi mbalimbali lakini ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma nzuri bila kujali kwamba ni watoto au wakubwa. Kwa hiyo, ifuatilie kwenye vile vituo kuhakikisha kwamba watoto kwenye vituo hivi wanapata huduma bora inayotakiwa na kama hawapati huduma inayostahili kwa sababu ya mapungufu ya vile vituo je, wao kama Serikali wanachukua hatua gani? Sio kuwaacha tu watoto wanateseka. Pengine yule aliyeanzisha kituo alikuwa na nia nzuri ya kuwasaidia watoto, lakini inafika mahali nguvu yake inakuwa ndogo au kama sio nguvu kuwa ndogo pengine watoto wanaongezeka, labda alianza na watoto kumi, kidogo kidogo wanaongezeka kulingana na mahitaji yanavyokuwa na yeye anavyoona kwamba anahitaji kuwaweka pale matokeo yake anajikuta kwamba makadirio yake ni tofauti na matarajio, bajeti yake inakuwa ndogo. Je, Serikali inamsaidiaje mtu kama huyo au taasisi kama hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali ihakikishe kwamba vituo vyote ambavyo vinalelea watoto yatima vinatoa huduma inayostahili na kama alivyozungumza Mheshimiwa Mng'ong'o baada ya watoto hawa kutoka hapa kwenye hivi vituo wanakwenda wapi? Serikali ihakikishe kwamba inafuatilia watoto hawa, tusiwatoe kwenye vituo vile halafu tunawaachia tu mitaani, wawe watoto wa mitaani wakubwa, tumewatoa kwenye *stage* ile utoto tunawaachia wakati wameshakuwa wakubwa. Tuhakikishe kwamba wakitoka pale tuna-*monitor* maisha yao kidogo kidogo. Sawa wametoka lakini je, wamekwenda shule? Mpaka tuhakikishe angalau wameweza kujitegemea, ndio Serikali iweze kutoa mkono wake. Ni muhimu sana kwa Serikali kufanya hivyo, kwa kweli hawa watoto ni wengi ambao hawana huduma, wengine wapo vituoni lakini wanategemea misaada. Kwa hiyo, mpaka aje mtu atoe ufadhili ndio waendelee, lakini ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba wanapata huduma nzuri wanazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona saa yetu ya kuahirisha kikao mchana inakaribia lakini bado nina wasemaji wengine na ni hoja ambayo tutaizungumzia siku nzima ya leo. Kwa hiyo, kama kuna wengine wanaotaka kuchangia ambao hawajaomba wanaruhusiwa kuomba. Kwa sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.25 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA,** Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina machache nadhani kwa siku ya leo yanatosha. Yupo Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Ruth Msafiri. Halafu tutakuwa na Manaibu Mawaziri na Waziri, halafu Mtoa hoja. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Mgana Msindai!

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie kwa kifupi kwa sababu mambo mengi wenzangu wameshayazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii na Wajumbe wake wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na wanaendelea kuifanya. Kwa kweli taarifa yao imekuwa ya kina na ina mambo mengi ambayo mengine tunayapongeza na mengine tunataka waendelee zaidi na vilevile tunaipongeza Serikali pale ambapo imechukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na mambo mengi inashughulika na ajira mbaya kwa watoto, tatizo ambalo bado linatukabili, watoto wadogo wanaajiriwa katika kazi za nyumbani. Tunaishukuru Serikali imejitahidi kupunguza lakini bado watoto wanaajiriwa wengine chini ya miaka 15, wengine wanaajiriwa wakiwa na miaka 10 na mishahara wanayoipata ni midogo sana wanalipwa shilingi 10,000/= eti kwa sababu wanapata malazi na chakula, kwa kweli watoto wetu hawatendewi haki. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali iendelee kukemea jambo hili mpaka mwishowe liishe kabisa. Watoto wadogo licha ya kufanya kazi za nyumbani wengine kama mabinti mpaka

inafikia inakuwa ni nyumba ndogo za matajiri waliowaajiri kitu ambacho kwa kweli ni cha aibu na ni kuharibu maisha ya watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia watoto wa mitaani Wizara hii ndiyo inayowashughulikia. Sasa ukienda Dar es Salaam na katika Miji mingine hata hapa Dodoma kwa mfano, ukitaka kujionea mfano halisi ni siku za Jumamosi kama kesho Mnadani, watoto wadogo wanapita wanaokota mifupa, watu wanakula nyama wanatupa mifupa ile wao wanaokota. Kwa kweli haya ni mambo ambayo ni lazima tuyaangalie na kuyakemea kwa sababu hao watoto ni Taifa la kesho. Kwa hiyo, ni lazima tuanze kuwaandaa mapema na ni lazima tuwajengee misingi mizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kupitia kwa wafadhili kule Wilayani ninakotoka tulikuwa na tatizo la ajira ya watoto lakini tulipata fedha wamewaanzishia miradi na wao wenyewe wameona kwamba kufanya kazi zao wenyewe wakajitegemea ni faida kubwa. Tunaiomba Serikali iendelee kuwatafuta miradi kama hiyo. Kwa mfano, kama fedha hizo zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wetu, ni juu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kuhakikisha vijana wetu, watoto wetu ambao wameishafikia umri wa kujitegemea, wanapata fedha hizo kwa maendeleo yao. Kwa kweli inasikitisha sana sana mahali pengine tunaona fedha hizo wanakopeshwa watu ambao wana uwezo wao lakini vijana wanaohusika wanakuwa hawapewi hiyo mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la Wizara hii ni Wizara iliyovuma sana tulipopata uhuru na sasa hivi haina watumishi, watumishi ni wachache sana. Unakuta Wilaya ina mtumishi mmoja au wawili na hawawezi kwenda vijijini wakati maendeleo tunataka yaende kwa watu wetu vijijini. Unakuta watumishi hao ni wachache, hawana usafiri, hawana nyenzo za kufanyia kazi, kama ripoti ilivyoonyesha kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi hao, tunaiomba Serikali iangalie upya ili wawaajiri wataalam wa kufanya kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata fedha zinazotengwa kwa Wizara hii ni ndogo mno na hata Serikali inajua na hii ni Wizara muhimu sana. Ninaomba sana kwa sababu tunataka maisha bora kwa kila Mtanzania, Wizara hii iongezewe fedha ili maendeleo yaende vijijini na ili watu wetu wajikomboe, waondokane na umaskini. Kwa hali hii, tunavyokwenda kwa kweli, nina wasiwasi kama tutafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitendea kazi, asubuhi Mheshimiwa Waziri alikuwa anajibu swali juu ya usafiri wa Chuo cha Maendeleo Nkasi, akasema watafuta gari hata iliyopo Wizarani, waitengeneze wawapelekee kule. Gari ambalo lipo Wizarani limeshindikana ndiyo wapelekwe kule Wilayani! Naomba sana zifanywe juhudi za makusudi *at least* Wilaya zipewe vitendea kazi. Hapo ndiyo vipo Vyuo vya Maendeleo na vyuo ambavyo kule mwanzo vilikuwa vya maendeleo. Lakini sasa hivi ukifika katika vyuo vingi vipo kwenye hali mbaya sana. Watumishi walioko huko wengi walishakata tamaa, hawana vitendea kazi na wana madai chungu nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali iangalie upya suala hili. Narudia kuomba kama Serikali inaona kupitia Wizara hii haiwezi kuvisimamia vyuo hivyo bado narudia kusema ni kheri viende Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, lakini viendelee kufanya kazi ile ile. Maana kwa kweli Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wanapata fedha za kutosha na Wizara hii ndiyo imechukua vyuo vya *VETA*. Kwa hiyo, hata Vyuo vya Maendeleo baadhi yake vikienda kule vitafanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii tunaweza kusema ni Wizara mtambuka, inashughulika na mambo ya afya, inashughulika na mambo ya maendeleo, kwa hiyo kwa kweli bila kuwa na vitendea kazi haitafanya kazi zake vizuri. Tunashukuru upande mmoja Serikali inajitahidi sana na Mashirika yaliyopo kwenye Wizara hii yanajitahidi sana lakini hata hivyo, ni jukumu la Serikali kuipa kipaumbele Wizara hii ili iweze kufanya mambo yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na kumbi za maendeleo ambapo wananchi wetu walikuwa wanakwenda kufanya utamaduni wao, kufanya maonyesho yao, lakini kumbi nyingi hizo zimesahaulika na zipo kwenye hali mbaya. Hata hivyo, naiomba Serikali iendelee kuisaidia Wizara hii irudishe heshima yake isiwe Wizara ombaomba, isiwe Wizara ambayo inajiendesha kwa shida. Hii ni Wizara kamili ya Serikali

inayohudumia wananchi wetu hasa watoto wetu ambao tunataka tuwajenge wawe na uwezo toka wakiwa wadogo mpaka huko mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yameishasemwa na wenzangu, sitaki kuyarudia, naunga mkono hoja hii mia kwa mia, na ninakushukuru sana wewe, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nitoe pole kwa familia ya Joseph Mbatia, kwa kufiwa na mpendwa wao Marehemu Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia na hii imenipa uchungu sana kwa sababu Marehemu Salome Joseph Mbatia alikuwa Mwana Jumuiya mwenzangu toka kata ya Mbokomu. Kwa hiyo, Jumuiya ya Mbokomu tumepoteza kiongozi shupavu. Ninaomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, nitoe pongeza zangu za dhati kwa wenzetu wa Chama cha Mapinduzi kufuatia Mkutano Mkuu na kipekee kabisa nitoe pongezi zangu za dhati kwako Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupata Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa lakini pia kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, nitachangia katika maeneo makuu matatu. La kwanza, naomba nianzie hasa kwa suala nzima la ajira na hasa kwa watu binafsi. Ninashukuru sana jana nilimsikia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akieleza ni jinsi gani wawekezaji binafsi wanavyowapunja mishahara wafanyakazi hasa Watanzania. Tunaona kwamba wafanyakazi wanapokea mishahara ya kima cha chini cha shilingi 48,000/=, kwa kweli fedha hizi ni ndogo sana haziwezi kuwatosheleza katika mwezi nzima na hasa ikizingatiwa kwamba wengi wao wana familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ni vyema wawekezaji hao waelewe kwamba wafanyakazi hao ndiyo wanaowatajirisha wao na hivyo ni lazima wawapatie mishahara mizuri ili na wao waweze kufanya kazi zao kwa moyo na hivyo kuweza zaidi kuwafanya wao (waajiri) waendelee kutajirika lakini pia na wao wapate huduma ikiwemo mishahara mizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika suala hilo hilo la ajira ambalo ninaamini kabisa lipo chini ya Kamati hii ni suala nzima la vijana wetu wanaomaliza Vyuo. Unakuta vijana wengi hata wanaosoma fani kwa mfano ya kilimo wanashindwa kwenda kufanya kazi zao za kilimo kutokana na miundombinu mibovu. Unakuta watu wamesomea Shahada ya Kilimo lakini wapo maofisini badala ya kuwa mashambani. Hivyo, ni matumaini yangu kwamba Serikali ikiweza kuboresha miundombinu katika sekta ya kilimo, basi ajira nyingi zinaweza kupatikana na hivyo tatizo la ajira litapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna suala zima la ajira za wageni. Tumegundua kwamba ni kweli Mataifa mengi yanaajiri watu kutoka nchi mbalimbali, lakini kwenye ajira ambazo ni *professional*. Lakini kwa hapa Tanzania imekuwa ni tatizo kubwa kuona kwamba hata ajira ambazo wangeweza kufanya Watanzania kwa mfano, sasa hivi ukipita Kariakoo utakuta Wachina wanafanya biashara ya umachinga. Kwa hiyo, nadhani ni jukumu la Wizara husika pamoja na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kuhakikisha kwamba ajira zile zinazoweza kufanywa na Watanzania, basi zifanywe na Watanzania ili waweze kupata kipato cha kuwatosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala nzima la *NGOs.* Ni kweli *NGO*s ni muhimu sana sio tu kwa Tanzania lakini kwa nchi mbalimbali, kwamba zinafanya kazi nyingi, kwa sababu kwa kweli kuna sehemu ambazo Serikali inashindwa, lakini unakuta *NGOs* inafanya kazi hizo vizuri sana. Nimegundua kwamba *NGO*s nyingi tunaziita ni za mfukoni au ni za watu binafsi, zimesajiliwa lakini unakuta hazifanyi kazi zile ambazo zimesajiliwa kufanya. Kwa hiyo, nafikiri ni jukumu la Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Msajili wa *NGOs* kuhakikisha kwamba zinafanya kazi zile ambazo zimeainishwa katika usajiliwa wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la michezo. Ni kweli michezo ni muhimu kama ambavyo Kamati imeainisha lakini bado mimi tatizo langu ni suala la viwanja vya michezo. Hapa niipongeza Serikali kwa Uwanja mpya wa Taifa lakini bado tunaamini kwamba vipaji vya watoto vinajengwa toka wakiwa shule za msingi. Lakini kutokana na upanuzi wa shule, mtakubaliana nami kwamba sehemu nyingi za shule yalipokuwa maeneo ya viwanja vya michezo sasa hivi kumejengwa shule nyingine. Kwa maana ya kwamba eneo moja lilikuwa ni la shule moja ya msingi lakini sasa hivi zimekuwa shule mbili. Kwa hiyo, eneo la shule ya pili, inakuwa ni kwenye eneo lile la uwanja wa michezo. Kwa hiyo, utakuta shule nyingi sasa hivi za msingi hazina viwanja vya michezo, hilo nalo ni tatizo. Kwa hiyo, ile dhana nzima ya kumjengea mtoto uwezo kuanzia shule ya msingi, inakuwa haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni mategemeo yangu pamoja na kwamba tunataka sana kupanua shule za msingi lakini basi liangaliwe pia na suala zima la michezo. Kwa sababu michezo pamoja na kwamba ni afya lakini pia ni ajira kwa baadaye. Kwa hiyo, tulikuwa tunategemea kwamba watoto wetu wataweza kujengewa uwezo wao toka shule za msingi ili wanapokwenda shule za sekondari na baadaye kwenda Vyuoni waweze kuwa na kile kipaji na baadaye kujijenga zaidi katika michezo angalau tuweze kushinda katika medali za Kitaifa na za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia suala lingine ambalo ningependa kuliongelea ni kuhusu michezo, kwa mfano pale Moshi, tulikuwa na soko la Kiboroloni ambapo kulikuwa kunauzwa mitumba. Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba soko lile sasa hivi limehamishwa lakini lilipohamishiwa kilikuwa ni kiwanja cha michezo kinaitwa *Memorial,* kiko ule Moshi. Kwa hiyo, utakuta kwamba ule uwanja wa michezo wa Moshi, sasa hivi haupo badala yake uwanja ule wa michezo umekuwa ni soko. Nadhani kwa kweli ni muhimu sana kama suala la michezo tunalipa kipaumbele basi liwe hivyo na kama eneo lilikuwa limetengewa kwa ajili ya michezo, Serikali isiligeuze eneo lile kwa ajili ya jambo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala nzima la vituo vya watoto yatima. Najua wengi wamelizungumzia labda katika kuweka msisitizo, ni kwamba sasa hivi tunajua kwamba vituo vingi vya kulelewa watoto yatima, vingine ni vya Serikali lakini vingine ni vya watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utakubaliana nami kwamba siku za hivi karibuni, vituo vingi vya watu binafsi wengine wameviteleza na sijui Serikali imechukua hatua gani. Lakini tatizo la watoto yatima linajulikana wazi na sasa hivi watoto yatima wanaongezeka kutokana na ugonjwa wa UKIMWI pamoja na mafarakano katika ndoa na hivyo kupelekea ndoa nyingi kuvunjika na hivyo watoto wengi kuwa yatima au kubaki mitaani na hivyo kuishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawapongeza wenye vituo hivyo lakini mimi suala ninalotaka kulizungumzia ni suala nzima la usalama wa watoto hao. Katika vyombo vya habari hivi karibuni, tumeona ni jinsi gani nchi ya Chad imekumbwa na kashfa kubwa ya watoto waliokuwa katika kituo wakiwa wanasafirishwa kwenda Ulaya, *actually* walikuwa wanapelekwa Ufaransa na suala hilo limeingiliwa na Rais wa Ufaransa pamoja na Rais wa Chad. Kwa hiyo, nadhani tuna jukumu kubwa au Serikali ina jukumu kubwa la kuhakikisha usalama wa watoto hao, hasa wale watoto waliopo katika vituo vya watu binafsi kwani inawezekana kabisa mtu binafsi akawa amewalea wale watoto, lakini labda ana *connection* na watu wa nje, baadaye akapata hiyo mipango akawapeleka nje. Kwa hiyo, nadhani ile iwe fundisho na tujifunze kutoka Chad tuone ni jinsi gani watoto wetu pia tunaweza kuwalea ili wasije wakachukuliwa wakaenda kuuzwa na wakafanywa vyovyote vile au kudhalilishwa kwa aina yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba katika taarifa nzima ya Kamati, sikuona suala nzima la udhalilishwaji wanawake, kwa sababu ninaamini Kamati hii pia inahusika na suala nzima la jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna kongamano linaloendelea kule Dar es Salaam kuhusu udhalilishwaji wa wanawake na watoto na kwa kweli ni mambo ya aibu kwamba sasa hivi Tanzania bado wanawake wanadhalilishwa vibaya sana, watoto wa kike wanadhalilishwa vibaya sana, lakini sijaona chochote. Kwa hiyo, nategemea kwamba labda Kamati pia ingeweza kupitia TAMWA wakaona wana

ripoti gani ili waweze kutuletea kwa sababu mambo yanayoendelea ni ya kikatili sana kwa wanawake na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala nzima la watoto kupata mimba wakiwa shuleni. Ninaamini watoto kupata mimba pia linahusu Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Watoto wa shule wanapopata mimba za utotoni bado tatizo linakuwa pale pale la umaskini na Kamati hii na Wizara husika zinahusika zaidi na maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la watoto kupata mimba shuleni kwa kweli ni tatizo ambalo nadhani pamoja na kutoa elimu, niliuliza swali hapa Bungeni, Waziri akasema wanafunzi wa shule za msingi wanapata elimu ya uzazi, lakini nadhani bado tatizo litakuwa pale pale na hata wakiwafukuza shuleni tatizo bado lipo pale pale. Kwa sababu Wizara hii kwa kweli ni mtambuka ina *cut across*, nadhani kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuwe na sheria labda sasa watoto wa kike waanze shule wakiwa na miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kibiolojia kwamba watoto wa kike wanavunja ungo wakiwa na umri kati ya miaka 12 mpaka 13, kwa wastani miaka kumi na mbili na nusu kwa Tanzania. Kwa hiyo, utakubaliana nami kwamba watoto wale wakianza shuleni wakiwa na miaka mitano kwa vyovyote watamaliza shule kabla ya hawajavunja ungo. Kwa maana hiyo, watoto wengi wanaharibikiwa kwa sababu hali ile inawafanya kwanza wasiende shule, lakini zaidi ya hapo wanapata mimba. Kwa hiyo, nadhani ifike mahali uje Muswada kwamba sasa iwe ni lazima watoto wa kike waanze shule wakiwa na miaka mitano ili wanapomaliza darasa la saba wawe hawajavunja ungo na kwa hiyo tatizo la mimba litakuwa halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo nataka kulizungumzia ni suala nzima la Wizara hii. Kwa kweli ninakubaliana kabisa na Kamati, siku zote nimekaa hapa Bungeni bajeti ya pili, hakuna Wizara inayopata bajetu ndogo kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na sijaelewa ni kwa sababu gani. Kwa sababu kimsingi, Wizara hii kwa kweli ni mtambuka na ukiangalia kama Kauli Mbinu ya Serikali au ya Chama cha Mapinduzi ya maisha bora kwa kila Mtanzania na Wizara hii ndiyo inayoshughulikia maendeleo basi nategemea kabisa kwamba kama haitapewa bajeti ya kutosha suala la maendeleo au maisha bora kwa kila Mtanzania litakuwa ngumu kwa sababu ukiangalia Wizara hii kila Wizara imo. Kwa hiyo, nategemea kwamba iwe changamoto *next* bajeti basi Wizara hii angalau iangaliwe kwa jicho la huruma ili iweze kufanikisha mambo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu ya kupata bajeti ndogo ndiyo utakuta hata vile Vyuo vya Maendeleo havifanyi kazi mpaka vinataka kuchukuliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kwa hiyo, nadhani waangalie ni jinsi gani Wizara hii inaweza ikapewa bajeti kubwa ili iweze kufanikisha majukumu yake ambayo ninaamini ni mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho kabisa kama muda utaniruhusu, naomba nitoe pongezi zangu nyingi sana kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Kwa kweli *NSSF* wamefanya kazi kubwa sana na hili nalizungumza kwa dhati na hasa nikizingatia suala nzima la ujenzi wa *Mabibo Hostel*. Nakumbuka nikiwa Chuo Kikuu kama Afisa Malazi, tulikuwa tunapata tabu kubwa sana kuanzia miaka ya 90, baada ya kuongezeka kwa wanafunzi lakini nashukuru kwamba baada ya *NSSF* kuingilia kati na kujenga mabweni, kwa kweli tuliweza kupunguza mzigo wa wanachuo zaidi ya 5,000 wakawa wanakaa Mabibo *Hostel.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niungane na wenzangu kwa kuwapongeza wale wote ambao wamepita katika mchakato wa uchaguzi wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi uliopita, nawapongeza sana wote walioshinda na nina hakika Mheshimiwa Naibu Spika ni miongoni mwa watu hao, nawapongezeni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli mambo mengi sana yamezungumzwa ambayo nilikuwa nimepanga kuyazungumza lakini nitagusia moja tu ambalo kusema kweli ni kero kwa nchi hii na ni kero kwa kila mtu na ni kero kiasi kwamba mtu anayetoka nje ya nchi anakuja kufanya kazi ambayo ingeweza kufanywa na mzawa na mzawa huyu akaweza kuishi maisha bora. Hao ni wageni haramu wanaoingia hapa nchini wakija hapa wanakuja kwa mipango mbalimbali wanaweza wakaja kama wachimbaji madini, wanaweza wakaja kama wafanyakazi kwenye mahoteli wakiwa wameitwa na jamaa zao, lakini wengine wanakuja kufanya kazi viwandani. Ukienda mahali kama Dar es Salaam kwenye viwandani kuna Wahindi wamejazana na watu wenye viwanda utakuta ni Wahindi. Ukienda kwenye mahoteli hali kadhalika. Lakini cha ajabu ni kwamba msako ukipitishwa na watu wa Uhamiaji wakienda pale kuangalia kama kweli hao watu wameingia hapa nchini kwa vibali, utakuta hawana vibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nimekuwa nikishiriki kufanya hiyo kazi, lakini kwa masikitiko makubwa wanapokamatwa watu wa namna hiyo inakuwa ni mzigo mkubwa sana kwa Serikali kuweza kupata fedha ya kuwarudisha kwao waliokotoka. Lakini chimbuko la tatizo ni nini? Chimbuko la tatizo ni kwamba hao watu wanakuja bila ya kuwa na tiketi ya kurudi. Lazima tukubaliane kwamba taratibu za wenzetu nje ya nchi huko ili uweze kwenda kule ni lazima uonyesha tiketi yako ya kurudi lakini hapa kwetu Tanzania hicho ni kitendawili. Tunawapokea na kuwaweka kwenye mahoteli, tunawaachia wanazagaa, wana *intermarriages* na hao watu, ni vichekesho Waheshimiwa Wabunge. Dar es Salaam nadhani mnaona jinsi dada zetu wanavyoishi maisha yale kwa kuoana na hao wageni wanaokuja. Sasa na wao wanatumia mbinu kujidanganya wageni wanakuja wakiamini kabisa kwamba akishamuoa msichana wa Kitanzania basi amehalalisha kupata uraia wake wa kukaa hapa nchini lakini hii sasa ni kazi ya Wizara ya Mambo ya Ndani hasa Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Uhamiaji inatakiwa iwe na *records* za wageni wanaokuja. *Records* zinazoonyesha kwamba mgeni ameingia nchini, ameingia tarehe ipi na ataondoka lini, ndivyo inavyotakiwa. Nasema Idara ya Uhamiaji kwa sababu ndiyo inayoshughulika na wageni wanapokuja hapa nchini lakini kwa sababu tupo kwenye mchakato wa Kamati hii ya Maendeleo ya Jamii, nadhani ni vitu viwili ambavyo vinaenda sambamba na nadhani tutapata msaada mkubwa sana kutoka kwenye Kamati hii kwa sababu ninaona Mwenyekiti yupo makini sana katika hili. Ni lazima kuhakikisha kwamba hivi vitu vinafanyika kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ili kuweza kudhibiti uingiaji kiholela wageni hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ambayo yangeweza kufanyika. Mambo yanayoweza kufanyika ni kuchapisha *special form* ambazo zinaonyesha mgeni umeingia lini na mgeni ataondoka lini. Si vibaya hata kumkumbusha mgeni, unakumbushwa kwamba bado una wiki moja ya kuondoka sasa, lakini sisi hii hatuifanyi. Naiomba Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa kweli ifanye kazi sambamba na Wizara hiyo kuhakikisha taratibu zinafuatwa. Nasema kwamba taratibu hazifutwi na ndiyo maana tumeendelea kuwa na wageni wengi wanaokuja kuishi hapa nchini wakifanya kazi kinyume cha taratibu na kuanza kupata ajira ambazo zingeweza kuwasaidia wazawa katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la fedha pia lipo kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ikiwa ni pamoja na Idara hii ambayo kazi yake kubwa ni kudhibiti wahamiaji haramu wanaoingia hapa nchini. Kusema kweli hawana fedha za kutosha na kama wangekuwa na fedha za kutosha, nina imani kubwa kabisa kwamba tusingekuwa na utitiri wa wageni wa namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni kuwadhibiti hao watu wanaokuwa na viwanda. Hao watu wanaokuwa na viwanda hapa wanakuwa na taratibu zao ambazo zinaingilia taratibu za nchi. Sasa kama hawawezi wakafuata taratibu zilizowekwa na nchi kwamba mfanyakazi lazima awe ni mzawa basi kama mtu akikiuka ama ana kiwanda ama ana Kampuni ya uchimbaji madini, basi huyo mimi kwa kweli

sitafurahi kama hataweza kunyang'anywa leseni ya kuendesha shughuli yake kwa sababu ndiyo changamoto ya kukaribisha hao watu ambao ni kero hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nizungumze kidogo tu mambo ambayo nilitaka kuyazungumza, naona mengi yamekwishazungumzwa, lakini nizungumzie kidogo kuhusu michezo. Vijana wengi sana wanazurura, wanakosa kitu cha kufanya. Nadhani kama michezo ingetiliwa mkazo nina hakika kwamba vijana wengi wangeweza kujihusisha sana na michezo na kutokupata muda wa kuzurura, lakini kwa bahati mbaya kabisa kwamba ukienda wilayani, mikoani utakuta viwanja havipo, vijana wana ari ya kuendelea na michezo, lakini unakuta kwamba hawana viwanja, hawana mpira. Lakini kuna Maafisa Utamaduni na Ofisi za Utamaduni zipo, kila Wilaya ina Ofisa wa Utamaduni, wanafanya kazi gani? Nina wasiwasi kwamba hawa Maafisa Utamaduni wanachaguliwa wale ambao hawana hamasa ya michezo, ndiyo maana hali ya michezo imerudi nyuma kabisa.

Sasa hivi tunafurahi kwa kuona kwamba Timu ya Taifa inasonga mbele. Sasa macho yetu yasiwe kwenye Timu ya Taifa tu, wachezaji wapo. Wachezaji wanatoka huko Wilayani ndio wataunda Timu ya Taifa. Lakini kama tutakazania Timu ya Simba na Yanga kwa sababu ziko Dar es Salaam tutaona kwamba kweli kwa upande wa michezo vijana hatuwatendei haki. Ni lazima Serikali ihakikishe kwamba inatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba viwanja vinatengenezwa karibu katika kila Wilaya na inawezekana kabisa. Hata kuchangia, Serikali inaweza ikachangia na uongozi wa Wilaya na wananchi wenyewe kwa sababu na wenyewe wanahamasika na michezo wakaweza kuchangia fedha zao kwa ajili ya kutengeneza viwanja ambavyo vitawapa hamasa vijana kuendelea na michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nije kwenye kipengele cha vituo vya kulelea watoto. Wote hapa tunazungumza sijui kituo cha Mabibo kituo, hosteli ya Mabibo, mimi natoka Kigoma kwani nikisema hosteli iwe Kigoma kuna tatizo gani? Hizi hosteli ziwepo nyingi basi! Hosteli ziwepo kikanda, lakini zinakuwa ni hosteli mbili, wakati watoto yatima wako nchi nzima. Sasa hatuwezi tukategemea hosteli moja au hosteli mbili zikawatosheleza. Nadhani ni dhahiri kabisa kwamba umefika wakati sasa kama Serikali inataka kusaidia watoto yatima lazima basi hizi hosteli zijengwe kikanda kwa maana kwamba watoto wa mikoa minne labda wanaweza wakaenda kwenye hosteli fulani kuliko mtoto atoke Kigoma apelekwe hosteli ya Mabibo. Kufanya hivi itakuwa vigumu kwa sababu Waheshimiwa Wabunge lazima tukubaliane kwamba wakati mwingine sisi Wabunge tunabeba mzigo. Tunapokwenda huko Wilayani utakuta watu wanakuja, huyu mtoto hajiwezi, sasa wewe Mbunge unamsaidia namna gani? Lazima usaidie hii *allowance* tunayopata hapa ndiyo tunakwenda kuwagawia watu kule. Lakini kwa nini tusifanye hivyo sisi.?

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli lazima Serikali ijizatiti kuwasaidia hawa watu, hivi vituo vijengwe, tusitegemee kituo kimoja, hata hivyo tunasaidiwa na watu wenye *NGOs* binafsi, wanasaidia sana watoto. Kama Serikali haiwezi basi kufanya hivyo iwaunge mkono hao wenye *NGOs* zinazosaidia watoto ili waweze kuwa na uwezo wa kuwasaidia watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema sikuwa na mengi ya kuzungumza kwa sababu mengi yamezungumzwa na yote yako wazi lakini kero yangu kubwa hasa ni wageni haramu ambao wameshaenea kila mahali. Sasa utafikiria nchi ni ya wageni lakini wanakaribishwa na watu ambao tunao humu ndani. Nakushukuru sana.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kujadili na kutoa maoni yangu kuhusiana na Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Kwanza kabisa nianze kutoa pole zangu, niungane na wananchi wote wa Mkoa wa Mara katika kutoa pole kwa kifo cha aliyekuwa Mheshimiwa marehemu Salome Mbatia, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kwa kweli sisi wana-Mara tumesikitishwa sana na kifo chake kwani kabla hajafariki alitutembelea kule Musoma, kwa hiyo, tumesikitika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na pole hizo napenda pia nikupatie pongezi wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa *NEC* na hatimaye kuingia kwenye Kamati Kuu, nakupongeza sana.

Vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, dada yangu Jenista Mhagama kwa kuchaguliwa kuingia katika *NEC*. Vilevile nawapongeza Wabunge wote waliochaguliwa kuingia *NEC*. Aidha, napenda pia kuipongeza Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa kazi nzuri sana waliyofanya. Pamoja na ufinyu wa bajeti lakini imejitahidi kutembelea maeneo mbalimbali na kuangalia shughuli zinazofanyika, nawapongeza sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu nianze kuchangia kwanza kabisa nielezee umuhimu wa Wizara hii. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kweli inachukuliwa kwa ufupi sana. Ningeiomba Serikali izichukulie kwa mapana kazi za Wizara hii, kwani inagusa makundi mbalimbali ya watu. Kitu kingine ambacho ningependa kuishauri Serikali nafikiri Mheshimiwa Rais ananisikia kama kunatakikana kufanya *replacement* ningemwomba Mheshimiwa Rais safari hii atupatie Naibu Waziri mwanamume kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwenye Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto tuna Mwenyekiti mwanamke na Makamu mwanamume na wameonyesha umahiri mkubwa hasa Makamu ambaye ni mwanamume. Kwa hiyo, namwomba kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais safari hii atupatie Naibu Waziri mwanamume kwenye Wizara hii. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuelezea umuhimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Asubuhi nilikuwa na swali kuhusiana na umuhimu wa Vyuo hivi kwa kweli niliridhika sana na majibu ya Waziri aliyonipatia. Lakini nina tatizo kidogo kwani sifahamu utekelezaji wake utakuwa lini. Kwa kweli vyuo hivi vina hali mbaya sana. Nikichukulia chuo kilichopo katika Mkoa wangu Chuo cha Buhare, Chuo hiki kina hali mbaya sana, kina zaidi ya wanafunzi 300 lakini kina walimu 2 tu.

Tunaweza kufikiria ni nini kinafanyika chuoni hapo. Wapo wanafunzi zaidi ya 300 walimu 2. Chuo hiki hakina gari, kina mpishi mmoja. Kwa maana nyingine naweza kusema chuo hiki ni kama vile kimekufa. Kwa hiyo, naiomba Kamati ya Maendeleo ya Jamii ikiongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Jenista Mhagama, ifunge safari na kuja mkoani kwangu Mara kutembelea chuo hiki na kuona kwa namna gani wanaweza kuishauri Serikali ili iweze tena kukifufua chuo hiki cha Maendeleo ya Jamii cha Buhare.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusiana na *NGOs*. Kwa kweli kumezuka mtindo mmoja ambao ni wa ajabu sana, kwa maneno mengine naweza kusema ni mtindo wa kitapeli. Watu wanasajili *NGOs*, lakini hizi zinabaki kwenye mifuko, hazifanyi shughuli yoyote. Sisi Wabunge tumeona na tumethibitisha haya katika mchakato mzima wa kufuatilia masuala mbalimbali ya UKIMWI. *NGOs* zipo kwenye mikoa yetu lakini hazijulikani hata ofisi ziko wapi na zinafanya nini. Kwa hiyo, ningeomba Kamati hii ifuatilie *NGOs* zote na kuhakikisha taarifa zao zote zinakwenda Serikalini na kwenye Wizara zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuliongelea, wenzangu wengi wameliongelea labda tu kwa lugha nyingine naomba niweze kusisitiza ni hili suala la ongezeko la ajira kwa wageni. Mimi inanipa taabu sana. Katika nchi yetu tuna wasomi wengi sana, tuna watu ambao ni *professionals* lakini wanatembea tu mitaani na mafaili, hawana kazi, ukiangalia kwenye viwanda vingi walioajiriwa ni wageni. Mimi nashindwa kuelewa ni kwa nini tunapenda sana kuwaajiri wageni, kwa nini tusiwe kama nchi zingine ambazo huwafikiria kwanza watu wao?

Mheshimiwa Naibu Spika, na sisi tuhakikishe kwamba watu wetu wanapata ajira halafu angalau wawepo wageni kidogo. Unakuta labda viwanda vya madawa, wafamasia wote ni wageni, naongelea viwanda vya madawa kama hivi vya Wahindi. Ukienda pale unakuta wafamasia ni Wahindi wakati sote tunajua kwamba wafamasia wako wengi na wamebakia mpaka kwenye maduka ya dawa baridi, hamna kazi. Sasa usawa uko wapi? Kwa hiyo, naomba sana hili liangaliwe na tujaribu kupunguza hicho kiwango kikubwa sana cha ajira za wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niongelee suala la watoto wa mitaani. Mimi ninapoongelea suala la watoto wa mitaani inanisikitisha sana, naona kama suala hili halijapewa umuhimu wala halijachukuliwa kwa umakini. Kwa sababu sasa hivi kuna watoto wengi sana wanaozurura mitaani na

wale ambao wameonekana kuwa *matured*, kwa mfano, wanawake wengi wamepewa mimba na hatimaye wengi wao wameambukizwa gonjwa hatari la UKIMWI. Sasa sijui tunafanya nini hapa?

Kupitia Kamati hii, naomba ijaribu kusaidiana na Wizara katika suala zima la kuhakikisha watoto wa mitaani wanapungua. Serikali iandae makazi maalumu angalau kila kanda. Na zamani kulikuwa na mtindo wa kukusanya watoto wa mitaani, ombaomba na kadhalika na kuna sehemu walikuwa wanahifadhiwa. Lakini sasa mtindo huo hatuelewi umeishia wapi na hatimaye watoto hawa wamekuwa wakizagaa ovyo mtaani na wale mabinti wakikamatwa na kupewa mimba na hatimaye kuambukizwa gonjwa la UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa kuongelea vituo vya watoto yatima. Napenda kuwashukuru wale wote ambao wanajishughulisha na suala zima la kutunza watoto yatima. Lakini kumekuwepo na tatizo moja kwa vituo hivi vya watoto yatima. Unakuta watoto wamefikia umri wa kwenda shule lakini hawawezi kwenda shule na wengine kwenda Sekondari lakini bado wako kwenye vituo vile. Kwa hiyo, naiomba Kamati ijaribu kutembelea vituo vile na kuangalia wale wote ambao wanatakiwa kwenda shule kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu waweze kuingia shule watoto hao badala tu ya kukaa pale kwenye zile kambi bila ya kwenda shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa kuongelea Kambi moja ambaye huwa inaniuma sana. Sina uhakika kama Kamati hii imetembelea Kambi hiyo. Mimi nilipata fursa kuitembelea Kambi ya Wakoma Nunge Kigamboni. Katika Kambi ile naishukuru imejengwa vizuri sana, lakini Wakoma wale baada ya kuwekwa pale ni kama wamesahaulika. Kuna kipindi wale Wakoma wanakaa pale kwenye ile kambi bila chakula. Naiomba Kamati kama inataka kudhihirisha haya wajaribu kuitembelea kambi ile. Wale Wakoma wanatabika pale, wanasubiri tu misaada ya watu wanaokwenda kuwatembelea waweze kuwapatia chakula. Kwa hiyo, naiomba Kamati itembelee Kambi hiyo na kuweza kuishauri Wizara namna ya kuwakimu wale Wakoma kwani nao wanahitaji kutunzwa kama wanavyotunza binadamu wengine wowote hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda tena kuishukuru Kamati hii, kwa kweli inafanya kazi nzuri sana. Lakini nitaridhika zaidi kama Kamati hii itafanya ziara Mkoani Mara na kwenda kutembelea kile Chuo cha Buhare. Chuo kile kwa kweli kina hali ngumu sana, wanafunzi wako pale lakini hawana walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi, ahsanteni wote kwa kunisikiliza.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, nilikuwa namtuliza jirani yangu hapa atulie na mimi nipate nafasi ya kuchangia ili nisije nikapoteza yale ambayo nimeyapanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze kwanza kwa dhati mwasilisha hoja Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati, ameiwasilisha kwa ufundi, kwa ustadi, kwa kweli inaonekana ni utafiti mzuri sana na mimi naiunga mkono hoja.

Baada ya pongezi zangu naomba nitoe salamu za rambirambi kwa familia ya marehemu Salome Mbatia ambaye amepoteza uhai wake juzi tu pamoja na Wizara husika ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Imepata pigo kubwa kwa sababu Mheshimiwa Marehemu Salome alikuwa ni mchapakazi na wote tulikuwa tunamwona jinsi ambavyo kwa kweli alivyokuwa amejitolea kuitumikia Serikali kwa moyo wake na kwa nguvu zake zote, Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *(Amin)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie katika uboreshaji wa hoja za Kamati. Kwanza niiombe Serikali ijitahidi kwa kadri inavyoweza Idara inayohusika na Utumishi ihakikishe kwamba inaiongezea Wizara watumishi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ni kwamba kati ya watumishi wanaotakiwa 3,300 inao watumishi 1,095, hali inayoonyesha kwamba wanayo theluthi moja ya watumishi na kwa hiyo

inapungukiwa watumishi karibu theluthi mbili ambao ni watumishi 2,205. Namba hii ni kubwa sana na kwa vyovyote vile kwa kweli inakuwa ni vigumu kuweza kufanya kazi za Wizara kadri inavyopasa. Naishauri sana Serikali upande wa utumishi iangalie ili iweze kupunguza kwa kiasi kikubwa huu upungufu wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile iliendana na kuboresha bajeti ya Wizara kama ambavyo wenzangu wamezungumza, hilo sitalizungumzia kwa undani kwa sababu wenzangu walivyozungumza na mimi nawaunga mkono. Lingine naomba nilizungumze kwa kifupi sana ni kuipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo inaboresha suala zima la michezo. Lakini kulingana na kwamba tatizo hili lilikwishakuwa la muda mrefu, imekuwepo ile hali ya kutokujali viwanja kwa ajili ya watoto wetu wadogo.

Huwezi ukategemea kukuza kipaji cha mchezaji katika umri wa utu uzima. Kipaji cha mchezaji kinakuzwa anapokuwa ni mdogo. Tangu wale wanapocheza kinachoitwa chandimu, wasichana wakifunga matambara wakiwa wanarushiana mipira ndio wakati ambapo mtoto anapoweza kujulikana kipaji chake. Viwanja vyote sasa hivi havipo na hata Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi hapa kwa kweli haijapewa nafasi yake kwa sababu kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kila kijiji kinatakiwa kitenge eneo kwa ajili ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi baada ya kuwa ardhi imekuwa chini ya Serikali za Vijiji, baadhi ya viongozi wenye uchu wameuza maeneo ya vijiji kwa watu binafsi, wamevibinafsisha pasipokuwa na utaratibu, matokeo yake hata watoto wetu sasa hivi hawana mahali pa kuchezea michezo.

Naomba suala hili liangaliwe, watoto wetu wapate viwanja na vitunzwe kizazi hiki cha leo na vizazi vijavyo kusudi watoto wetu waweze kupata mahali pa kuchezea na taifa letu lipate mahali pa kujifunzia watoto wetu na kuweza kupata watoto ambao wana vipaji kuliwakilisha Taifa letu na kuleta heshima kwa upande wa michezo. Si vizuri sana kuipuuza sana michezo na wala tusitegemee kwamba tutapata wachezaji kwa kutumia uwanja wa Dar es Salaam tu, uwanja huu wanakwenda ambao wameshakuwa mahiri, lazima tujue tunawatoa wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ninalopenda kulizungumza ni kuhusu *SACCOS*. Kuianzisha *SACCOS* mpaka ifike mahali pa kupata sifa na ikajulikana ikapata usajili ni kazi kubwa sana. Lakini kazi hii kubwa ambayo imekuwa imekwishakamilika inapofika wakati wa kupata mikopo *SACCOS* hizi zinapata matatizo makubwa kweli kweli ya kupata mikopo. Wanaobahatika kupata mikopo wanakumbana na mikopo yenye riba kweli kweli.

Nimepata kusoma kwenye gazeti *SACCOS* moja ilichukua mkopo *CRDB* kwa asilimia 10 na yenyewe inakwenda kuutoa kwa asilimia 11. Hebu niambie sasa huyu mwanachama anapata faida gani ya kuwa ndani ya *SACCOS* na ni vigumu sana kwa mwanachama mmoja mmoja ama kwa mwananchi mmoja mmoja kupata mkopo wa moja kwa moja kutoka kwenye Benki. Lakini tunategemea kwamba huyu mwanachama ambaye yuko ndani ya *SACCOS* ndiye mwenye urahisi na wepesi wa kuweza kupata mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba, ni kwamba riba hizi ziangaliwe, zisiwe kubwa sana kuwaumiza hawa wananchi waliojiunga kwenye *SACCOS* lakini vilevile naomba inapokuwa imekusudiwa kutoa mikopo ni lazima elimu ya biashara na uendeshaji wa mikopo ipewe uzito. Vinginevyo fedha hizo zitakwenda kupotelea ndani ya *SACCOS* na *SACCOS* hizi zitakufa kwa sababu watashindwa kuziendesha na kuzirudisha kwa jinsi inavyotakiwa na ndani ya wakati na badala ya kupenda mikopo wakaichukia.

Kwa sababu ya historia ya watu ambao wamewahi kuuziwa nyumba zao, watu wengi walikuwa wameigopa mikopo ya Benki kwa kudhani kwamba mkopo wa Benki maana yake ni kutoa muhanga mali uliyonayo. Lakini naomba tena chini ya *SACCOS* inawezekana kabisa mtu akaweza kupata mkopo, akapata elimu ya kuendesha na akaweza kupata faida na pia akaweza kurudisha ule mkopo na hata wengine wakaweza kupata faida. Kwa hiyo, ninachoomba elimu ya kutosha itolewe ili kila *SACCOS* iweze kuhakikishiwa kupata mkopo. *SACCOS* isiishie kuwa maneno tu, zimekuwepo, tumekwishapata watu wamejiunga lakini bado hazijaweza kuwa na hakika ya kupata mikopo. Wapate mikopo na elimu ili waweze kufaidika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda nilizungumze, ninapenda niipongeze sana Kamati kwa jinsi ilivyoelezea juu ya utaratibu mzima wa mkakati wa Serikali katika kuongeza ajira na niipongeze Serikali katika suala zima la kuongeza ajira zipatazo milioni moja ifikapo mwaka 2010.

Serikali imeweka jambo hili vizuri naipongeza sana. Kitu ninachoomba sana hali za watumishi na wafanyakazi ziangaliwe. Kuwe na hali bora za wafanyakazi na watumishi katika maeneo mbalimbali kusudi isiwe kwamba watu wanaweza kupata ajira lakini ukakutana na tatizo la mishahara, tatizo la mazingira mabovu, wakakutana na huduma mbovu.

Ni jana au juzi kwenye gazeti moja kijana amekatika vidole, lakini amekatika vidole kwenye mashine mahali ambapo yule mwenye kiwanda kile wala hata hamjali. Sasa hali hii inakatisha tamaa, ajira kweli ameipata kijana, amefurahia lakini alipoteza vidole sasa anabaki anahangaika mwenyewe, hii haiwezi ikawa ni furaha, hatuwezi tukashangilia hizi ajira, tunaomba kwamba ajira ziende pamoja na kuboresha mazingira na kujali hali za wafanyakazi katika maeneo ambapo zitapatikana kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kima cha chini cha wafanyakazi. Naipongeza Serikali kwamba mara kwa mara ina utaratibu wa kuboresha kima cha chini tuseme karibu kila mwaka. Lakini kima cha chini hiki kimekuwa na pengo kubwa sana kati yake na kima kingine kinachofuata kima cha juu.

Kwa hali halisi kima cha chini bado kiko chini sana. Naomba kiboreshwe walau kimwezeshe huyu mfanyakazi kuweza kumudu maisha yake na kuweza kutumia fedha zake hizo kwa mwezi na ziweze kumsaidia na kufikia malengo yake ambayo ameyapata. Kwa hiyo, nashauri kwamba ajira mpya za vijana ziendane vilevile na kuboresha maisha ya wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kustaafu kazi ni kazi, wapo wachache wetu humu ndani ya Bunge ambao wamekwishastaafu kazi wanaelewa. Lakini sisi wengine tunalijua hili kwa hisia kwamba kustaafu kazi ni kazi. Kwa hiyo, ni vizuri sana kuboresha maisha ya wafanyakazi ambao wamestaafu.

Kwa kweli kustaafu kazi ni kuongeza gharama za maisha, kwa sababu mtu anapostaafu kazi hapo ndipo mwisho wa safari *imprest*, mwisho wa kazi za ziada, mwisho wa kupewa posho za matibabu, mwisho wa kupata posho za nyumba, mwisho wa posho za usafiri, ni mwanzo wa maisha magumu. Wakati huo huo wakati mtu amefika katika hatua ya kuwa katika maisha magumu ni wakati ambao amekwisha kuzeeka, umri wake umekwisha kuweza kufanya kazi tena. Kwa hali hiyo unakuta ni wakati mtu anatakiwa aangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri Serikali iwaangalie wastaafu kwa jicho la huruma sana ikizingatia kwamba kuja kufika umri wa kustaafu mtu amepita katika vikwazo vingi sana. Amepita katika hali za namna mbalimbali mpaka amefikia kutunukiwa heshima ya kustaafu kwa kweli ni vizuri Serikali imtunze. Kwa maana kwamba kima cha chini hiki kilichokuwepo sasa hivi kwa ajili ya wastaafu naomba kiendane sawasawa pasipo kupungua, ikibidi kiwe ni zaidi ya kima cha chini cha mfanyakazi aliyepo kazini.

Sana sana kibadilike kadri kima cha chini cha mfanyakazi aliyepo sasa kinavyobadilika ama kiboreshwe hata zaidi ya pale kwa sababu huyu anatakiwa baada ya kustaafu aendelee kuishi maisha yake ya kawaida. Kama alikuwa mpangaji alipie nyumba ile, maji, umeme, asomeshe watoto wake ambao pengine walikuwa hawajamaliza kusoma, vile vile aendelee na maisha yake kama kawaida naye ajichanganye na jamii nyingine. Huyu Mtanzania aliyestaafu asitengwe katika jamii kama vile kule kustaafu kwake ilikuwa ni makosa. Ninaomba wastaafu wapewe kipaumbele, waangaliwe kwa maslahi yao na waweze kumudu maisha yao na gharama za maisha baada ya kuwa wamestaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nayo mengi ya kuzungumza, lakini napenda nikiri kwamba wenzangu waliozungumza kwanza wamechangia vizuri na kwa mujibu wa taratibu zetu sina haja ya kurudia yale ambayo wamekwisha zungumza. Kwa sababu hiyo nirudie kusisitiza juu ya hili suala la ajira nililolizungumza sasa hivi kuhusu hali bora za wazee wetu na wafanyakazi vilevile, na kuiomba Serikali iboreshe maisha yao na iangalie uwezekano wa kuongeza wafanyakazi katika Wizara ya

Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto. Hili ni suala la msingi sana kwani kazi haziwezi kufanyika bila ya kuwa na watenda kazi .

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naendelea kuiunga mkono hoja ahsante sana.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Bunge lako Tukufu, awali ya yote na mimi kwa sababu ni mara yangu ya nizungumze kuhusu suala zima la msiba wa Mheshimiwa Salome Mbatia. Tupeane pole humu sisi Wabunge wa Jamhuri ya Muunganao wa Tanzania kwa kumpoteza mwenzetu ambaye alikuwa kipenzi chetu, ambaye tulikuwa tukimpenda sote lakini kifupi tu ni kwamba tulimpenda kweli, lakini nadhani Mungu amempenda zaidi.

La pili, niendelee kuwapa pole wale wote waliojaliwa kunusurika katika misafara mbalimbali au katika shughuli za utekelezaji ndani ya Chama na Serikali ya nchi hii ili basi waendelee kufarijika kwamba Mungu amewanusuru na leo bado wapo duniani.

La tatu, napenda kuwapongeza wote mlioshinda ndani ya Chama cha Mapinduzi, Chama Tawala ukiwemo wewe Naibu Spika na Mwenyekiti wa Kamati hii na wote ambao mliingia katika mchakato mkubw. CCM haina mchezo, yenyewe huwa inatafuta kweli walio wakweli na wanapata katika kuliongoza jahazi hili ndani ya Chama cha Mapinduzi akiwemo Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi, Rais Jakaya Mrisho Kikwete, hongereni sana wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nacharurwa kwa Kiswahili lakini nitaendelea tu. Ninachotaka kusema katika suala zima la taarifa hii ya Wizara maana yake naomba niiseme mapema nimemwuliza mwingine inaitwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Nafahamu ni kwamba moja waliloongelea kwanza napenda niipongeze taarifa hii, kwa kweli wameiandika kifupi na inaeleweka. Ni taarifa nzuri chini ya Mama Jenista Mhagama, ameiandika vizuri sana. Lakini mahali popote palipo na andiko na meza ikaruhusu kuzungumza basi yapo mawili, matatu ya kuweza kuchambua na kuwekana tu sawa lakini kwa nia njema ili tuweze kuelewana vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza mimi ningependa kuongelea *NGOs*. Hivi *NGOs* ni nini na Serikali ni nini? Ninaongea hivi kwa makusudi mazima kwa sababu unaweza ukakuta yaani watu wanaamua kuunda *NGO* fulani, wanaamua kabisa kuunda Taasis Isiyo ya Kiserikali, hawajui lolote waanzie wapi, hawajui hata kuandika hata andiko, hawajui wafanye nini. Wanawafuata wataalamu wale wale ambao tunaishi nao ofisini mwetu kwenye Wizara zetu zile zile, ndiyo wanawalipa wawaandikie maandiko, wawafanyie taratibu zote ili *NGO* yao iwe *live*. Mimi huwa najiuliza, hivi sasa kama Serikali ndiyo inayajua haya na mara nyingi inawajua hata wafadhili mahali walipo na jinsi gani wanaweza wakafanya maandiko wakafanya vyovyote wanavyoweza, inaruhusu *NGO* hizi kuwa utitiri nchi nzima, hivi kazi ya Serikali ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusifanye juhudi za makusudi kuzipunguza *NGOs* kwa sisi kujua tunapaswa kufanya nini ili hizi *NGOs* ambazo nyingi huwa ni za mifukoni tuzipunguze kwa kujua sisi tunapaswa kufanya nini ili kama ni kulea watoto tuwalee, kama ni kuwaelea walemavu tuwalee, kama ni kulea watoto yatima tuwalee. Kwa nini tunashindwa kufanya hivyo? Hilo ndilo suala linaloniweka njia panda. Kwa nini tunashindwa kuwa kweli wakakamavu ili tupambane na *NGOs* hizi. Tunapozungumza masuala ya kusema *NGOs* nyingi ni za mifukoni ni kwa sababu hiyo.

Napenda niwe wazi, sasa ninaomba Kamati hii iweze kuona njia pekee tu kabisa za kuweza kujadili na waone jinsi ya kupunguza hizi *NGOs* hizi. Jinsi zinavyofanya *NGOs* basi Serikali ifanye ili kusudi tuweze kuzipunguza. Maana hata katika taarifa yao wanasema kuna udanganyifu mkubwa, wanasema hawa ni watoto yatima kumbe si yatima, huyu mtoto anaishi katika mazingira magumu kumbe hapana! Hii yote huyu anayemdanganya anatafuta asaidiwe na *NGO* kwa sababu Serikali imeshindwa. Naomba tuwe makini katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo napenda niliongelee ni suala la vikundi hivi ambavyo vinajiunga lakini inafika mahali wanasema hawana soko mahala pa kuuzia bidhaa zao. Niliangalia safari

moja katika runinga nikakuta kuna ziara nadhani ilikuwa kama si ya Rais basi ilikuwa ni ya Waziri Mkuu. Kwamba kuna sehemu kulikuwa na soko la kuuzia masoko ya nafaka sikumbuki ni mkoa gani. Lakini jinsi gani wanawake wale nilivyowaona walifurahia, wamelima mazao wana mahali pa kwenda kuyauzia mazao yao. Wanapeleka na wanashangilia, wanapiga vigelegele kama nini. Sasa tatizo la sisi ndani ya nchi hasa hasa akinamama ndiyo mara nyingi wanaachiwa kazi hizi za biashara ndogo kikiwemo kilimo na mazao madogo madogo haya, tunakosa kuwatafutia soko. Lakini anapolima apeleke wapi, Kamati niiombe ijadili kwa undani kabisa katika taarifa zao wapi wanaweza wakapata kutatua tatizo hili ili kusudi hawa wananchi wanaoshughulika na biashara ndogo ndogo wanapopata mazao yao wayauze wapi? Peke yake Mkukuta wala hatutausikia baada ya miaka yetu mitano Bungeni hapa. Akipata tu mahala pa kuuzia mazao yake mama huyu hakuna kabisa, na wala hilo neno MKUKUTA litakwisha hamtaamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimepigiwa kengele lakini napenda kusema kuna hoja inazungumzwa kuhusu suala zima la mtoto wa kike aanze shule akiwa na miaka mitano. Ndugu zangu sijui tunasahau, hivi anapoanza miaka mitano ndiyo kakomaa? Tunasahau huku nyuma wahalifu vibaka hawa na hawa watu wazima hawa, madume haya yanawaingilia watoto wakiwa na miaka mitatu mnasahau hilo?

Leo atakapokuwa na miaka mitano atakuwa ameshawekewa kufuli gani, hebu tulione hili. Miaka mitano haisaidii kama hatutajadili kikamilifu jinsi ya kuwaadhibu hawa wanaomwingilia mtoto wa kike akiwa na miaka mitatu na kuendelea, wala haisaidii. Miaka mitano atakuja kumaliza darasa la saba ana miaka mingapi? Kama kuna uovu, uovu hauna miaka. Niwaombe katika hili tuendelee tu kujadili adhabu ya kumwadhibu huyu anayemwingilia kimwili mtoto wa kuanzia mwaka mmoja na kuendelea. Mnacheka nini? Mnacheka kwa sababu mnawaingilia? (*Kicheko*)

Miaka mitano narudia haitasaidia! Niombe tujadili adhabu ya kuwaadhibu hawa. Mimi hicho ndicho ninachokisisitiza kabisa ili tuikomeshe hii na tukijua kuikomesha watoto wetu wa kike watasoma kwa amani mpaka hapo watakapoweza kuchukua nchi hii hadi wenyewe kuwa Marais.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba nimalizie kabisa niiulize Wizara hii au Kamati hii; je, inapoongelea masuala ya watoto wanamwongelea na yule mtoto mlemavu aliyekataliwa shuleni Kigoma, Kasulu kitu kama hicho? Mlemavu yule amekwenda kutafuta shule mwenyewe anakataliwa; je, katika hili tunalizungumza vipi? Mtoto anajitokeza ndani ya familia bila kutafutwa na Kamati, bila kutafutwa na Serikali, anatafuta mwenyewe! Tuone aibu katika hili lililojitokeza ndani ya vyombo vya habari. Hawa watoto wanaozaliwa katika hali hiyo labda kuwepo Sheria au kuwepo na taratibu za kuwaokoa hawa bila kujitafutia wenyewe nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu haya, naiunga mkono taarifa hii ahsante sana!

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nadhani Serikali na watu wengine wote wameisikia hiyo hoja ya mtoto huyo. Sasa nitamwita msemaji wetu wa mwisho kwa upande wa Wabunge, Mheshimiwa Chacha Wangwe.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu na kabla sijaanza kuichangia ningependa kutoa rambirambi zangu kwa Marehemu Lucky Dube. *(Makofi/Kicheko)*

Najumuika na *Jah People* wote duniani kwa sababu huyu alikuwa ni mwanasiasa mwenzetu ila aliamua kutoa *message* yake kwa njia ya muziki na ilifika kama vile Bob Marley, kwa hiyo, najiunga na ndugu zake wote walioko Inanda Kwa Zulu Natal na *Jah People* waliopo kila mahali Kingstone Jamaica, Afrika Magharibi na kule Ethiopia. Sasa manake hatuamini katika kifo, tunaamini kwamba anaishi daima na *message* yake itaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la maendeleo ya jamii, jinsia na watoto napenda kusema kwamba Wizara imeshindwa vibaya. Kamati imejitahidi sana kuchangia na nampongeza Mheshimiwa Mama Jenista Mhagama. Lakini hii ndiyo Wizara ambayo imeshindwa vibaya sana katika Wizara zote katika Serikali yetu kwa sababu haina *planning*. Hakuna mikakati yoyote ya kuendeleza jamii, jinsia na watoto wa nchi hii na nitatoa mifano.

Wizara hii haijali kitu kinachoitwa rasilimali watu. Kwa sababu rasilimali watu ndiyo mali muhimu tuliyonayo nchini na kwa sababu ya kushindwa kwake ndiyo maana sasa hivi tuna watu wanaoitwa watoto wa mitaani, kwa kumaanisha kwamba hawana baba wala mama wala mlezi. Tuna wazee wa mitaani, hawa hawazungumziwi kwa sababu Wizara inaona hawana maana yoyote. Kuna vijana wa mitaani, hawa ndiyo wanaoitwa wazembe na wazururaji, vibaka machinga na changudoa. Tunasahau kwamba hawa ni watoto wetu ambao tumeshindwa kuwapa malezi mazuri elimu na ajira. Huku ni kushindwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi wiki iliyopita kuna wazungu walikamatwa huko Chadi katika Mji Habeche wakiwa wameiba watoto ndege nzima. Kwa hiyo, hii inaonekana kwamba wenzetu baada ya Sera zao za kupunguza kizazi kushindwa sasa wanaanza kuiba watu ili wawe na watu. Lakini sisi hatuoni kwamba hawa watu tulionao wana maana yoyote ndiyo maana wanaranda randa mitaani, watoto kabisa ambao tumewazaa sisi tunawaita watoto wa mitaani wengine baba zao ni Wabunge, wengine baba zao ni watu wenye ajira lakini sasa kwa sababu ya ile *irresponsibility* ambayo ni ya Serikali. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Una maanisha Wabunge wa sasa na wa zamani pengine?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ndiyo, sio wa sasa tu hata wa zamani. (*Kicheko*)

Hao watoto wanarandaranda nchi nzima na ni wengi mno ndiyo maana hata kule Kanda ya Ziwa tulikuwa tuna Kituo kinaitwa Kuleana, ni kwa sababu wale watoto walikuwa kila mahali wanaranda randa. Ukienda Mbeya unawakuta, Kigoma unawakuta, Dar es Salaam wamejaa. Lakini hili ndilo suala ambalo hii Wizara ingeangalia namna ya kutunza hawa watoto ili nao baadae waje wawe ni wananchi wenye manufaa katika nchi hii badala yakuwapoteza huko mitaani.

Kitu kingine ambacho Wizara hii imeshindwa kukiangalia ni utaratibu wa malezi kwa sababu tulikuwa na utamaduni wetu wa Kiafrika ambao ulikuwa na namna ya kuwapa watu maadili ya kuweza kufahamu kwamba kujamiiana ovyo hakufai, kwa hiyo, hilo lilikuwa halitokei watu walikuwa wanasubiri mpaka waoe au waolewe. Tulikuwa pia na utaratibu wa kuelewa kwamba kitendo cha kumpa mimba mtoto wa mtu ni kibaya na binti mwenye alikuwa anafahamu kwamba ni vibaya kukubali kupewa mimba. Lakini sasa jinsi ya watoto wetu wanavyopata mimba katika shule zetu kwa maelfu inaonyesha kwamba ni kushindwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kuwapa watu maadili ya kuelewa kwamba hicho kitendo hakifai. Kwa hiyo, hili ndilo wanapaswa waliangalie kwamba je, tutawapate Watanzania maadili ya kuelewa hicho kitendo hakipaswi kufanyika kwa wakati ambao haufai.

Kwa hiyo, kutoa adhabu kali na kutunga Sheria za adhabu kali ni ishara ya kushindwa kwa Serikali yetu kuweza kuwashauri na kuwalea wananchi waelewe maadili muhimu. Kwa sababu adhabu haisaidii. Adhabu kali haitasaidia hata kama tutawanyonga kama vile Wabunge wengine walivyosema au kama watahasiwa na inaonekana kwamba inaelekeza kwa kijana wa kiume lakini haielekezwi kwa kijana wa kike kwa kuelewa kwamba wanakubaliana.

Nadhani adhabu ambayo ingefaa ni moja tu ile ambayo mababu zetu walituonyesha, wewe ukimpa mtoto wa mtu mimba adhabu ya kukupa wewe ni kumwoa. Kwa sababu sasa wewe unapomkamata na kumfunga miaka 30 sasa atakayelea huyo mtoto ni nani? Kwa sababu baba amefungwa miaka 30, mama sasa amekuwa changudoa, mtoto lazima atakuwa mtoto wa mtaani. Kwa hiyo, wangepewa adhabu ya kuwaoa hata kama wawe Walimu, Wabunge, wawe Madaktari akishampa mtoto wa mtu mimba anamwoa. Kwa sababu siku hizi ni rahisi ni *DNA* inaonekana baba yake ndiyo huyu. Hiyo itasaida kuwapa *responsibility* wale watu wanaowapa watoto wa watu mimba wawatunze wale watoto. Lakini hii adhabu anayepewa mtu kwa kufungwa sana, inasababisha yule mtoto awe mtoto wa mtaani na tutakuwa tumeharibu ile familia moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho pia ningependa hii Wizara ikiangalie, kutokana na maadili mabovu, sisi tumekubali vitu ambavyo havifai. Tunasema kwamba katika kuzuia UKIMWI usiendelee kuwepo katika jamii yetu kupunguza watu wetu kuna njia tatu ambazo zimekuwa *recommended*. Njia ya kwanza wanasema ni *Abstain*, kuacha kabisa hii inaonekana ni ngumu sana. Njia ya pili kuwa na

mpenzi mmoja au mshirika mmoja, hii inaleta *sense* kwa sababu hata watu wa dini wanakubaliana na hii. Lakini mimi naungana na mashirika ya dini kusema ya kwamba kondomu tuingalie sana. Hiki kitu kimeletwa na wale wale ambao wanadai kwamba tumekuwa wengi sana kwa namna ya kutupunguza na hao ndiyo wanao- *encourage* kwamba tuwe na *Promiscuity* watu waone kwamba kitendo cha kujamiiana ni kitendo cha kawaida.

Kondomu sasa zipo mpaka vijijini. Ukizunguka hata mitaani ukiangalia macho yako chini kwenye mitaro ni kondomu tupu. Sasa uelewe kwamba ile kondomu maana yake ni kwamba ni jeneza, kuna watu mle ambao wanatupwa ovyo. Wengine wangekuwa Mawaziri, wengine Madaktari na Mainjinia, tunatupa watu ovyo na hii nadhani hata kwa Mungu ni mbaya sana. *(Makofi/Kicheko)*

Kama ni hivyo basi kwa sababu hatimaye wale ambao wana- UKIMWI watakufa na namuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kusema kwamba watu wote tupimwe. Ni kweli tujue kwamba ni idadi gani ya Watanzania ambao tayari imekuwa *affected*, hawa ndiyo walelewe, watunze na pia wapewe dawa za kurefusha maisha na pia waonyeshwe kwamba wasijamiiane na wengine. Nadhani ni mpango mzuri. Isiwe tu kwamba ni kupima tu ili tujifahamu wale ambao tunaumwa ili na wale ambao wapo sasa wawe *encouraged* kuoana na kuendeleza kizazi ili kisiishe. Kwa sababu kama wale ambao ni wagonjwa tayari watakuwa watakufa, wengine ambao ni wazima wanendelea kuua mbegu ndani ya kondomu sasa hatimaye hakutakuwa na watu katika hili taifa. Kwa hiyo, na hili pia tungeliangalia tuone kwamba litakuwa na madhara gani kwa baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikielekea mwishoni napenda kuzungumzia *NGOs*. Mimi sikubaliani kwamba *NGO* zipunguzwe, nadhani kuna *NGOs* ambazo zimefanya kazi nzuri sana hasa kuanzisha vituo vya watoto yatima. Kwa sababu inaonekana kwa mwenendo huu tunaoenda hatimaye watoto watalelewa kwenye vituo vya watoto yatima, wazazi wao hawatakuwepo na hiyo ni kazi nzuri ambayo inafanyika. Pamoja na kwamba kuna wengine ambao wanazo za mifukoni kwa ajili ya ufisadi lakini sidhani kama ni wote. Sasa hii Wizara iache kueneza sera za kunyanyapaa watu kwa sababu mpaka dakika hii hayo ma-*group* niliyoyazungumzia sidhani kwamba Wizara hii inatakwimu zake. Idadi ya watoto wa mitaani nadhani haieleweki. Idadi ya wazembe, wazururaji na wamachinga, vibaka na machangudoa sidhani hata hii Wizara imejitahidi kufahamu tuna watu wangapi ambao wanaishi katika mazingira magumu kama hayo pamoja na wazee wa mitaani ambao ni watu ambao wamestaafu lakini jamii imewakataa wanateseka mitaani. Basi ione namna ya kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa ningependa kuiomba Serikali iongeze Bajeti katika Wizara hii kwa sababu hii ndiyo Wizara yenye watu. Tanzania ni watu na Mwalimu Nyerere alisema kwamba ili nchi iendelee alitaja kitu cha kwanza ni watu halafu ardhi na sasa tusitoe ardhi yote. Mheshimiwa mmoja amesema kwamba hata vijijini sasa ardhi inauzwa ovyo watu hawatakuwa na mahali pa kukaa. Kwa hiyo, tutunze watu, tutunze ardhi ili Tanzania ije kuwepo hata mwaka 3000 vinginevyo kwa mwenendo huu watu watakwisha kwa UKIMWI. Watu watakwisha kwa njaa na vilevile hao wanaokuja sasa kutoka nchi nyingine ndiyo watakaokaa katika nchi hii kwa sababu Watanzania hawatakuwepo. Mimi ushauri wangu ni huo na naomba wananchi wote na vilevile Serikali izingatie. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chacha leo umejitahidi kweli kutoa kali. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge kwa sababu hii ni hoja ya Kamati sasa nitawaita Mawaziri ambao Wizara zao Kamati hii inafanya nao kazi. Kwa hiyo, itakuwa Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Ndiyo maana nilikuwa nauliza unaposema Wizara hii ipi kwa sababu hii Kamati inafanya kazi na Wizara tatu, moja ikiwa hii ya Jinsi na watoto. Kwa hiyo, na hawa Mawaziri watapewa dakika kumi na tano kila mmoja na mtoa hoja atapewa dakika thelathini. Sasa nitamwita Waziri wa Habari wa Habari, Utamaduni na Michezo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA) :** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kutoa ufafanuzi wa taarifa nzuri iliyotolewa na Kamati ya Maendeleo ya Jamii na Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Jenista Mhagama Mbunge. Kabla sijatoa ufafanuzi na mimi naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Korogwe na mimi mwenyewe binafsi na familia

yangu kutoa rambirambi kwa kifo cha Mbunge mwenzetu na Naibu Waziri mwenzetu Marehemu Salome Mbatia. Kwa kweli ni pigo kubwa tunamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Baada kutoa rambirambi hizo naomba na mimi nichukue nafasi hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa mafanikio makubwa na Mkutano Mkubwa ambao umefanyika kidemokrasia katika kijiji cha Kizota. Naomba nipongeze na niwapongeze wote walioshinda kuanzia Mwenyekiti wetu na wajumbe wote. Kipekee nikupongeze wewe Mheshimiwa Naibu Spika,kwa kuwa Mjumbe wa *NEC* na kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichukue nafasi hii sasa kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, kuipongeza Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Nampongeza Mwenyekiti na naipongeza Kamati yote kwa ujumla kwa taarifa nzuri sana ambayo wametuletea hapa Bungeni. Hongereni sana. Lakini kikubwa ambacho naomba niseme kwa niaba ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ni jinsi ambavyo tumefanya kazi kwa karibu sana. Nataka niwapongeze kwa ushirikiano wenu, sisi kama Wizara tumejisikia kwa mchango na ushauri wenu ulikuwa wa hali ya juu sana na nitamke wazi kabisa kwamba ushauri wenu umefanya Wizara yetu ifanye kazi na ijitume na tuweze kubadilika katika utendaji wetu. Hongereni kwa hilo. Yapo masuala ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia sekta mbalimbali katika Wizara yetu, nitayazungumza kwa kifupi. Mheshimiwa Hafidh Ali yeye alikuwa na hoja tatu. Kwanza, aliipongeza Wizara yetu kwa maana ya Serikali kujenga uwanja mpya, lakini la pili alitaka elimu itolewe kwa wananchi wanaoingia kwenye uwanja huu mpya kwa jinsi ambavyo kumetokea uharibifu wa hali ya juu sana, hasa katika mechi ya Taifa *Stars* na *Cranes* ya Uganda. Vyoo viliharibika, zaidi ya viti 300 viling’olewa na wengine walijisaidia juu ya vyoo na vitu vingi ambavyo vilijitokeza vya ajabu ajabu na akasema basi Wizara ifanye utaratibu wa kutoa elimu kwa umma kwa wanaoimgia kiwanjani. Lingine ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Hafidh ni kwamba kuwe na mkakati wa mafunzo ya sheria mbalimbali za michezo kwa maana ya michezo yote kuanzia shuleni, waandishi wa habari, wachezaji wenyewe hasa wa timu ya taifa, vijana pamoja na wananchi kwa ujumla. Nashukuru kwa mchango wake, ulikuwa mzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na hilo la kwanza ni kwamba Serikali imepokea pongezi kwa uwanja na tunashukuru kwa sababu ni kwa faida ya wote kwa sababu ni kodi yetu na tunaendelea sasa hivi kutafuta fedha kumaliza *phase two* utakapofika mwaka 2009. Lakini kubwa niseme tu kwamba hiki ni kiwanja ambacho kinatambuliwa na *FIFA* na *IAAF* na kinaweza kutusaidia hata kupata michezo ambayo inachezwa kwa kombe la dunia kwa timu kufanya mazoezi. Kwa hiyo, ni jambo la kujivunia na kupongeza sana. Lakini lingine kubwa ambalo Mheshimiwa Hafidh Ali amelizungumzia ni hili ambalo alisema baada ya kubainika uharibifu mkubwa uliotokea ndani ya uwanja mpya kufuatia mchezo wa majaribio kati ya timu ya Taifa na Uganda, Serikali imeliona hili, tukafanya kazi kubwa zaidi kabla ya mchezo dhidi ya Msumbuji. Kwa wale ambao walikuwa wanatazama runinga, Mkurugenzi wetu wa Maendeleo ya Michezo Nchini, Ndugu Henry Ramadhan, tuliweka utaratibu wa kupata vipindi kwenye *TV* na tukapata nafasi kwenye gazeti na kwenye *Radio*. Tulifanya mambo matano, cha kwanza ni namna ya kuingia kiwanjani na matumizi ya vifaa vilivyomo, somo lilikuwa linatolewa kwenye *TV* na Mkurugenzi mlikuwa mnamwona anapita. Lakini pili, mtazamaji alikuwa anatakiwa kuingia mlango upi kulingana na tiketi yake, kama ni shilingi 20,000/= au 40,000/= uingilie wapi, alikuwa anatoa maelezo hayo. Tatu , jukwaa analostahili kukaa wakati ameingia akae wapi, alielekezwa aende wapi. Lakini kingine ni matumizi ya vyoo alikuwa anatoa *demonstration* namna ya kutumia choo. Kwa sababu tumekuta wengine wamesimama juu ya choo ambacho unatakiwa ukae lakini mtu kasimama.Tano, ni jinsi ya kutoka nje ya uwanja mara baada ya mchezo wenyewe kwamba aende mlango gani na geti gani. Lakini lingine ni namna ya kuegesha magari yanaoingia kiwanjani. Hii ni elimu ambayo tutaendelea kuitoa ili angalau uharibifu usitokee. Nafurahi kusema mechi dhidi ya Msumbiji, uharibifu huo ulipungua sana baada ya elimu ile kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo Mheshimiwa Hafidh alizungumzia ni Sheria za michezo. Nakubaliana na yeye kabisa kwamba mchezo wowote duniani kwanza namba moja ujue sheria. Hili tunalifanyia mkakati Baraza la Michezo kwa kushirikiana na vyama vya michezo. Tuna masomo maalumu yatatolewa timu zitakapokuwa kwenye mafunzo iwe timu ya vijana anatolewa mtaalamu kama vile Hafidh ambaye ni mtaalamu wa Kimataifa kwenda pale kufundisha timu ile. Tutafanya utaratibu huo na pia katika silabasi ambayo Wizara ya Elimu wanaitoa kwa elimu ya michezo kuanzia darasa la kwanza na kuendelea, somo la sheria za michezo ni soma mojawapo. Kwa hiyo, mtoto ataanza kupata kujua sheria

akiwa mtoto mdogo mpaka akiwa anacheza mchezo akiwa kiwanjani. Tunaandaa utaratibu wa Watangazaji kama ulivyosema wewe mwenyewe pamoja na waandishi wa habari kupata mafunzo ya sheria. Kwa sababu wanaoanza kusema ni goli au ni *off side* kumbe si *off side*. Tunafanya hivyo pia kwa watazamaji. Kwa hiyo, hivyo ndivyo jinsi ambavyo tumejikita kwenye hilo.

Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o alizungumza mambo mawili. Mfuko wa Utamaduni ufufue utamaduni wa asili. Lakini pia akazungumzia utamaduni ule wa zamani wa wazee wetu kutoa hadithi zenye maadili mema ufufuliwe. Nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, Mfuko wa Utamaduni ulianzishwa mwaka 1998 kwa lengo la kuhamasisha na kuchochea kukua kwa fani ya utamaduni. Baadhi ya kazi zake ni kufufua utamaduni wa asili na kufanya utafiti wa mila na desturi za Kitanzania na kiafrika kwa ujumla. Nataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba terehe 11 siku ya Jumapili, Mfuko wa Utamaduni utatoa semina kwa Wabunge wote kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa hiyo, wote tuhudhurie ili tupate mengi zaidi ambayo amezungumza Mheshimiwa Mama Mng'ong'o. Tutapata maelekezo zaidi na ile ni semina, kwa hiyo, tutapata nafasi ya kuuliza maswali mengi. Nampongeza kwa mchango wake huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo alitoa hoja mbili pia. Anakumbushia Serikali kurudisha michezo mashuleni, anataka wachezaji wa zamani Serikali iwatambue, wapate mafunzo na wafundishe watoto. Ni suala zuri, nataka nimhakikishie kabisa kwamba, kwa upande wa Serikali kurudisha michezo mashuleni, hili tayari Serikali imekwishatamka na kama mnakumbuka ametamka mwenyewe Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Margret Sitta. Kwa bahati nzuri, nataka niwahakikishie kabisa Waheshimiwa Wabunge kwamba tayari mikakati ya kuanzisha mashindano hayo imekwishaanza. Mwaka huu tutaanza Desemba na mwaka ujao tutaanza *full swing*. Kwa hiyo, tunarudisha mashindano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na hili alilozungumza, tayari utaratibu wa kuwatafuta wachezaji wa zamani ambao tunajua ni hazina na uzoefu, tunawaandaa na kuwafundisha ili wao sasa ndiyo wawe makocha kama wenzetu wa nchi nyingine wanavyofanya duniani kwa sababu tunaamini kabisa, mchezaji wa siku nyingi atakuwa amepitia mafunzo ya muda mrefu na ana uzoefu wa kutosha na amefanya semina nyingi, badala ya kutumia vijana wadogo wadogo hawa. Huu ni utaratibu ambao tunauandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba alikuwa na hoja moja kubwa, alisema kwamba alitaka kufahamu utendaji wa Baraza la Michezo la Taifa ukoje, mbona haoni utendaji wa BMT Mikoani na Wilayani? Hili ni suala nyeti na ni zito.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaelimishe tu Waheshimiwa Wabunge kuwa Baraza la Michezo limetungwa kisheria na Bunge lenu hili. Baraza la Michezo limetungwa mwaka 1967 kwa Sheria Na. 12, likarekebishwa mwaka 1970. Lakini lengo kubwa la Baraza la Michezo ni kusimamia na kuendeleza michezo nchini kwa *levels* zote. Katika ngazi ya Taifa, Baraza la Michezo linaundwa na Waziri mwenye dhamana ya michezo na yeye ndiye anateua wajumbe wasiozidi 29. Kuna wengine anawateua kutokana na nafasi zao kama vile Katibu wa baadhi ya vyama, mfano *TFF, BATA (Basketball, Volleyball, Netball)*, wanaingia kwa nafasi zao.

Wengine anawateua kutokana na uzoefu anaofahamu yeye na Mwenyekiti pia anamteua yeye. Katibu wa Baraza la Michezo, anaajiriwa na Baraza kwa sifa kwa kutangaza kwenye gazeti. Katika ngazi ya mkoa, Kamati ya Maendeleo ya Michezo ya Mkoa ndiyo yenye jukumu la kufanya kazi za Baraza. Baraza la Michezo la Mkoa linateuliwa na Mkuu wa Mkoa na Mwenyekiti ni Afisa Tawala wa Mkoa, Katibu wake ni Afisa wa Michezo anayeishi katika Wilaya ya Makao Makuu ya Mkoa na wataalamu wengine. Vivyo hivyo kwenye Wilaya, Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Wilaya ni Afisa Tawala wa Wilaya na yeye anateuliwa na Mkuu wa Wilaya na Katibu wake ni Afisa Michezo wa Wilaya ile.

Majukumu yao ni yale yale ambayo yako kwenye Baraza la Michezo la Taifa. Tatizo tunalolipata hapa na Mheshimiwa Killimbah alikuwa amezungumza haki kabisa na yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, ni kwamba huko Wilayani na Mikoani, michezo haiendi. Haiendi kwa sababu hizi Kamati hazifanyi kazi yake ipasavyo na hata Mabaraza ya Madiwani katika Wilaya zetu, hawatengi hata fedha za

michezo. Kwa hiyo, unakuta michezo katika Wilaya, Michezo katika Mkoa haiendi, lakini iko Kamati, yuko Mkurugenzi, yuko *RAS*, yuko *DAS* na Kamati nzima ambao kazi yao ni hiyo kama ambavyo Baraza la Taifa linafanya. Kwa hiyo, napenda kutoa wito hapa kwamba tubadilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru Waziri Mkuu kwa sababu Bunge lililopita aliwaita Wakuu wa Mikoa wote, akakaa nao na sisi tukaandaa *paper* ya namna ya kuendeleza michezo katika nchi hii. Tukakaa, tukajadiliana, tukawaambia Wakuu wa Mikoa watusaidie tuone namna gani ya kusogeza michezo katika nchi yetu. Kwa hiyo, naamini kabisa michezo itasogea kwa jinsi ambavyo tunakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Kijiko, Mheshimiwa Ruth Msafiri, wamezungumzia hoja nzito ya viwanja. Huwezi kucheza mchezo bila viwanja! Tunalo tatizo hili na ni tatizo sugu, ni kweli. Shule inaanzishwa, hakuna kiwanja. Sasa hivi tumesema kila Kata iwe na *Secondary School*, hakuna viwanja. Sheria na Kanuni kwa wenzetu wa Serikali za Mitaa, Maofisa Mipango miji, Serikali za Vijiji, Kijiji kinapoanzishwa lazima kiwe na viwanja vya michezo. Ni muhimu kutambua hili, lakini unakuta viwanja havipo katika maeneo na watu hawajali kuviweka, matokeo yake ni kwamba watoto wanacheza barabarani, hawana sehemu za kucheza.

Nataka niwapongeze Waheshimiwa hawa ambao wamezungumza hili, ni kwamba ni kweli lazima tuwe na viwanja. Napenda kutoa wito, Serikali za Vijiji, lazima tutenge viwanja vya michezo. Shule inapoanzishwa, lazima kuwe na viwanja vya michezo, huwezi kuwa na shule haina kiwanja cha michezo, watoto hawana mahali pa kucheza, matokeo yake wanakwenda wanafanya vitu ambavyo havipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niyaseme haya machache, yako mengi lakini nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na nashukuru Kamati kwa jinsi ambavyo wametoa taarifa yao hapa. Asanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Na yale msiyojibu, mtayatumia kwa utekelezaji, siyo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza niungane na wenzangu katika kutoa pole kwa ndugu na jamaa na marafiki wa Marehemu Salome Mbatia kufuatia kifo chake. Lakini pia niungane nanyi katika kumtakia heri na kupona haraka Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, rafiki yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

Vilevile niungane nanyi katika kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, dada yangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kutoa vizuri ripoti yake na vilevile niwapongeze wajumbe wa Kamati hiyo kwa kufanya kazi vizuri na kushirikiana nasi vizuri. Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitumie nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa mjumbe wa *NEC* na mjumbe wa Kamati Kuu wewe na viongozi wengine wa Chama waliochaguliwa katika kipindi hiki kilichomalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, sasa kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja hasa zilizojitokeza katika Taarifa ya Kazi za Kamati. Kwanza hoja ya madeni ya *NSSF*. Naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba *NSSF* ilitambua tatizo la madeni sugu na kwa kutambua hivyo, mwaka mmoja uliopita iliunda kitengo maalumu cha kufuatilia madeni. Kitengo hicho kinafanya kazi zake vizuri sana. Kwa kipindi cha mwaka mmoja kimeweza kukusanya zaidi ya shilingi milioni 900 kati ya shilingi bilioni 4 na sasa hivi deni lililobaki ni shilingi bilioni 3.1 na kazi inaendelea kwa kasi kuendelea kufuatilia, kuhakikisha deni lote linapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kulikuwa na hoja ya wanachama wa *NSSF* kuweza kukopeshwa kutokana na michango wanayoitoa. Kwa sasa sheria haziruhusu, lakini tumeichukua hii hoja kwa uzito maalumu na tutaiingiza katika mchakato wa mjadala wa sheria mpya za Hifadhi ya Jamii kuona kwamba tunaweza kufanya nini katika kuona jambo hili linaweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kuhusu mradi wa nyumba za bei nafuu ambapo Kamati imeona na Wabunge wengi wameona ni muhimu mradi huu kwa kuwa ni mzuri, usambazwe katika mikoa mbalimbali. Tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba jambo hili ni jema na tayari *NSSF* imekwishaanza kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba mradi huu unasambazwa nchi nzima na kwa sasa tayari viwanja vimepatikana Shinyanga, Mwanza wanaendelea kupima na tutaendea kufanya hivi hatua kwa hatua kuona kwamba kadri inavyowezekana tufikie eneo kubwa zaidi la nchi kwa sababu *NSSF* ni Shirika la Kitaifa, siyo la sehemu moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile niongelee hoja iliyojitokeza kuhusu ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Hatua tuliyofikia kwa sasa si mbaya. Waraka wa Baraza la Mawaziri tayari ulishafikishwa kwenye Kamati ya Baraza la Mawaziri *(IMTC)*. *NSSF* imeagizwa kushirikiana na mwekezaji binafsi. Sasa hivi hadidu za rejea za namna ya kumpata mwekezaji zinakamilishwa na baada ya hapo akipatikana mbia wa kushirikiana na *NSSF*, kazi hiyo itaanza mara moja. Kwa hiyo, tunataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba jambo hili tunalipa uzito wa kutosha, tunatambua umuhimu wake kwa Taifa na umuhimu wake kwa maendeleo ya Dar es salaam na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imejitokeza ni kuhusu kupunguzwa kwa riba katika mikopo inayotolewa. Naomba niseme kwa sasa kwa utaratibu wa kiuchumi, mambo ya riba yanategemea sana nguvu ya soko na riba ambayo ipo katika mikopo hii ya fedha za uwezeshaji. Ni asilimia 10 ambayo tunaamini kwa sasa ni kiwango kidogo, isipokuwa ile michache ambayo inakwenda kwenye *SACCOS* ambayo kuna asilimia chache inaongezwa.

Kwa hiyo, tunadhani kwa sasa tunakwenda vizuri na kiwango hiki cha riba huku tukiendelea kutafakari namna bora zaidi ya kuboresha ili watu waweze kukopa na kufanikiwa zaidi. Hoja ya elimu ni nzito na katika hii awamu ya pili ya mikopo ya uwezeshaji, tumeizingatia kikamilifu na tayari Taasisi zitakazohusika na mikopo hii zimepata mafunzo na zenyewe zimeelekezwa kutoa mafunzo ya kutosha kwa wakopaji. Kwa hiyo, jambo hili limezingatiwa na litapewa kipaumbele katika awamu hii inayofuata ya ukopeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kilio cha Kamati ya Maendeleo ya Jamii cha siku zote kimezingatiwa na hivyo *SCCULT* imeongezwa katika taasisi zitakazoshirikishwa katika kupata mikopo hii ili *SACCOS* zifikiwe kirahisi. Changamoto ya kuongeza wanachama wa *SACCOS* pia Serikali inakubaliana nayo na kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, umetengenezwa utaratibu unaitwa *Corporative Reform and Modernization Programme* ambayo itasaidia katika kuhamasisha uanzishaji wa *SACCOS* endelevu. Naomba tuwahakikishie kwamba tutashirikiana nanyi kwa karibu kuona kwamba utaratibu huu unafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati imetaka mikakati ya kukuza ajira iimarishwe zaidi ili tuhakikishe kwamba lengo lililokusudiwa la ajira milioni 1 linafikiwa. Naomba niseme kwamba tunatoa kipaumbele cha kutosha kuhakikisha mikakati hii inaimarishwa vizuri zaidi. Tunaenda vizuri mpaka sasa hivi katika zoezi la kukuza ajira, zoezi la kuimarisha ajira, lakini tunataka kuimarisha zaidi na tumeelewana kwamba mkazo mkubwa tutauweka katika sekta ya kilimo, viwanda vidogo vidogo, barabara, uchimbaji madini na utalii kwa sababu tunaamini kwamba sekta hizi ndiyo msingi mkubwa wa utoaji wa ajira nyingi kama zinasimamiwa na kuendelezwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati iliongelea habari ya Kima cha Chini kwa sekta binafsi. Serikali imetoa tamko kwamba Kima cha Chini kianze tarehe 1 Januari, 2008. Mwanzo tulisema kianze mwezi wa 11 lakini tukagundua kwamba hatukuwapa nafasi ya kutosha waajiri kujiandaa na tukaona ni busara tuwape muda nao wajiandae. Kwa hiyo, zoezi hili litaanza Januari. Niwahakikishie tu kwamba tutakuwa tunafuatilia kwa karibu jambo hili kuona kwamba linatekelezwa kwa kufuata sheria na kwa kujali wafanyakazi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la ongezeko la ajira kwa wageni nchini, nataka niseme kwamba tatizo hili linachangiwa na mambo kadhaa. Ni kweli kwamba wageni ni wengi sasa hivi wanaofanya kazi ambazo zingeweza kufanywa na wazalendo, lakini ziko sababu zinazosababisha jambo hili. La kwanza, kuna wale wanaofanya udanganyifu mkubwa wakati wanaomba vibali vya kufanya kazi

nchini. Wanakuja nchini wakiomba kufanya kazi fulani, wakionyesha utaalamu wa kazi hizo. Ukweli ni kwamba wanapopata vibali hivyo hawafanyi kazi zilizokusudiwa. Lakini la pili, ni wale waliopata vibali vya muda mfupi vya kukaa nchini, wenyewe wanaita *business visa*, nao huwa wanatumia vibali hivyo vibaya kuliko ilivyokusudiwa. Pia kuna wale wanaofanya matumizi yasiyo sahihi ya vibali wanavyopewa na ni vigumu kwa mwananchi wa kawaida anayetoa taarifa kwa Serikali kujua ni aina gani ya kibali mtu huyu mgeni anafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tumejaribu kutafakari kama Serikali namna tunavyoweza kupunguza ukubwa wa tatizo hili. La kwanza, tumeunda Kamati ambayo inashirikisha Uhamiaji, Chama cha Waajiri, Chama cha Wafanyakazi *(TUCTA)* na Taasisi ya Uwekezaji Nchini *(TIC).* Kamati hii ndiyo inachambua namna ya kuwapa vibali wageni. Tumeweka Utatu wa namna hii wa kufanya kazi kwa pamoja ili kila mtu ajue nafasi yake kwa jamii. Kwa hiyo, taasisi hii inafanya kazi kwa pamoja, hakuna mtu anayepata kibali bila kupitia vyombo hivyo nilivyovitaja. Hii ni sehemu ya kujaribu kupunguza uwingi wa wageni hawa ambao hawana sababu ya kuwepo wakati Wazalendo wapo. Lakini pia tumeeunda Timu ya Ukaguzi ambayo tunaendelea kuiimarisha ambayo kwa vyovyote vile isipopata ushirikiano wa karibu wa wafanyakazi na wananchi, haitafanikiwa.

Kwa hiyo, nitoe changamoto ya kuwaomba Waheshimiwa Wabunge watusaidie kutoa ushirikiano kwa timu hii ya Ukaguzi. Vilevile tunaandaa marekebisho ya Sheria ya Ajira nchini ili Sheria hii itusaidie kuziba mianya ambayo ipo ambayo inafanya watu ambao wanafanya kazi za wazalendo, wasipate kazi. Kwa hiyo, tutaomba Waheshimiwa Wabunge Sheria hii itakapofika mbele yenu, basi mtupe ushirikiano wa kutosha ili ipite haraka na ianze kufanya kazi haraka. Vilevile tumeunda *Labour Exchange Centres* ambazo tutaziweka katika Kanda mbalimbali nchini ili ziwasaidie waajiri wa ndani kujua wazalendo wenye sifa wanapatikana wapi. Mpaka sasa Kanda hizo chache ambazo tumeziweka, zinafanya kazi zake vizuri na tutaendelea kuziimarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kuhusu *OSHA*. Kuhusu *OSHA*, Serikali imekwishachukua hatua za kutosha kujaribu kuiimarisha. Uchache wa wafanyakazi katika *OSHA* umefanyiwa kazi katika mwaka huu wa fedha. Tayari katika mahitaji ya wafanyakazi 40, tumeajiri wafanyakazi 28 kati ya mwezi Julai na sasa na kati yao 14 ni Wakaguzi. Kwa hiyo, tutaendelea kuchukua hatua za kuimarisha *OSHA* ili iweze kuwa na sifa na watumishi wanaofanana na majukumu ambayo *OSHA* inayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia hoja hizo kwa haraka haraka, naomba sasa nipitie baadhi ya michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo iligusia Wizara yetu. Kwanza, ni hoja ya Mheshimiwa Hafidh Ali. Mheshimiwa Hafidh Ali aliomba tuone uwezekano wa kupata walimu wa kufundisha *SACCOS* kule Zanzibar ili kasi iwe kubwa kwa Zanzibar kama ilivyo katika maeneo mengine. Naomba nimhakikishie kuwa ombi lake hilo tutalifikisha Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ili ishauriane na Wizara inayohusika Zanzibar kuona namna wanavyoweza kusaidiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Vita Kawawa alitaka *SACCOS* za Namtumbo zipewe mikopo yao moja kwa moja. Naomba niseme katika awamu hii ya pili tunayoishughulikia tutafuatilia kwa karibu tuone namna ambavyo Namtumbo inafikiwa kwa urahisi na kwa namna ambayo ni bora zaidi. Mheshimiwa Lediana Mng’ong’o yeye alitaka fedha za mikopo za vijana ambazo zinatoka Wizarani ziende kwenye *SACCCOS* ya vijana. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tulikwishafanya uamuzi na katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri mwezi wa Nane alisema kwamba kuanzia sasa fedha za vijana zinazopitia Wizarani, zitapitia kwenye *SACCOS* za vijana. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge watusaidie kuendelea kuwahamasisha vijana kujiunga katika vyama vya kuweka na kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ezekiel Maige, yeye aliongelea suala la kushusha riba kwa *SACCOS* kwa *CRDB* na *NMB*. Nasema Serikali itaendelea na mazungumzo na *BoT* na hizi Benki kuona namna ya kufanya. Hatua tuliyopiga si mbaya kwa sababu hata mwanzo tulipoanza mazungumzo, riba haikuwa ya asilimia 10.

Tumefanya mazungumzo kwa muda mrefu, tumeshuka kutoka zaidi ya asilimia 16 mpaka tukafika hapo. *NMB* na *CRDB* zinaposhughulika na utaratibu ambao si wa uwezeshaji, riba zake ni zaidi ya mara mbili ya riba ya kawaida. Kwa hiyo, hatua si ndogo maana kuna wengine wanasikitika kweli, wanasema, "jamani hii mikopo ina faidia gani? Riba inaongezeka pale mpaka inafika asilimia 13". Sasa nasema ni kwa sababu tu hawajapata taarifa kwamba kwa mfano mikopo ya *NMB* ile ya kawaida ambayo si ya uwezeshaji, riba yake ni asilimia 2 kwa mwezi ambayo maana yake mwaka inafika asilimia 24. Kwa hiyo, kuwa na asilimia 13 au 12 bado tumepiga hatua ambayo tunapaswa kupongezana kwa kazi hiyo tunayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya viwango vya maslahi kwa wageni, naomba niseme tu kwamba kwa sasa bado kama Serikali tunashughulikia kima cha chini, mambo mengine haya tutaendelea kuyazungumza kuona namna tunavyoweza kuyafanya. Lakini hatujaweka bado utaratibu ambao tunaenda kwenye sekta binafsi kupanga viwango vya kila mtu alipwe kiasi gani. Na sina hakika kama kuna nchi ambayo imeanza kufanya hivyo. Lakini tutatafuta *modality*, tutatafuta njia bora ya kuona namna ya kulichukua jambo hili na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kutokopeshwa *SACCOS* mpya, hii inanipa tabu kidogo. Inanipa tabu kwa sababu kanuni tu za kibenki hazikubali jambo hili kwamba leo uanzishe *SACCOS*, kesho upate mkopo. Nakumbuka siku moja alikuja kunitembelea ndugu yangu mmoja pale Dar es Salaam, akaniambia: "Bwana, sasa Mjomba hebu nisaidie nimekwishaanzisha *SACCOS* na wanangu 6 tupate mkopo mara moja, unajua hii habari iwasaidie wadogo zako". Lakini sasa utaratibu huu mgumu sana, wewe unaanza *SACCOS* leo, kesho unataka mkopo. Sasa nilipata tabu, nadhani na hili linawapa tabu na watu wa Benki. Naomba na sisi tujaribu kulielewa tu kwamba watu wakijenga kwanza uwezo wa kuweka akiba wao wenyewe, wakaweza kukopeshana wao wenyewe, itasaidia kufanya Benki ziweze kuwaamini na mikopo hii iwe endelevu, ama sivyo mikopo hii itaishia kuitwa sadaka za JK badala ya mikopo ya Serikali ya uwezeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie suala la Mheshimiwa Magdalena Sakaya kuhusu kuzingatiwa kwa viwango vya mishahara. Tutaendelea kuzingatia mara kwa mara. Hii mishahara ya sekta binafsi tumeanza kwa mara ya kwanza mwaka huu na tutafanya hivyo kila mwaka. Lakini pia habari ya waajiri kutisha wafanyakazi ni kinyume cha sheria. Tutafuatilia kwa karibu kuona kwamba wafanyakazi wanafanya kazi katika mazingra mazuri yasiyo na vitisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mushashu alitaka kujua awamu ya pili inaanza lini. Naomba nilijulishe Bunge lako kwamba maandalizi yote yamekamilika ila tu siwezi kusema wanaanza kesho asubuhi. Watakapokuwa tu tayari, wataanza. Lakini maandalizi yote ya msingi yamekamilika, tuko tayari kuanza, tunaomba tu mvute subira kidogo, itakamilika. Halafu Mheshimiwa Msindai aliongelea mishahara midogo kwa watumishi wa ndani. Katika nyongeza ya mishahara mipya ya kima cha chini tumeizingatia na kwa mara ya kwanza watumishi wa ndani nao wana kima cha chini cha mishahara yao na tutaendelea kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Susan Lyimo, yeye aliongelea umuhimu wa kumarisha miundombinu ya kilimo ili kukuza ajira. Tunakubaliana naye moja kwa moja kwa sababu hii hoja ni ya msingi na ya kweli, tutashirikiana kuhakikisha kwamba inatekelezwa. Mheshimiwa Felix Kijiko yeye alihangaika sana na habari ya wageni haramu. Naomba nikiri kwamba Serikali pia inakerwa na wageni wa namna hii na Mheshimiwa Kijiko alisema wanaowakaribisha wako humu humu. Naomba nilithibitishie Bunge lako kwamba humu hakuna anayekaribisha wageni haramu, lakini wanakuja wenyewe kwa taratibu haramu. Tutaendedelea kuchukua hatua za kuhakikisha tunadhibiti jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rosemary Kirigini aliongelea habari ya kupenda kuajiri wageni. Naomba na lenyewe liwe katika majibu yale ya msingi kwamba tutaendelea kuchukua hatua ya kupunguza ajira kwa wageni. Mheshimiwa Ruth Msafiri, yeye aliongelea habari ya kuangalia upya riba na watu kuumia kazini na kiwango cha kima cha chini. Niseme hoja zake zote tumezichukua kikamilifu na tutazifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba tena niwashukuru sana kwa kunisikiliza, asanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa, nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ili aweze kujibu hoja za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – MHE. DR. BATILDA S. BURIAN (k.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO):** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nianze kwanza kwa kutoa rambi rambi zangu na kuendelea kuwaombea familia ya mwenzetu aliyetutoka, Mwenyezi Mungu awajalie moyo wa subira na aweze kulaza roho ya marehemu wetu Salome Mbatia, mahali pema peponi, *Amin*! Pia nizidi kumwombea Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Sophia Simba ili aweze kupona haraka na aweze kujiunga nasi katika shughuli za kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba basi, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwanza nianze kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Natoa pongezi hizi kwa Kamati na wajumbe wote wa Kamati hii. Adha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia taarifa hii na ambayo kwa kweli imetoa mchango mkubwa sana ambao tutaupeleka katika Wizara na tunaahidi kwamba utaweza kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia tunaweza tukaigawa katika maeneo manne. Kwanza, kulikuwa na suala zima la ufinyu wa bajeti ya Wizara hii. Lakini vilevile, Waheshimiwa Wabunge walizungumzia suala zima la kuboresha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa maana ya kuboresha maeneo ya Vyuo vile na upungufu wa vifaa na vitendea kazi pamoja na kuwa na Wakufunzi na Walimu wa kutosha. Lakini pia kulikuwa na suala la uratibu wa shughuli nzima za *NGO*s. Na lingine ambalo wamelizungumzia wengi kwa kina sana ni suala la watoto yatima, jinsi gani Wizara na Serikali kwa ujumla inashughulikia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii bado ni finyu. Lakini ni vizuri pia tukakumbuka kwamba wapi tumetoka. Bajeti hii kama tutakumbuka mwaka 2004/2005 ilikuwa ni shilingi bilioni 4.9. Lakini Serikali imeendelea kupandisha bajeti hii kutokana na kupatikana kwa mapato katika Mfuko wa Serikali na hata kufikia shilingi bilioni 11 mwaka huu. Kwa hiyo, tumekuwa tukipandisha bajeti hii. Mwaka 2005/2006 ilikuwa shilingi bilioni 8.4, mwaka 2006/2007 ilikuwa ni shilingi bilioni 10.4 na mwaka huu katika bajeti tuliyopitisha ni shilingi bilioni 10.9, yaani karibu na shilingi bilioni 11. Lakini bado tunakiri kwamba bajeti hii bado ni ndogo kutokana na ukubwa wa kazi nzima ambayo Wizara hii inataka kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikiri na kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika suala hili zima la kushawishi na kuhamasisha bajeti iweze kuongezeka ambao ni pamoja na Mheshimiwa Killimbah, Mheshimiwa Bernadeta Mshashu, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Msindai, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Chacha Wangwe. Wote hawa na wengine ambao sijawataja, wameweza kuzungumza kwa kina jinsi gani tunahitaji kuongeza bajeti hii. Lakini pia niweze kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, pamoja na bajeti hii ambayo imetengwa katika Wizara, bado kama Serikali tunatambua nafasi ya Wizara hii katika shughuli zingine katika sekta zingine na ndiyo maana katika mkakati ule wa kuboresha mazingira tumetengewa shilingi milioni 100 kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya jamii. Kwa hiyo, Wizara inaweza ikatumia kiasi kile kutoka katika sekta ile ya mazingira lakini pia tumeongea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na wenyewe pia katika shughuli za upimaji wa Vijiji, tumeomba Wizara hii ipatiwe fedha kwa ajili ya kushughulikia suala hilo. Kwa hiyo, tunafanya kila jitihada na napenda niwahakikishie kwamba kilio chenu tutakifikisha Serikalini na Serikali tunajua umuhimu wa Wizara hii, tutaendelea kuongeza bajeti kila hali inavyoruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililozungumziwa ni suala la jitihada za kuboresha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Waliochangia katika suala hili ni Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Msindai, Mheshimiwa Chaurembo na wengine wengi ambao sijawataja hapa. Lakini kwa ujumla lengo zima ni kuhakikisha kwamba kwa kweli vyuo hivi vinaleta tija iliyokusudiwa. Mimi nasema changamoto hii tunaichukua na niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi Wizara ina mpango wa kimkakati. Ina mpango wake wa kimakakati wa miaka 10 na kupitia mpango ule kuna miradi na programu mbalimbali ambazo zitatekelezwa. Kwa hiyo, tunawahakikishia masuala ya Vyuo hivi yataboreshwa ikiwa ni pamoja na kupata walimu na kuweza kutoa

upungufu wa watumishi ambao Mheshimiwa Msindai kwa kweli amezungumzia kwa kina kwamba Wizara ifanye kila jitihada tuweze kupata watumishi wa kutosha pamoja na Mheshimiwa Ruth Msafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda Waheshimiwa Wabunge wajue, ni suala zima la ubunifu. Tumepita katika baadhi ya Vyuo hivi, Vyuo ambavyo vimekuwa na Wakuu wa Vyuo wabunifu, tumeona matokeo yake. Naweza nikatoa mfano wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Singida. Chuo kile kutokana na ubunifu wa Mkuu wa Chuo wameweza kuwa na uhusiano na vyama rafiki Sweden na wakaweza kujengewa Bwalo kubwa ambalo ni sawa na ukumbi wa mikutano kwa ajili ya vyakula lakini pia hata ukitumika kwa ajili ya mikutano na hata kusomea. Lakini pia wameweza kupata *facility* ya *computer* na kuweza kutumia kwa ajili ya Chuo kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo kingine ni cha Monduli. Kutokana na ubunifu pia wa Mkuu wa Chuo, wameweza kupata misaada mbalimbali na kufanya vitu mbalimbali ambavyo Vyuo vingine vimeshindwa. Naomba niwahamasishe na tuweze kuwahakikishia kwamba wale Wakuu wa Vyuo ambao watashindwa kwenda na kasi ya ubunifu na kwenda na mambo ya kisasa itabidi waachie ngazi ili tuweze kupata watu ambao wataweza kufanya kazi katika mazingira ambayo ni ya ubunifu na siyo *business as usually*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lililozungumziwa pia ni kuhusu kama Wizara inashindwa kuendesha hivi vyuo basi viende Wizara ya Elimu kupitia programu yake ya VETA. Mimi naomba niseme tu kwamba umuhimu wa Vyuo hivi vya maendeleo ya jamii wote tunajua pamoja na stadi hizi za kazi, lakini pia inatoa mafunzo maalumu kwa ajili ya kuhamasisha shughuli nzima za kujenga Taifa.

Kwa hiyo, kama tutasema kwamba vyuo hivi viwe tu kwa ajili ya stadi za kazi, tutapoteza dhana nzima ya ushawishi ya kuhamasisha masuala mazima ya kujitolea na kufanya hiari katika kujenga taifa. Tunachoweza kusema ni kwamba tutazidi kushirikiana na vyuo hivi vya VETA na sasa hivi kuna mkakati ambao kupitia VETA ambao ndiyo waratibu wa shughuli zote za mafunzo ya ufundi wanapata misaada ambayo kupitia misaada ile wanazigawa katika Vyuo vyote ikiwa ni pamoja na vyuo hivi vya maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna utaratibu sasa hivi wa wanafunzi hao kufanya mitihani ambayo inatoka *VETA* na wakishinda basi wanapewa vyeti vile vya *VETA*, kwa hiyo mambo yote hayo yanaaangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la majumba au kumbi zile za maendeleo (*Community Development Centres)* amezingumzia Mheshimiwa Msindai na Waheshimiwa wengine walizungumzia pale asubuhi. Ni kweli kabisa kumbi hizi za maendeleo ambapo ni *community centres* zilikuwepo zamani na zilikuwa zinafanya kazi nzuri sana. Sisi kama Wizara tayari tumekwishawaandikia halmashauri kuweza kuzirudisha kumbi zile ambazo zilikuwa zinafanya shughuli zile kwa ajili ya shughuli iliyokusudiwa, bado wengine wametekeleza wengine hawajatekeleza. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tukahamasishe Halmashauri zetu tukapata huduma hii na kuwe na maeneo kama haya ambayo yanaweza kuleta chachu kwa kukutanisha watu, kufanya warsha mabalimbali lakini pia hata kufanya mafunzo na kuleta maendeleo yanayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunapozungumza masuala ya ukeketaji, masuala ya unyanyasaji wa watoto, ubakaji wa watoto wadogo, ni kumbi hizi za *Community Centres*, ndiyo zinazoweza kutumika kutoa elimu, kuhamasisha, kuleta ustaarabu kuwafanya watu wakaweza kuelewa mambo ya msingi kabisa ambayo yanatakiwa wananchi wajue katika maeneo yao.

Maeneo haya ni muhimu sana na yanaendana na dhima nzima ya kuwa na halmashauri au jiji zinazokuwa na *facilities* zote zinazotakiwa. Jiji bila ya kuwa na *Community Hall*, kuwa na jumba lao la kufanya mikutano, au jiji bila kuwa na *community centres* haikamiliki. Kwa hiyo, mimi nawaomba tupitie mikutano yote ya *council* tuweze tukahamasisha kuhakikisha kwamba hizi *community centres* zinarudi na zinafanya kazi zile ambazo zilikusudiwa toka awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Benelith Mahenge, Mheshimiwa Kijiko, Mheshimiwa Suzan, walizungumzia suala zima la umuhimu wa upatikananji wa takwimu kwa ajili ya watoto yatima na hii pia ni pamoja na Mheshimiwa Chacha Wangwe. Niseme tu kwamba Wizara inashirikiana sasa hivi na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kuweza kuhakikisha kwamba takwimu zinaratibiwa na kuweza kupata takwimu katika vituo vile vinavyolelea watoto. Suala hili linashughulikiwa kwa umuhimu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine linalozungumziwa ni uratibu wa shughuli nzima za *NGOs*, niwaeleze tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kitengo hiki cha uratibu wa shughuli za mashirika yasiyo ya kiserikali kilipotoka Ofisi ya Makamu wa Rais na kupelekwa katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, kimeanza kwa kuweza kuainisha mashirika yale ambayo yalikuwa yamesajiliwa na kuyataka yasajiliwe upya kupitia kitengo hiki cha uratibu.

Kupitia usajili huu kitengo hiki kinapima utendaji wa hizi *NGOs*. Tutafuatilia kwa karibu, lakini pia kuna hii mitandao ya mikoa ambapo tunatumia mitandao ile kuweza kuhakikisha kwamba wanajua *NGOs* zilizopo katika mikoa yao na tuwafuatilie tuweze kuona zile ambazo ni za mfukoni tukazibana na tukazifuatilia shughuli zao na wakakosa usajili na kufutiwa *NGOs* zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala jingine la usalama wa watoto. Mheshimiwa Suzan Lyimo amelizungumzia hili na Waheshimiwa wengine, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Rose Mary Kirigini, lakini niseme tu kwamba hili kwa kweli tunalifuatilia na Wizara sasa hivi inalifuatilia kwa karibu kwa sababu kuna mifano mingi tumeona matatizo na tutakwenda tukijua kwamba suala hili la kuhakikisha haki na usalama wa watoto unazingatiwa.

Kulikuwa kuna hoja pia je, Serikali inaweza kuangalia sasa uwezekano wa watoto wa kike kuanza shule wakiwa na miaka mitano. Niseme tu kwamba wazo hili lilikuja toka mwaka 1998 kupitia programme ya *ESDP* wakati tunatayarisha *MMEM* na kwa pale tulikuwa tunafikiria kwamba ni kweli tatizo hili la mimba la watoto linaweza likapungua tukiwaanzisha watoto wa kike shule wakiwa na umri wa miaka mitano (5) lakini pia jambo kubwa tunataka kutafakari hapa ni kwamba:

Je, hawa watoto wako tayari kujiunga na shule wakiwa na miaka mitano? Au je, shule zilizopo ziko tayari kuwapokea watoto wakiwa na miaka mitano?

Kwa hiyo, suala zima ambalo tunataka kuimarisha sasa hivi ni umuhimu wa malezi na makuzi ya awali ya watoto, hivyo tunataka kuhakikisha kwamba masomo ya awali yanaanza na ni *compulsory* kwa watoto wote ili wakianza japo wakiwa na miaka mitatu mpaka mitano wataweza kuanza darasa la tano na wakaendelea vizuri. Wote tunatambua kwamba umri wa mwaka mmoja mpaka mitano ni umri ambapo mtoto anakua kiakili kwa asilimia zaidi ya 80, kwa hiyo, tunapoteza sana watoto wetu kwa kutowashughulisha katika umri ambao ni muhimu sana.

Hivyo tunalizingatia hilo na tunaangalia ni jinsi gani litaweza kutekelezwa katika ngazi ya kitaifa na sio katika maeneo machache ya miji mikuu peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hewa alizungumzia kwa uchungu kabisa uhalifu na ukatili wanaofanyiwa watoto wadogo. Kwa kweli hili suala tunavyolisikia inaonesha ni jinsi gani nchi yetu bado tunatakiwa tujikomboe kutokana na adui, kwa kweli katika Jamii iliyoendelea, jamii ambayo ina watu ambao wana kiwango kizuri cha elimu.

Masuala ya ushirikina unaoendana na kubaka watoto wadogo wa umri wa mpaka miaka mitatu-mitano ni mambo ambayo yanasikitisha sana, sasa tunasema kwamba suala hili si tu la kiserikali lakini pia ni la kijamii.

Si suala ambalo tutaanza kunyosheana mikono na kuweka sheria kali, lakini pia ni kutoa elimu kwa kupitia mbinu mbalimbali, kupitia viongozi wetu wa dini na taasisi mbalimbali. Kwa hiyo, changamoto kwa kweli ni sisi sote Watanzania tuone ni jinsi gani tunaweza kushiriki katika vita hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Mheshimiwa Chacha Wangwe nadhani alitaka kutufanyia tu mzaha kidogo na isitilahi wakati alipozungumza kwamba yule binti anayebakwa basi yule bwana amwoe. Sidhani kama yeye binafsi binti yake akifanyiwa hivi atakubali tu kirahisi aolewe, najua kwa mila ya Kikurya nadhani lazima angemkata panga.

Kwa hiyo, basi mimi naomba tusifanye mzaha katika masuala haya ya mimba za watoto hasa wanafunzi, ni suala gumu na baya na kwa kweli tunatakiwa wote tufanye kila jitihada kuona kabisa kwamba suala hili haliendelei na halipewi nguvu na kuanza kufanyiwa mzaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba yote nimenakili na tutayawasilisha katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na watayajibu kwa kina. Nawashukuru wote waliochangia na ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi, Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na mimi kwamba Mawaziri wamejitahidi kutoa ufafanuzi hata kama wamepata muda mfupi na wengine wanakaimu Wizara hizo. Sasa nimwite mtoa hoja, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata ya kuchangia katika Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikakati ya kuongeza ajira nchini, ni vizuri Serikali kusaidia vijana kupata mikopo yenye riba nafuu na si hivyo tu kuwasaidia kuweza kusoma *VETA* hata kwa mikopo ili waweze kusimamia shughuli zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, vile viwanda vilivyotaifishwa na havifanyi kazi kama Kiwanda cha Magunia, Moshi hata vile ambavyo havijataifishwa kama cha *Machine Tools, Moshi,* vifufuliwe ili vijana hawa wapate kazi katika viwanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na wafanyakazi wengi sana kutoka nchi za nje ambao wanafanya kazi ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania kwa mfano kazi za mahotelini, za kutandika hata vitanda, *Waiters,* wanatoka nchi jirani. Ni kigezo gani kinatumika kuajiri watu hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hizi *NGOs* ambazo zinazokuja kuisaidia Tanzania. Hawa wageni wamefanya hapa Tanzania ni mahali pa kuwapatia watu wao ajira. Wanaleta msaada lakini wanakuja kama wataalam wanajilipa mishahara mikubwa *at the end of the day* zile fedha zinarudi kule kule? Ni kwa nini kama ni *training* wasipewe muda fulani wawachie Watanzania kuendelea kufanya kazi hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vituo vya watoto yatima, ningependa kujua je, Serikali ina takwimu, kuna vituo vingapi vya watoto yatima? Mashirika mengi yamekuwa yakitumia mwanya huu kujinufaisha yenyewe. Inabidi Serikali kuhakikisha kama hivi vituo vina watoto na kama watoto hao wanatunzwa ipasavyo kwa kupatiwa chakula, malazi mazuri, elimu na kadhalika kwa sababu pia kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto wa mitaani. Ninashauri Serikali iingilie kati na kuona ni njia gani muafaka ya kutunza watoto hawa na ipitie vituo vyote vya watoto kama vinakidhi mahitaji.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kwa taarifa yake nzuri sana na yenye maelezo yanayoeleweka vizuri. Naunga mkono taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, napenda kuchangia eneo moja la majukumu ya Wizara chini ya Kamati yake, nalo ni kuhusu Watanzania waliokwama nje ya nchi na hawana uwezo wa kurudi nyumbani hasa walioko Urusi (Russia). Watanzania hao ni watoto waliozaliwa na Watanzania na kwa ndoa halali lakini hawawezi kurudi Tanzania kwa wazazi wao kwa sababu mbalimbali mfano kutokuwa na Hati za Kusafiria na kadhalika. Kamati inasema nini juu ya Watanzania hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Kamati kwa taarifa yake nzuri na mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, *NSSF* wamekwama wapi wakati fedha wanazo? Hivi ni kwa nini wawategemee Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Fedha? Mbona wamejenga majengo makubwa tu hapa nchini? Hivi maamuzi ya ujenzi wa majengo hayo nayo hutegemea maamuzi ya Wizara nyingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Kigamboni, ni kitega uchumi kwa *NSSF*, kama fedha wanazo wajenge tu, kutegemea maamuzi ya Wizara nyingine daraja hilo halitajengwa. Wakati umefika kwa taasisi zetu zenye fedha kuwekeza kwenye miundombinu kama wanavyofanya nchi nyingine hapa duniani. Hong Kong na Japan ni mifano ya nchi za kuigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba Kamati iwataje wadaiwa sugu ambao hawajalipa michango yao *NSSF* kwani kutolipa michango yao ambayo ni ya wafanyakazi wao baadaye itawaletea wafanyakazi hao usumbufu wa upatikanaji wa fedha zao za mafao mara wanapostaafu kazi. Mheshimiwa Mwenyekiti azitaje taasisi na Wizara hizo wakati wa majumuisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naungana na ushauri wa Kamati wa kueneza miradi ya nyumba za bei nafuu nchi nzima. Hata hivyo, miradi hii inapojengwa, kuhakikishwe kuwa miundombinu muhimu kama vile barabara, maji, umeme inakuwepo na pia kuwe na maeneo ya makaburi badala ya kuzitegemea Serikali za Mitaa kusogeza huduma hizo kwa wananchi. Tujifunze kutoka kwa nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, nashauri kwa wanafunzi wanaosoma kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ambao wana fani mbalimbali ama wenye fani za kufanana wajiunge pamoja na kupatiwa vifaa vya kufanyia kazi au kila mwenye fani binafsi apewe vitendea kazi ambavyo vitamwezesha kufanya miradi ya kujitegemea badala ya kupatiwa zabuni kupitia Halmashauri za Wilaya kama ilivyosahuri Kamati kwani kwa mujibu wa Sheria za Ununuzi na Ugavi *(Procurement and Suplies Act)* itazibana Halmashauri kuwapatia zabuni wanafunzi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, nakubaliana na Kamati kuhusu ushauri wao wa Serikali kuleta marekebisho ya Sheria ya Haki Miliki kwa wanamuziki ambayo itaboresha maslahi ya Wasanii wetu ambao kwa sasa wanaonufaika na sanaa hizo ni *Promoters* na *Producers*. Marekebisho hayo, napendekeza yaletwe haraka kwani hiki ni kilio cha siku nyingi, wengine wamekata tamaa na wanafanya tu hawana jinsi kwa kuwa hiyo ni fani yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, kwa kuwa hii ni taarifa ya mwaka 2006, nataka nifahamu hali halisi ya ujenzi wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo, chuo pekee nchini na kama kimepatiwa gari katika mwaka 2007.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nimpongeze Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa mjumbe wa *NEC* Mkoa. Naamini hiyo ni kutokana na uwezo wako mkubwa na upendo wako kwa watu wote bila kubagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuipongeza Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa kazi nzuri waliyoifanya ingawa taarifa ni ya mwaka 2006 lakini imeweza kwenda kama *digital* na kuingiza taarifa muhimu za mwaka 2007. Hii inaleta hamu ya kuchangia na inaonyesha umahiri wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa watumishi, tatizo hili kwa upande wangu linatokana na kutoona umuhimu wa Wizara hii na majukumu yake. Kwani kila mwaka kuna wahitimu wengi ambao zaidi ya nusu wanakuwa hawana ajira na matokeo yake kukata tamaa na taaluma yenyewe. Nashauri ifanywe tathmini ni wahitimu wangapi waliopo ambao hawana ajira, watangaziwe na endapo Serikali ipo *serious* iwachukue na kufidia upungufu huo. *If we are serious, it can be done.* Kamati isimamie suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema wakati wa bajeti, Kamati yako ihakikishe kuwa Taaluma ya Maendeleo ya Jamii ni mtambuka (*cross-cutting*), Wizara iangalie namna ya kuwasiliana na Wizara nyingine kwa mfano Kilimo, Afya, Mifugo, Maji, Mazingira, UKIMWI na kadhalika kuhamasisha na kuwaelimisha wananchi kuhusu maeneo mbalimbali. Kada ya Maendeleo ya Jamii, ina somo la namna ya kuelimisha wananchi na kuwahamasisha, hivyo watumike ili hatimaye tija iweze kuonekana na elimu mpaka kwa wale wa chini kabisa. (*grassroot level)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na wanawake na watoto, ninyi kama Kamati, wazee mnawatazamaje? Tukumbuke pasipo wazee tusingekuwepo vijana. Hebu Kamati itoe changamoto kwa Wizara kuona jinsi ya kuwaenzi na kuhakikisha maisha bora kwa kila Mtanzania yanawafikia hata hawa wazee, ahsante.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, iko haja ya Serikali kutoa upya maelekezo yanayohusu matumizi ya fedha za miradi ya UKIMWI. Fedha nyingi sana za miradi kama *USAID* na *TACAIDS* zinapelekwa kwenye Halmashauri zote nchini lakini matumizi yake hayalengi kusaidia mambo halisi, zaidi ni semina tu. Maoni yangu ni kuwa asilimia fulani ya fedha hizo zisaidie waathirika wanaoishi na virusi vya UKIMWI, wagonjwa, kuwalipia ada na *uniform* yatima na kadhalika. Baadhi ya Halmashauri zinafanya hivyo lakini baadhi hawafanyi hivyo kwa maelezo kuwa mwongozo hausemi hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *NGOs* zilizosajiliwa kisheria zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI ziwe zinapewa fedha za UKIMWI zinazopelekwa kwenye Halmashauri. Kwa sasa Halmashauri nyingi hazipendi kushirikisha *NGOs* ambazo zinafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la Usalama wa Afya Mahali pa Kazi, jambo hili ni *very serious.* Wafanyakazi wengi hasa wanaofanya kazi viwandani wanaathirika sana kiafya, wengi wamepata *T.B.* pamoja na matatizo mengine. Ombi langu:-

(a) Sheria inayohusu *OSHA* iletwe haraka ili iwe na nguvu lakini pia na mtandao mkubwa zaidi kwa nia ya kubaini na kuwafungulia mashtaka wanaokiuka Kanuni za Usalama wa Afya Kazini.

(b) Kutokana na madhara yalivyo makubwa kwa afya za wafanyakazi hasa viwandani, *OSHA* inapaswa kuwa na takwimu halisi ya watumishi wanaoathirika makazini ili kuandaliwe utaratibu wa kuwasaidia baada ya kuathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, viko baadhi ya viwanda ambavyo ni lazima mfanyakazi ataathirika tu hata hatua zote za kulinda afya zikifuatwa. Je, wafanyakazi hao wana Bima yoyote? Je, baada ya kuathirika uko utaratibu wowote wa kuwalipa kutokana na madhara hayo waliyoyapata? Watu wetu wengi wanakufa, hatua zichukuliwe haraka. Naunga mkono taarifa hii na nina shauri Bunge liipokee.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikupongeze wewe kwa heshima kubwa uliyopewa na Chama chetu baada ya Uchaguzi Mkuu kukupa kura nyingi sana na baadaye kuchaguliwa kama mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimpongeze Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kuchaguliwa kwake katika Halmashauri Kuu ya Taifa na kwa kututolea taarifa nzuri sana ya Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina machache ambayo ningeiomba Serikali ifanye yafuatayo katika kipindi kifupi:-

Serikali kwa makusudi, itoe kipaumbele kusomesha vijana wengi kwenye fani hii ya maendeleo ya jamii. Heshima ya fani hii imepungua sana, sijui ni kwa nini. Nalisema hili kwa sababu ni lazima kuwapata wahamasishaji wakuu wa maendeleo na wanaoweza kuelezea kutafsiri na kuhamasisha jamii ili kujua majukumu yao. Nani tunatarajia aelezee mipango kama:-

- *TASAF* na jinsi inavyosaidia kusukuma maendeleo.

- MKURABITA na umuhimu wa wananchi kujua namna ya kurasimisha mali.

- MKUKUTA na jinsi uchumi unavyoweza kuimarishwa.

MKURABITA na MKUKUTA pekee inahitaji waelezaji. Hata *NGOs* na misingi ya utendaji wake ni lazima kukawa na waelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sioni mwingine wa kufanya kazi hii isipokuwa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii. Kwa msingi huo, Serikali bado iombwe itoe kipaumbele kwa kada hii ya watumishi waongezwe kwa kasi kubwa ili matarajio ya Rais wetu ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania yaweze kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na ushauri wote wa Kamati hii na naiunga mkono taarifa hii na ushauri huu ufikie uongozi wa Serikali kuanzia Ofisi ya TAMISEMI, Mipango, Fedha na Wizara yenyewe.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa hongera kwa ushindi wa *NEC* kwenye Mkutano Mkuu wa CCM pamoja na walioshinda wote, kwa wale ambao kura hazikutosha, iko siku zitatosha wawe na subira.

Mheshimiwa Spika, pia kwa leo nampongeza mwasilishaji taarifa hii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, pamoja na Kamati yake yote kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naziomba Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kwa sasa chini ya Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na vionogzi wa Serikali ya Awamu ya Nne, kufanya juhudi ili Ilani ya Uchaguzi wa CCM, itekelezwe kwa vitendo na kwa usimamizi mzuri. Kwa wale viongozi au watendaji, wataalam au wananchi wasiopenda kazi zao za maendeleo ya nchi yetu waangaliwe na kama wanapitiliza kuharibu au kuangusha maendeleo yetu ya jamii, basi hatua za kazi au sheria zifuate mkondo wake. Maendeleo ya nchi ni sifa kwa nchi yetu. Elimu itolewe kwa sekta ya maendeleo ya jamii na Mabaraza yasimamie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Magogoni, naunga mkono hoja hii iliyowasilishwa kwa asilimia mia moja, ahsante.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kipengele cha wageni kufanya kazi wanapokuja hapa nchini, ni kitendo cha kusikitisha sana kwa sababu kwa kufanya hivyo, nafasi za kazi ambazo zingefanywa na wazawa zinachukuliwa na wageni. Kasoro hii inasababishwa na utaratibu mbovu unaofanywa na Idara ya Uhamiaji ama Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kutokuwa na *records* sahihi za wageni wanapoingia na kuwafuatilia ili kuhakikisha kuwa siku zinapofika za kuondoka wanaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingine zote zinafanya hivyo na kunakuwa na *control* ya wageni kinyume chake hapa nchini ni wageni kuendelea kuishi nchini hata pale vibali vyao vinapokwisha. Sekta za madini, viwanda na mahoteli, zinaongoza kwa kuwa na wageni haramu ambao wanafanya kazi bila vibali.

Aidha, katika mwaka 2003, Wizara hiyo ilijaribu kufanya msako wa watu wa aina hiyo na hata walipokamatwa, ilishindikana jinsi ya kuwarudisha kwa sababu wengi wao walijikuta hawana *tickets* za kurudia kwao. Wakati huo huo, Serikali ilikosa fedha za kuwasafirisha. Nadhani ni vema sasa kwa Wizara hizo kuwa na udhibiti mkali kwa kuhakikisha kila mgeni anapoingia nchini anakuwa na *ticket* ya kurudia na pia Wizara kuwa na *records* za tarehe za kurudia ili kuwa na urahisi wa kuwafuatilia. Hiyo, inawezekana tu kama *entry forms* za kuingilia wageni zitaboreshwa kwa kuweka vipengele vya kuwabana wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi wanakosa wasaa wa kuendelea na michezo kutokana na tatizo la kukosekana kwa viwanja vya michezo. Serikali ichangie na kusimamia ujenzi wa viwanja kuanzia Wilaya hadi Mikoa. Vile vile, Ofisi za Utamaduni nazo ziwe na Maofisa wenye tija na michezo na wahamishaji wazuri. Tofauti na hali ilivyo sasa Maafisa Utamaduni hawahamasishi michezo kitendo kinachowafanya vijana kuzurura tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watoto yatima, ninapendekeza kwa makusudi mazima, Serikali ijenge vituo vya kulea watoto yatima na kuvisimamia ipasavyo. Sasa hivi kazi hiyo ya kusaidia watoto yatima na walemavu imeachwa kwa wanasiasa kama vile Wabunge kuwahudumia na wakati mwingine kuwasomesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Nianze kwa kutoa pongezi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Jenista Mhagama, kwa taarifa nzuri ambayo inaigusa jamii inayoendelea na ile iliyo mbioni kuendelea, hii inaendena na usemi wa maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za pekee, ziwaendee Mawaziri wote walioshiriki kukiboresha Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Misungwi, Mheshimiwa A. Migiro na Naibu wake, pia Waziri Mheshimiwa Sophia Simba na Naibu wa awali Mheshimiwa Dr. B. Buriani na kwa shukrani za pekee ziende kwa Naibu Waziri, Marehemu Salome Mbatia aliyekitembelea Chuo cha Misungwi na kuongea na watumishi na kuahidi kuyafanyia kazi yale matatizo yaliyojitokeza ambayo yanakwamisha utendaji kazi katika chuo hicho. Wana Misungwi walilia sana kusikia Naibu Waziri wao amepata ajali na kufariki. Wanamuombea kwa Mungu roho yake ilazwe mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Waziri alitembelea Chuo hicho hivi karibuni naye alijionea na katika majibu aliyonipa ni kukamilisha ukarabati uliobaki na pia kumalizia suala la samahani katika chuo chetu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara ikumbuke kukamilisha ukumbi wa mikutano ambao utasaidia sana mikutano mbalimbali hasa ile ya wanachuo kutokana na chuo kupanuka na kupendwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa chuo hiki sasa hivi kinazidi kupanuka, kwa nini kisiwe chini ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ili kiendelee kutoa mafunzo kwa Mkoa mzima kama ilivyo kwa vyuo vya *Arusha Technical, Mbeya Technical* na Dar *Technical?* Hii itasaidia sana kwa Kanda ya Ziwa.

Naomba sana Wizara inayohusika ishughulikie suala hilo. Mfano ni kama Chuo cha Ushirika, Moshi, kilikuwa chini ya Wizara ya Ushirika 2003, tulikiruhusu kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu *UDSM.* Hivyo, hata kwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii kuwa chini ya Wizara ya Elimu ya Juu kwa kuanzia ni sahihi, naomba hilo likubalike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kuipongeza Kamati kwa kutembelea Jimbo langu na kuishauri Serikali mambo mengi ambapo mengine yametekelezwa ikiwemo vitendea kazi kama vile gari ya ofisi na vingine vingi. Naahidi ushirikiano na Wanakamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, nashauri wapatiwe zabuni. Nashauri vijana au vikundi hivi wanapomaliza mafunzo katika vyuo husika na kupata matokeo mazuri, washauriwe kupeleka matokeo hayo kwenye Halmashauri zilizo karibu nao ili waweze kutambulika ni fani ipi amefuzu ili Halmashauri hiyo iwe na kumbukumbu hai ofisini ili pindi mhusika anapoomba zabuni fulani, ofisi iwe na kurejea kumbukumbu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *SACCOS*, idadi ya *SACCOS* Kenya ni kubwa mara kumi yetu. Je, ni sababu gani ambazo zinasababisha utofauti huo ili hata kama Wabunge mnatuhamasisha ili nasi tukawahamasishe wananchi inabidi tujue ili tukapambane vizuri, ahsante.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi sasa ya kuweza kuhitimisha hoja yangu kwa niaba ya Kamati yangu ya Maendeleo ya Jamii ambayo tumeanza kuizungumza toka asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafanya hivyo kwa heshima na taadhima kabisa, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge wote waliochukua nafasi yao ya ziada kuhakikisha kwamba wanatoa michango yao mbalimbali, aidha kwa maneno au maandishi ili kuweza kuboresha hoja yangu ambayo niliiweka mezani kwako leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maneno wako Waheshimiwa Wabunge (16) ambao ni Dr. Binilis Mahenge, Mheshimiwa Annie Chaurembo, Mheshimiwa Hafidh Ali, Mheshimiwa Lediana Mng’ong’o, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Benadete Mshashu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimwa Rose Kirigini, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Maria Hewa na msemaji wa mwisho alikuwa Mheshimiwa Chacha Wangwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale waliochangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Elietha Switi, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, na Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, hao walikuwa ni wachangiaji (11).

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba kwa kweli nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, naamini kabisa wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia ama kwa maneno au kwa maandishi basi wataendelea kuwasiliana na Kamati yetu ili kuweza kuboresha shughuli zetu kwa taarifa ambayo tutaitoa katika mwaka ujao kwa maana ya kwamba mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapokea kwa heshima kubwa pongezi nilizopewa na wachangiaji mbalimbali na hasa kushinda kwangu kuchaguliwa kuwa mjumbe wa *NEC* kupitia mkoa wa Ruvuma. Nitaziwasilisha salamu hizo kwa wanachama wa Chama cha Mapinduzi kule mkoani kwangu, lakini vilevile nawashukuru Wabunge kwa kunipongeza kuongeza Bunge lako tukufu hasa wewe na Mheshimiwa Spika msipokuwepo. Nawashukuru sana lakini wao ndiyo wanaonipa ushirikiano wa kutosha na hivyo kuweza kufanya kazi zangu kwa umakini ambao wameuelezea leo hapa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana kwa kutambua umuhimu wa Kamati hii ya Maendeleo ya Jamii. Kamati yetu kama ilivyoelezwa na Wabunge wengi ni Kamati mtambuka, imeweza kuunganisha Wizara tatu ambazo zimeelezwa na kutolewa maoni mbalimbali na kutolewa maoni mbalimbali na Kamati na Waheshimiwa Wabunge kama ilivyojionesha lakini inabeba dhana kubwa sana ya azimio la kuendeleza jamii katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa maendeleo ni wa lazima na ukizingatia kwamba maendeleo peke yake ndiyo yatakayoondoa agenda ya umaskini. Umaskini sio ugonjwa na wala hauambukizwi lakini cha kushangaza ni kwamba kila Mtanzania ana umaskini wa aina yake ambao haufanani na jirani yake wala rafiki yake, na hivyo juhudi za kupambana na umaskini huo ni za kwetu sisi sote kwa pamoja tukianza na Serikali yetu, jamii nzima na wadau mbalimbali na hivyo basi baada ya muda tunaweza kujikuta kwamba jamii hii ya Watanzania imeweza kuendelea na kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo usemi unaosema kwamba moto huwaka kule kulikobakia kichaka, kwa hiyo basi haya tuliyojifunza leo ni yale yaliyojitokeza katika mwaka wa 2006 lakini katika mwaka wa 2007 tunaamini kabisa kwamba ripoti yetu ya Kamati itaonesha mwelekeo mzuri wa kiutekelezaji na kiutendaji wa Serikali lakini pamoja na Kamati nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo yaliyojitokeza na kupitia Kamati na kupitia Waheshimiwa Wabunge, lakini nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wakiongozwa na Waziri wa Nchi, ambao wametusaidia sana kujibu michango ya hoja mbalimbali za Wabunge. Labda mimi tu niseme kwamba yale yote yaliyotolewa maelekezo na Serikali yamepokelewa mbele ya Bunge lako lakini sisi kama Kamati itatupasa kuendelea kusimamia utekelezaji wa haya yote yaliyojibiwa na Serikali hapa ili kujua kama kweli yataweza kufanyika na kumsaidia mwananchi wa Tanzania kupata maisha bora.Tutapenda kujua muda na wakati muafaka wa kuanza kwa shughuli hizo na kukamilika ili kupima utekelezaji wenye tija katika haya yote ambayo yameelekezwa mbele yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba wapo Waheshimiwa Wabunge wengine walishangaa. Baadhi ya taarifa hazikujitokeza kwenye Kamati yetu, na mimi naomba niwaambie kwamba utendaji wa Kamati ulijigawanya katika matukio mbalimbali na yale ambayo Waheshimiwa Wabunge walifikiri kwamba ni kwa nini hatukuweza kuyazungumza, naamini kabisa yatajitokeza katika taarifa yetu itakayofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, makubwa ambayo yametolewa maelezo ya kina, kwa mfano suala zima la ujenzi wa daraja la Kigamboni, tunaendelea kusisistiza kwamba kwa kweli lipewe muda wa kuanza na kukamilika. Tunajua kwamba Serikali inaendelea na mchakato lakini mchakato utakwisha lini na daraja litakwisha lini? Kwa hiyo, hayo ni mambo ya msingi. Yapo yaliyojitokeza kwa mfano sera ya kushughulikia mifuko ya hifadhi ya jamii nchini. Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza vizuri na naamini katika ripoti yetu ya Kamati ya mwaka 2007 tutatoa taarifa kwa kweli hali inaendelea vizuri.

Wapo wengine wamesisitiza kabisa maswala ya Sheria zilizopitwa na wakati. Nakubaliana nao na Kamati imefanyia kazi ya kutosha sana eneo hilo. Kwa mfano, tumezungumzia Sheria ya *OSHA* na Mheshimiwa Naibu Waziri amesema namshukuru sana, na sisi kama Kamati tumeendelea kuisimamia na naamini kwamba taarifa ya Kamati itakayofuata itatoa picha halisi ama pia Sheria inayohusu hakimiliki kwa wasanii na wanamuziki hiyo pia nayo italetwa mbele ya Bunge lako hivi karibuni na itaweza kushughulikiwa. Vilevile, Mheshimiwa Suzan alizungumza sana suala zima la sheria zinazowakandamiza Wanawake na kuwanyayasa watoto. Naamini hilo ni eneo lingine ambalo Kamati yetu itabidi ilisimamie kwa nguvu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo mifano ya sheria ambazo kwa kweli zimepitwa kabisa na wakati na tungeomba Serikali kupitia Waziri wa Nchi tunapofanya mabadiliko ya Sheria nyingine tuona umuhimu Sheria hizi nazo zipewe kipaumbele. Mara nyingi tumekuwa tukiangalia Sheria nyingi tunazileta lakini hizi zinazohusu Wanawake na watoto hazijapewa kipaumbele kwa kiasi cha kutosha. Kwa mfano, kuna Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ambayo inamruhusu mtoto wa miaka 14 kuolewa, sasa inapingana kabisa na Katiba yetu na mikataba mbalimbali ya kimataifa abayo sisi pia kama nchi tumekuwa tukiiridhia. Mtoto

wa mika 14 hayuko tayari katika suala zima la uzazi, kwa hiyo, unaona kabisa kwamba ni kweli watoto wamekuwa wakikandamizwa kwa namna moja ama nyingine. *(Makofi)*

Kwa kuwa Sheria hiyo ya ndoa inamruhusu mtoto kuolewa, mtoto anayeolewa kwa mika 14 sisi wanawake tunajua ni matatizo makubwa kiasi gani atayapata kwa kuanza kuwa mama katika umri huo mdogo wa miaka 14. Masuala ya uzazi yatampa shida na mambo mengine mengi tu ya kindoa yatamsumbua sana mtoto huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo Sheria pia ya kulea mtoto nje ya ndoa ya mwaka 1949. Toka mwaka 1949 haijabadilishwa, kifungu cha (5) kinachekesha, kinasema kwamba Baba wa mtoto anapaswa kulipa kiasi cha shilingi 100/- kwa mwezi kama gharama za matibabu, elimu na matunzo ya mtoto. Sasa shilingi mia moja kwa mwezi huyo mtoto anayelelewa nje ya ndoa kwa shilingi hizo mia moja kwa mwezi sijui ananunua kitu gani. Sehemu ya sita ya Sheria hiyo inaweka ukomo wa huduma ya huyo Baba kwa mtoto wake na inasema kwamba mtoto akifikia umri wa miaka 16 hiyo shilingi mia moja haitaendelea kutolewa tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa mazoea yetu sisi Waafrika, mtoto anaendelea kuwa wako mpaka pale atakapoanza kujitegemea, kwa hiyo, wale watoto walioko ndani ya ndoa wanafaidi hiyo *hospitality* ya wazazi, lakini kama ni wa nje ya ndoa akifika miaka 16 hata hiyo shilingi 100/-hatakiwi tena kuipata. Kwa hiyo, naona Sheria kama hizi bado kwa kweli hazikidhi mahitaji, ama Sheria hiyo kifungu cha (6) inaendelea kusema kwamba, mara tu mama akishaolewa na mume mwingine basi hizo fedha hazitatolewa tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mama huyo mtoto wake ana miaka mitano lakini akapata mwenzi wa kumwoa, kwa hiyo, baba haulizwi kwa nini tena hapeleki fedha kwa ajili ya matunzo kama ni mtoto wa nje ya ndoa. Sheria hizi zina umuhimu wa kuletwa katika Bunge letu haraka iwezekanavyo ili kuweza kutoa haki sawa kwa watoto na kwa akinamama.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu nimalizie na mfano mwingine. Ipo Sheria nyingine ya mirathi ya kimila, Tangazo la Serikali Namba 436 la mwaka 1963. Sheria hiyo ni ya mirathi ya kimila ambapo inatoa kipaumbele kwa watoto wa Kiume kurithi mali nyingi zaidi kuliko watoto wa kike na Sheria hiyo hiyo inamtaka mjane atunzwe na watoto wake na sio mali iliyoachwa na Mume wake, tena watoto wenyewe hapo nadhani ni wa kiume siyo wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali kabisa kwamba Kamati yetu bado ina kazi kubwa ya kusaidiana na Serikali yetu na inaonesha nia ya kuhakikisha kwamba inatoa msaada wa karibu ili kutengeneza usawa huu wa kijinsia katika maeneo mbalimbali na mimi niseme kwamba tunapopiga kelele na kuomba Serikali iongeze bajeti katika Wizara zote hizi tatu na hasa Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii tuna maana kubwa. Tunasema tunataka kujenga usawa wa kijinsia hatutaki kusema kwamba tunataka wanaume wawe nyuma, wanawake wawe mbele hapana!

Usawa wa kijinsia kwa maana ndogo tu kwa mfano, kila siku tumekuwa tukihangaika, akinamama wanafanya kazi nyingi sana maeneo ya vijijini na wangependa wapunguziwe kazi na hasa wanapokuwa wajawazito wanakuwa na majukumu mengi ya kulea. Mwanaume hawezi kupika kwenye jiko la mafiga matatu hata siku moja kule kijijini lakini kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii ikiongezewa fedha za miradi ya maendeleo ikatafuta uwezekano wa kuanzisha jiko angalau refu kidogo la *stove* baba atapenda kupika kwenye jiko lile kuliko lile la mafiga matatu. Na hapa *automatically* ule usawa wa kijinsia utaanza kuwa *practised* ama kwa upande mwingine, akina baba kubeba mzigo wa kuni kichwani haiwezekani kabisa Mheshimiwa Naibu Spika!

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Wangwe hakukuelewa kabisa hapo……! *(Kicheko)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, ama kubeba mzigo wa kuni kichwani, mwanaume hawezi kubeba mzigo kichwani, lakini

kama Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto ikawezeshwa fungu la fedha, wakatengeneza teknolojia labda ya toroli la namna fulani ambalo litamfanya mama aweze kubeba mzigo wa kuni kwenye toroli, nakuhakikishia toroli hilo litatumiwa na baba na wala sio mama, na *automatically* utakuwa umemfanya baba amsaidie mama kwa kupunguza kazi nyingine za shuruba katika mazingira aliyonayo. Hapo ndipo tunapojenga hoja kwamba Wizara ya Maendeleo ya Jamii iongezewe fedha ili iweze kweli kuonesha kwa vitendo ni namna gani usawa wa jinsia unaweza ukaja bila kugombana na bila kusahau agenda ya *fifty fifty*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee tu kusema kwamba tunaendelea kushukuru kwamba Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana imesimamia vizuri sana suala zima la fedha za kuiwezesha jamii. Na yapo mambo mawili matatu yamejitokeza Mheshimiwa Waziri ameyajibia na Waheshimiwa Wabunge wangetaka kufanyiwa marekebisho. Naamini kwamba Kamati itaendelea kuzingatia yale yote yaliyojadiliwa hapa ndani ili kuweza kuboresha huo mfuko wa uwezeshwaji jamii, na hasa kuwakuta wananchi wa vijijini wale wakulima, wafugaji ambao ndiyo hasa wanatakiwa kuwezeshwa na karibu pato kubwa la taifa linategemea kilimo, ufugaji na sekta za namna hiyo. Kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, mkakati wa awamu ya pili unaweza ukatusaidia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* imepongezwa sana na mimi nakubaliana kama Mwenyekiti wa Kamati, nimeona kazi nzuri zinazofanywa na Shirika hilo na sisi tunaendelea kuwapa nguvu na moyo. Tunaamini kabisa kwamba huko mbele kwa kweli shirika hili linaweza kufanya mambo makubwa sana ndani ya nchi yetu ya Tanzania, kwa hiyo, tunawapongeza na mimi ninapokea pongezi za Waheshimiwa Wabunge na kwa kweli wanafanya kazi vizuri .

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kuvipa hadhi Vyuo vya Maendeleo ya Jamii nadhani imezungumzwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri wa Nchi na ameitolea maelezo kwa niaba ya Wizara na nafikiri tu kwamba maendeleo na msingi wa mapinduzi ya viwanda katika nchi yeyote kwa kweli yalianzia na mafundi hawa wadogo wadogo. Kwa hiyo, na sisi tunaamini hawa mafundi wakitoka katika *clusta* ile ya maendeleo ya jamii wakaingia katika ufundi stadi kwenye *VETA* na baadaye wakaweza kuingia kwenye ufundi mwingine mkubwa na wakasimamiwa vizuri hawa ndiyo watakaoleta mabadiliko ya maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Nchi na ninaomba kwa kweli eneo hili kwa niaba ya Kamati kama tulivyokubaliana lifanyiwe kazi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo lilijitokeza ambalo nadhani sisi pia tulichukue na tuendelee kushauriana na Wizara husika, ni suala la fedha ambazo zinatolewa kwa ajili ya miradi mbalimbali ya UKIMWI. Kumekuwa na fedha nyingi sana katika nchi yetu sasa hivi zinatolewa kwa ajili ya kusaidia tatizo hili la UKIMWI lakini matumizi yake yamekuwa si ya kuwiana na hayaendi sambamba kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Simbachawene, aliomba kwamba itengenezwe sera maalumu ama mpango maalumu ili fedha hizi za wafadhili zinavyofika kwenye Halmashauri zetu zitumike moja kwa moja kusomesha wale watoto yatima watakaokuwa wametambulika. Zitumike kuwalea wale wajane na wagane, na zitumike vilevile katika kuhakikisha wagonjwa na waathirika wa UKIMWI wanawake kwa wanaume wanapatiwa chakula bora. Kwa hiyo, nadhani hili nalo tuliweke kweye Serikali yetu ili miongozo hii ikifika kwenye Halmashauri zetu na yote ikafanana inaweza kusaidia, kwa sababu fedha hizo ni nyingi kutoka kwa wafadhili na zimekuwa zikija kwa wingi sana katika Halmashauri zetu .

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Beatrice Shelukindo, alikuwa anashangaa, hivi wazee ni mali ya nani mbona Mheshimiwa Mwenyekiti hujawasema katika taarifa yako? Naomba niseme kwamba kikamati wazee si mali ya Kamati yangu, lakini kijamii wazee ni wetu sisi wote, kwa hiyo, wote tunatakiwa tushirikiane katika kuona tunawalea na tunawahudumia. Mheshimiwa Rose Kirigini, ameiomba Kamati yangu ihakikishe inafika katika Chuo cha Buhare, naomba nimthibitishie kwamba nitatekeleza hilo na tutaliweka kweye programu yetu ijayo ili tuweze kuja na tuone tunaweza kusaidiana namna gani katika kuhakikisha tunasaidia na Chuo hicho pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala jingine ambalo lilitiliwa msisitizo sana na Mheshimiwa Paul Kimiti na yeye alikuwa anapenda sana kuona kwamba Wizara hizi ambazo zinahusika na uwezeshaji jamii,

Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, na Wizara hii ya Wanawake, Jinsia na Watoto, zione umuhimu wa kusimamia miradi ile mikubwa na kuona kwamba watumishi wa sekta hizo ndiyo wanakuwa waelezaji wa maendeleo kupitia miradi kama ya *TASAF*, MKURABITA, MKUKUTA na miradi mingine mikubwa ya namna hiyo kwa sababu hiyo ndiyo inayolenga kuikomboa jamii. Nakubaliana kabisa na ushauri wa Mheshimiwa Paul Kimiti na ninadhani katika vikao vyetu vya Kamati tutaona ni namna gani maafisa wetu wa maendeleo ya jamii watachukua jukumu hilo kwa pamoja ili kuweza kusaidiana na Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mama Hewa, alikuwa ameiomba Kamati iangalie hivi ni kwa nini hizi *NGOs* zisipunguzwe, lakini naomba tu nimwombe mama Hewa akubali ziongezeke kwa sababu sasa hivi majukumu ya Serikali kwa kweli ni kupunguza kazi kutoka kwenye mkono wa Serikali na kuwaacha watu binafsi wazifanye. Lakini tusisitize tu kwamba Serikali iendele kuvaa miwani na kuwa na macho makali ya kusikiliza na kuziangalia zinafanya kazi kwa kiasi gani kwa manufaa ya Watanzania na sio kwa manufaa ya mashirika hayo ambayo si ya Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kurudia lakini tumepokea kwamba msisitizo mkubwa umewekwa katika ajira za kigeni, tutaendelea kufuatilia kuwa linatekelezwa namna gani kama vile Waziri alivyosema. Hoja ya watoto yatima waliopo vituoni, waliopo majumbani na wale walipo katika mazingira magumu tunapokea, na Kamati itaendelea kufuatilia kwa kiasi kikubwa na kutoa taarifa Bungeni. Hoja ya *NGOs*, hoja ya uhaba wa Maofisa wa Maendeleo ya Ustawi wa Jamii, hoja ya masuala ya Utamaduni, hoja ya masuala ya michezo mashuleni na kadhalika, naomba niseme kwamba kwa kuwa Naibu Mawaziri wamejibu hoja hizo vizuri lakini bado niseme sisi kama Kamati tutaendelea kuzichukua, tutazisimamia, na tutashirikiana na Serikali na kuona haya yote yaliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge yanaweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwandishi mmoja Robert Green aliyetunga kitabu kinachoitwa 48 *Laws of Power* amesisitiza sana kutimiza maagizo yote kwa kufanya matendo kupitia *demonstration* na *actions.* Kwa hiyo, naamini kabisa kama Kamati yetu itajitahidi kufanya kazi na Serikali kwa kufanya matendo yakinifu yatakayoonekana ku-*deliver* maendeleo kwa wananchi wetu wa Tanzania kwa kweli jinsi tulivyoanza na jinsi Serikali yetu ya Awamu ya Nne inavyofanya kazi kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya haya yaliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge yakitekelezwa naamini kabisa tutafika mahali ambapo tutawaondoa wananchi katika umaskini na kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana ipo michango ya Waheshimiwa Wabunge wengine tumeshindwa kuisema moja kwa moja na hasa kwa kuwataja kwa majina, lakini niwahakikishia tu kwa kweli nimejitahidi kuandika kila kilichosemwa. Na wale walioleta michango yao kwa maandishi tumeipokea na tumeiweka na naamini yote itaonekana kwenye *Hansard* yako, lakini kama kumbukumbu ya Kamati yetu itaendelea kubakia kwa kutusaidia kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwanza, kwa kunisikiliza lakini pili kwa kuchangia mada hii, imekuwa na wachangiaji wengi. Hoja yetu ya leo na mimi kwa kweli sikuweza kuamini kama Waheshimiwa Wabunge wangeweza kuwa na hamu ya kutusaidia na kutoa ushauri katika Kamati yetu. Kwa hiyo, niwashukuru sana na niwahakikishie ushirikiano katika kuchangia shughuli zingine zozote zinahusu Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii ambayo ina Wizara tatu ndani yake.

Naomba nikushukuru sana kwa kuongoza kikao cha leo vizuri na hasa mimi nilipokuwa nikitoa hoja yangu kwa siku hii ya leo, lakini pia niwashukuru Makatibu na hasa nimshukuru Katibu wangu na Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ndani ya Kamati yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hiyo, yaliyotolewa na kuchangiwa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali katika siku hii ya leo. Naomba kutoa hoja.

**MHE. HAROUB MASOUD:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA**: Mbona mnasimama kwa wasiwasi, wadau wote mnapaswa kusimama hasa Wajumbe wa Kamati hiyo kwa sababu aliyoyasema Mwenyekiti ndiyo ya kwenu. Kwa hiyo, mnapaswa kusimama bila kukaa, kama vile Serikali wakitoa hoja yao wanasimama basi na ninyi ni hivyo hivyo (*Kicheko*).

Mimi binafsi napenda niseme kwa hakika kabisa kumekuwa na kazi nzuri kabisa imefanywa na ninyi Waheshimiwa Wabunge kuijadili hoja hii, Mawaziri waliohusika kuzijibu hoja zile hata kama ni muda wa dakika 15, nafikiri wamejibu vizuri sana na Mwenyekiti mwenyewe naye amejibu vizuri sana hoja na wengine tuliokuwa wasikilizaji tumepata moyo zaidi. (*Makofi*)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa mwaka 2006 ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nina tangazo dogo tu, nafikiri asubuhi nimetangaza kwamba semina itakuwa siku ya Jumapili katika ukumbi wa Msekwa saa 5.00 tarehe 11, lakini pia naomba Kamati ya Mheshimiwa Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na biashara anaomba niwatangazie Waheshimi Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuwa kesho tarehe 10 kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika saa 4.00 asubuhi katika Ukumbi Namba 432. Wenyeviti wengine pia wamepewa maazimio kwa ajili ya wiki ijayo, nadhani nao watatoa taarifa zao wakati mwingine.

Naomba niwashukuru sana na naomba hii iwe *recorded* kabisa kwa wananchi wote. Wiki hii tumemaliza Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi na Viongozi wamechaguliwa. Mme-*notice* kwamba pongezi zimetolewa kutoka vyama vyote Bungeni kwa wale walioshinda, hata wenzetu wa Kambi ya Upinzani wamekipongeza Chama. Mimi nadhani hiyo ndiyo *spirit* ambayo inatakiwa iwe ndani ya Nchi.

Kuwepo kwa Vyama vingi sio uhasama na nadhani Bunge linaonesha mfano kwamba mara nyingi tunakuwa vyama tofauti lakini tupo kama kitu kimoja. Kwa hiyo, sisi tumepata moyo sana wa Chama cha Mapinduzi kwamba tunao wenzetu ambao wanatambua kuwepo kwetu sisi wote ni kwa ajili ya maendeleo ya Nchi na si vinginevyo. Kwa hiyo, naomba ushirikiano huu tuendeleze nao wateja wetu ni wamoja, ni Wananchi, hivyo tujitahidi kila mara kwani urafiki wetu na umoja wetu ndiyo utafanya wananchi wajisikie ni wamoja. Naomba niwapongeze sana ndugu zetu wa vyama vya upinzani kwa kuona kwamba wenzenu tumemaliza mkutano na ninyi mkimaliza tutawapongeza hivyo hivyo na hivyo ndivyo tutakavyoongoza nchi yetu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Spika jana alieleza kwamba leo angetoa ufafanuzi kuhusu mambo ya usalama pale kwenye geti, hatujakamilisha kwa hiyo, hatuna kikubwa cha kuwaambia. Hatujakamilisha kwa sababu tulikuwa tuwasiliane na watu wengi zaidi, pengine wiki ijayo mapema tutakuwa na kauli ya kusema.

Waheshimiwa Wabunge, vinginevyo, naahirisha kikao mpaka Jumatatu saa 3.00 Asubuhi.

*(Saa 1.35 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 12 Novemba, 2007 Saa 3.00 Asubuhi)*